# Nipashe

Jumatano Machi 4, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580170

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

MWANGA WA JAMII




## Abiria walia kutelekezwa kwenye daraja lililokatika

UKURASA 2


Sudan inavyoonja shubiri ya wafadhili ikijikwamua
Ukurasa 20
Jambo la 50/50 Uchaguzi 2020
Ukurasa 19
siasa
JUMATANO MACHI 4, 2020
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
Ukurasa 18
Kifuatacho baada ya BVR kiwe mafunzo elimu uraia
'Safari ya matumaini' tarajiwa ya kada Membe inaishia wapi?
Na Ani Jozeni
KUNA msemo wa falsafa kuwa historia inajirudia, lakini siyo kwa mazingira yale yale. Baadhi ya wanafasihi wanasema mara ya kwanza tukio hilo la kihistoria linakuwa ni mkasa, ila linapojirudia inakuwa ni mzaha.
Ndivyo ambavyo inawezekana tukio la uchaguzi mkuu uliopita lijirudie mwaka huu, lile la 'safari ya matumaini,' kutokana na mtangaza nia mahiri uchaguzi wa mwaka 2015 Edward Lowassa, 'kukatwa' na chama chake. Safari hii kilichokatwa si jina la mtangazania ila la mwanachama mkongwe kufukuzwa na chama chake cha Mapinduzi -CCM, anayefukuzwa ni Bernard Membe.
Hata hivyo kinachowapasua vichwa baadhi ya watu ni hatma ya kada Membe, je itakuwaje?
INAENDELEA UK.16
Bernard Membe. PICHA: MTANDAO
Ukurasa 17
Netanyahu adai kushinda uchaguzi uliofanyika Israel
Utaratibu huu utazima wanaotumia mlungula Ukurasa 14

UKURASA 13

# Walichoteta JPM, Maalim Seif Ikulu

**MAZUNGUMZO** yawahusisha pia Profesa Lipumba, Mbatia... *Endelea ukurasa wa 2*



## GWAJIMA AHOJIWA POLISI UKABILA

UKURASA 2



Rais John Magufuli akisalimiana na mwanasiasa mkongwe ambaye ni mshauri wa Chama cha ACT- Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kugonganisha miguu bila kushikana mikono, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. Salamu hiyo ni kutekeleza ushauri wa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu wenye lengo la kujihadhari dhidi ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona. **PICHA: IKULU**

## Ubunge Simanjiro waibua balaa CCM

UKURASA 11




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play | Download on the App Store


## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**MAJALIWA: WALIOFUJA MALI MKONGE KUKIONA**



WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itawachukulia hatua watu wote waliohusika na ubadhirifu wa mali zikiwamo nyumba za Mamlaka ya Mkonge Tanzania...

UKURASA WA 4

**UMEME MEGAWATI 80 KUANZA MWAKANI**

BODI ya Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) inatarajia kupokea umeme wa mradi wa maporomoko ya Mto Kagera ya Rusumo, unaojengwa katika Kata Rusumo wilayani Ngara mkoani Kagera ifikapo mwaka 2021.

UKURASA WA 3

**DC ASHANGAA WAFU KUMDHAMINI KARANI**

MKUU wa Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, Deodatus Kinawilo, ameshangazwa na kitendo cha karani wa Chama cha Msingi cha Ushirika...


**MICHEZO** SIMBA: AZAM FC DARAJA LA YANGA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Walichoteta JPM, Maalim Seif, Lipumba, Mbatia

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS John Magufuli jana alikutana na kufanya mazungumzo na wanasiasa watatu; Maalim Seif Sharif Hamad, Prof. Ibrahimu Lipumba na James Mbatia, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Baada ya mazungumzo hayo, Maalim Seif Sharif Hamad ambaye aliwahi kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alisema yeye na Rais Magufuli walizungumzia masuala ya kudumisha amani, usalama na upendo kwa watu wote.

Alisema amefurahishwa na dhamira ya Rais Magufuli kukutana na viongozi mbalimbali na kujadiliana mambo yenye maslahi kwa nchi.

Prof. Lipumba ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), alimpongeza Rais Magufuli kwa ahadi yake kuwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu utakuwa huru na wa haki.

Mtaalamu huyo wa uchumi pia alipongeza juhudi zinazofanywa na serikali kupambana na rushwa, kudhibiti matumizi ya serikali, kulinda na kutumia vizuri rasilimali za taifa, kuboresha elimu na kuimarisha uchumi.

Prof. Lipumba alitoa wito kwa Watanzania wote kuweka uzalendo mbele na kudumisha amani na utawala bora, huku akiwataka wanachama wote wa CUF kujiandaa kushiriki Uchaguzi Mkuu utakaofanyika baadaye mwaka huu kwa kufuata taratibu na sheria zilizopo.

Aliwakosoa wanasiasa wanaopinga kila jambo linalofanywa na serikali, akisema serikali ya awamu ya tano imetekeleza vizuri mambo mengi yaliyokuwa yakisemwa na vyama vya upinzani, hivyo siyo sawa kwa vyama hivyo kupinga jambo vilivyotaka litekelezwe na linatekelezwa, akitolea mfano kurekebisha Sheria ya Madini na kupambana na rushwa.

Kwa upande wake Mbatia, mbali na kufurahishwa na dhamira ya Rais Magufuli juu ya Uchaguzi Mkuu kuwa huru na wa haki, aliwataka wanasiasa waache kukamiana na kuchochea mambo hasi dhidi ya taifa, badala yake waungane kuendeleza mambo mazuri yanayofanywa na serikali ikiwamo kuboresha elimu, upatikanaji wa nishati na mengine yenye maslahi mapana kwa wananchi.

Mbatia alitoa wito kwa wanasiasa na Watanzania wote kwa ujumla kuweka mbele maslahi ya taifa badala ya kukumbatia mambo yenye maslahi binafsi.

Aliipongeza serikali kwa kufanya vizuri katika maeneo mbalimbali licha ya kwamba wapo baadhi ya watu wanaobeza mafanikio hayo.



Askofu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima (kulia), akitoka katika Kituo cha Polisi Kati, baada ya kuhojiwa na Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam jana, kwa tuhuma za kusambaza kipeperushi na sauti kwa lugha ya Kisukuma zenye lengo la kuhamasisha watu kuunda kikundi cha kikabila nchini. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Gwajima ahojiwa polisi kwa tuhuma za ukabila

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limemhoji Askofu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, kwa tuhuma za kusambaza kipeperushi na sauti kwa lugha ya Kisukuma kuhamasisha watu kuunda kikundi cha kikabila nchini.

Taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Camillius Wambura, ilidai kipeperushi hicho chenye picha ya Rais John Magufuli kimesambaa kwenye mitandao ya kijamii kikiwa na maandishi yanayosomeka kwa lugha ya Kisukuma.

Katika taarifa yake hiyo, Kamanda Wambura alisema Askofu Gwajima pia ametoa ujumbe wa sauti wenye ujumbe wa kumpongeza Rais na kuhamasisha Wasukuma kurejesha utamaduni wao wa zamani wa kutumia lugha yao, kusaidiana katika shida na raha na kuwataka waunde vikundi kwenye mitandao ya kijamii vya watu 2,000 kwa lengo la kufuatilia watu wanaomtukana Rais na kuwashughulikia.

"Katika ujumbe huo wa sauti, Askofu Gwajima pia amewataka Wasukuma matajiri kuungana kwa pamoja kwa lengo la kuwasaidia Wasukuma maskini ili kuondoa dhana ya kwamba Wasukuma ni maskini na ni washamba.

"Kufuatia ujumbe huo, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limemhoji Askofu Gwajima kutokana na ujumbe huo kuonekana kuhamasisha vitendo vya kikabila, jambo ambalo linaweza kuwagawa Watanzania na kupelekea kuvunjika kwa amani na mshikamano wa nchi utakaotokana na uwapo wa matabaka ya kikabila.

"Baada ya mahojiano hayo, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limemuonya Askofu Gwajima na kumtaka kuacha mara moja vitendo vya kuligawa taifa kwa kutumia vigezo vya ukabila na kutoa onyo kwa wote wenye nia ya kutaka kuligawa taifa kwa njia ya ukabila, udini au ukanda.

"Jeshi la Polisi halitamwonea muhali mtu yeyote atakayebainika kujihusisha na vitendo vya aina hiyo na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao," Wambura alisema.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alisema wanatoa wito kwa wananchi kuendeleza umoja na mshikamano uliopo nchini bila kujali dini, kabila wala rangi ya mtu kama ambavyo Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alivyopinga vitendo vya kibaguzi na kutunganisha kuwa wamoja kwa lugha ya Kiswahili.

# Abiria walia kutelekezwa kwenye daraja lililokatika

**Na Idda Mushi, GAIRO**

MAELFU ya abiria wanaosafiri kwa mabasi kupitia barabara kuu ya Dodoma-Dar es Salaam, wamelalamika kutelekezwa kwenye daraja lililokatika mkoani Morogoro na kulazimika kutumia gharama kubwa kufika waendako.

Wasafiri hao wamekwama kwenye eneo daraja la Kiegeya, maarufu Daraja la Mkange, wilayani Gairo mkoani Morogoro, baada ya daraja hilo kukatika juzi kutokana na mvua inayoendelea kunyesha.

Wakizungumza na Nipashe katika eneo hilo, abiria hao walilalamikia utaratibu ubovu wa wasafirishaji, wakidai wanaposhuka ndani ya gari, mkataba unakuwa umeisha.

Felista Mhagama, Fatuma Benjamin, Sylvester John na Malulu Machama, walisema walitarajia kutakuwa na magari ya kuwafaulisha lakini haifanyika hivyo.

Walisema wamekuwa na wakati mgumu kutumia muda na gharama kubwa kuvuka upande mwingine na wanalazimika kulipia mizigo na kuonyeshwa njia.

Alisema wamiliki wa mabasi wamekataa kuwarudishia nauli zao na hata kuwapa magari mbadala ya kuendelea na safari, hivyo kulazimika kulipa nauli mara mbili.

KAULI YA TABOA

Wakati abiria wakitoa malalamiko hayo, Katibu wa Chama cha Wasafirishaji Tanzania (Taboa), Eneo Mrutu, alisema kwa sasa wamiliki wa mabasi wanafaulisha abiria kwa utaratibu wa magari kwenda hadi eneo la tukio, abiria wanavushwa na kuingia kwenye basi lingine.

Kufa kufaana! Wananchi wa eneo hilo wametumia nafasi hiyo kujipatia kipato kwa kuwaonyesha wasafiri njia za uchochoro kuvuka upande wa pili wa barabara.

Wananchi hao wanawabeba wasafiri na kuwasaidia mabegi kwa malipo ya kati ya Sh. 500 hadi 5,000, kulingana na huduma anayopewa mhusika.

Hali hiyo inatokana na kwamba wasafirishaji kwa sasa wanapeleka magari hadi eneo hilo na baadaye abiria wanafaulishwa kwenye magari yaliyo upande wa pili na kuendelea na safari.

Mkazi wa Kiegeya wilayani Gairo, Gilbert Sing'ana, alisema kazi hiyo tayari imemwingizia kipato cha Sh. 30,000.

"Kama yeye (abiria) hatoweza kuvuka, nambeba yeye na mizigo yake, na sisi hapa ndipo tunapopata riziki," alisema.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kuandika, alisema kuharibika kwa daraja hilo kumetokana na uchakavu wa muda mrefu kwa kuwa limedumu kwa zaidi ya miaka 30 bila kukarabatiwa.

Alisema kuwa barabara hiyo imewekwa kwenye mpango wa matengenezo na upambuzi yakinifu umeshafanyika, kinachosubiriwa sasa ni kuanza ujenzi na ukarabati kwenye maeneo yote yenye kasoro.

Alisema daraja hilo kwa sasa linajengwa na Jeshi la Wananchi na kwamba ni lazima njia hiyo ifunguke kwa kuwa serikali imehamia eneo hilo kuhakikisha mawasiliano yanarejea.

HABARI KITAIFA

# DC ashangaa wafu kumdhamini karani

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

MKUU wa Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, Deodatus Kinawilo, ameshangazwa na kitendo cha karani wa Chama cha Msingi cha Ushirika Kaibanja, Sweetbert Mutembei, kudhaminiwa na watu waliofariki dunia.

Kiongozi huyo amepigwa na butwaa baada ya kufuatilia malalamiko ya wakulima wa kahawa kutolipwa fedha zao na chama hicho kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita, huku sehemu ya kahawa inayodaiwa kukusanywa na wakulima hao ikiwa haiko ghalani.

"Sijawahi kuona maishani mwangu, mtu anadhaminiwa na watu waliokufa kazini, karani huyu anatuhumiwa kuhujumu kahawa ya wakulima, haonekani lakini nilipofuatilia waliomdhamini kwa kazi hii, wote ni marehemu. Ofisa ushirika huu ni uzembe wa hali ya juu," alisema.

Kinawilo alisema kitendo cha karani huyo kudhaminiwa na watu waliofariki dunia kimetokana na uzembe wa Ofisa Ushirika, Mutawajibu Rwiza, na kumwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, kumpangia kazi nyingine.

"Alitakiwa kuhakikisha kwamba karani huyo anadhaminiwa na watu walio hai, wote hawa wamefariki, yaani wafu wanamdhamini vipi karani? Kumdhamini kwao kunaonyesha hakukuwa na umakini kwa ofisa ushirika," alilalamika.

Alisema uchunguzi alioufanya kwa kushirikiana na uongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Kagera (KCU 1990 LTD), umebaini kuwapo kwa upotevu wa tani 25 za kahawa yenye thamani ya Sh. milioni 28.

Mkuu wa Wilaya huyo aliitisha mkutano wa dharura na wakulima wa zao la kahawa katika eneo hilo, uongozi wa Chama cha Ushirika cha Msingi Kaibanja na uongozi wa KCU.

Wakati mkutano huo ukiendelea, kiongozi huyo wa wilaya aliwakabidhi viongozi wanne wa chama hicho cha msingi kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Bukoba kwa uchunguzi, lakini karani aliyekuwa analalamikiwa, hakuwapo.

"Karani huyu ambaye ametoweka na hapa hayupo, naomba asakwe popote pale alipo, aletwe kujibu tuhuma zinazomkabili na upotevu wa kahawa ya wakulima, lakini hawa wanne, OCD ondoka nao uwahoji, dhuruma kwa wakulima kwa awamu hii haikubaliki," alisema.

Alisema serikali inajitahidi kukusanya mapato ya ndani ili kupunguza kero za wananchi wakiwamo wakulima wa kahawa, lakini wanatokea watu wachache wasio waaminifu na kula fedha za wakulima.

Mkaguzi wa Ndani wa KCU aliyefanya ukaguzi na kubaini upotevu huo wa kahawa, Robert Kateka, alisema ukaguzi uliofanyika ulibaini uwapo wa wanachama wanaokidai chama hicho zaidi ya Sh. milioni 28.



Mwenyekiti wa Taifa wa NCCR-Mageuzi na Mbunge wa Vunjo, James Mbatia (kulia), akikabidhi kadi ya uanachama kwa aliyekuwa Katibu Mwenezi wa Baraza la Vijana la Chadema (Bavicha), Edward Simbeye, baada ya kujiunga rasmi na chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waiomba mahakama kurudishiwa kadi benki

**Na Hellen Mwango**

MKURUGENZI wa Uthamini wa madini ya almasi na vito wa serikali, Archad Kalugendo na Edward Rweyemamu, wanaokabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi wamewasilisha maombi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakiomba kurejeshewa kadi zao za benki.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, jana amekiri mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi kupokea nakala ya maombi hayo.

Wankyo alidai upande wa Jamhuri unaomba siku 14 kwa ajili ya kujibu maombi ya utetezi.

Upande wa utetezi haukuwa na pingamizi kuhusu ombi la Jamhuri kupewa siku 14.

Awali upande wa Jamhuri ulidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi wake bado haujakamilika, lakini wamewaelekeza wapelelezi wafanikishe maeneo machache yaliyobaki.

Hakimu Shaidi alisema, maombi hayo yatatajwa Machi 6, na kesi ya msingi itatajwa Machi 20, mwaka huu, washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa wanakabiliwa na kesi ya kuisababishia serikali hasara ya Sh. 2,486,397,982.54 kati ya Agosti 25 na 31, 2017 katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Dar es Salaam na Shinyanga.

# Majaliwa: Waliofuja mali mkonge kukiona

**Na Khadija Mussa, MUHEZA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itawachukulia hatua watu wote waliohusika na ubadhirifu wa mali zikiwamo nyumba za Mamlaka ya Mkonge Tanzania.

Vilevile, amesema serikali itafanya uchunguzi katika mashamba yote ya mkonge ili kubaini yameendelezwa kwa kiasi gani na sehemu ambazo hazijaendelezwa zitachukuliwa na kugawiwa kwa wananchi ili walime mkonge.

Majaliwa aliyasema hayo jana alipozungumza kwa nyakati tofauti na wananchi wa Kata za Segera na Kabuku akiwa katika ziara yake ya kikazi wilayani Handeni mkoani Tanga.

Machi Mosi, mwaka huu, Waziri Mkuu alipokea taarifa ya uchunguzi wa tuhuma mbalimbali katika tasnia ya kilimo cha mkonge mkoani Tanga na kuagiza mapendekezo yaliyotolewa na timu iliyofanya uchunguzi, yakiwamo ya kurejeshwa serikalini kwa nyumba na 176 eneo la Bombo ambayo ilimilikishwa kwa Salum Shamte, yafanyiwe kazi.

Nyumba nyingine zilizopendekezwa kurejeshwa serikalini ni pamoja na nyumba 10 zilizoko ndani ya Jiji la Tanga katika maeneo ya Raskazone, Bombo, Nguvumali na Mtaa wa Market ambazo zilinunuliwa na watumishi kwa udanganyifu.

Timu hiyo maalum ya uchunguzi iliundwa na Waziri Mkuu na ilifanya uchunguzi mkoani Tanga kuanzia tarehe Novemba 29 mwaka jana hadi Februari 7 mwaka huu. Timu hiyo iliyokuwa na wajumbe 13, ilihusisha maofisa kutoka ofisi mbalimbali za serikali.

Waziri Mkuu alisema kwa kuwa katani ndiyo zao la biashara mkoani Tanga na serikali itahakikisha watu wote wenye mashamba makubwa ya mkonge ambayo wameshindwa kuyaendeleza, itayachukua na kuyarejesha kwa wananchi.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu amesema serikali imejenga vituo 352 vya afya nchi nzima vikiwamo viwili vilivyojengwa Handeni.

Waziri Mkuu alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe, kuhakikisha wananchi wanaokwenda kufuata huduma za matibabu katika vituo vya afya na zahanati, wanapatiwa dawa badala ya kuelekezwa kwenda kununua kwenye maduka ya watu binafsi.

Alisema serikali imeongeza bajeti ya dawa kutoka Sh. bilioni 37 hadi Sh. bilioni 269, hivyo hakuna sababu ya mwananchi kwenda eneo la kutolea huduma ya afya na kukosa dawa.

Waziri Mkuu pia alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Handeni ahakikishe kila kijiji kinapata huduma ya majisafi na salama kwa kusimamia uchimbaji wa visima kupitia fedha za makusanyo ya ndani.

Waziri Mkuu alisema serikali kupitia kampeni ya Rais John Magufuli ya kumtua mama ndoo kichwani, itahakikisha wananchi katika maeneo yote nchini wanapata huduma ya maji safi na salama karibu na makazi yao.

Kuhusu umeme, Waziri Mkuu alisema maeneo ya wilaya hiyo ambayo bado hayajapata umeme, yote yatasambaziwa umeme kupitia Mradi wa Nishati Vijijini (REA) na wananchi hawatawajibika kulipia gharama za nguzo.

Alisema Rais Magufuli anataka kuona nyumba ya kila Mtanzania ina huduma ya umeme unaounganishwa kwa gharama nafuu ya Sh. 27,000.

chemicotex
the brands for you

TAARIFA KWA UMMA



*Engliberth Daudi Mwamkinga*

113541602

HII NI KUTAARIFU UMMA KWAMBA MWENYE PICHA HAPO JUU **ENGLIBERTH DAUDI MWAMKINGA** SI MFANYAKAZI TENA WA **CHEMI & COTEX INDUSTRIES LIMITED** KUANZIA TAREHE **4-03-2020.** ANATAFUTWA KWA TUHUMA ZA KUKIMBIA NA FEDHA ZA KAMPUNI, **KW/RB/1283/2020.**

TUNAOMBA KUUTANGAZIA UMMA KWAMBA KAMPUNI YA CHEMI & COTEX INDUSTRIES LIMITED HAITAHUSIKA NA MIAMALA, AU SHUGHULI YOYOTE ITAKAYOFANYWA NA MTAJWA HAPO JUU KWA JINA LA KAMPUNI.

***ATAKAYEPATA TAARIFA ZAKE ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI CHA KARIBU. ZAWADI NONO ITATOLEWA.***

# Umeme wa megawati 80 kuanza mwakani

**Na. Restuta Damian, NGARA**

BODI ya Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) inatarajia kupokea umeme wa mradi wa maporomoko ya Mto Kagera ya Rusumo, unaojengwa katika Kata Rusumo wilayani Ngara mkoani Kagera ifikapo mwaka 2021.

Mradi huo utakapoanza kutekelezwa, utasaidia kutatua changamoto za umeme nchini.

Mradi huo unaendeshwa na nchi tatu za Tanzania, Rwanda, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), ambazo zimeingia makubaliano ya uhitaji wa nishati hiyo kutoka bwawa la mto Kagera.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dk. Alexander Kyaruzi, alisema mradi huo utanufaisha wananchi kwa kuwa na umeme wa uhakika kutoka kwenye bwawa hilo.

Dk. Kyaruzi alisema, mradi huo wa megawati 80, na utagawanywa kwa nchi hizo tatu na kila nchi kupata megawati 27.

Aidha, alisema kwa Tanzania, kituo kikuu cha kuingiza na kusambaza umeme kinaendelea kujengwa katika Kata ya Nyakanazi wilayani Biharamulo, ambacho kitagawa maeneo yote ya ndani na nje.

"Huu umeme utakuwa wa uhakika na utagawa mikoa yote ya Tanzania na hata nchi jirani walihitaji. Mfano mkoani hapa tulipo (Kagera) umeme unatoka Uganda na bado una changamoto kidogo," alisema Kyaruzi.

Meneja wa mradi huo, Darren George, alisema ujenzi wa mradi umefikia asilimia 60 ikiwa ni hatua ya kwanza na ya pili kwa uwekaji wa miundombinu ya nchini ya mitamba.

"Hatua hizo mbili tulizonazo isingekuwa changamoto ya fedha kutoka na matetemeko ya ardhi kwenye makazi ya watu, tungekuwa hatua za ukamilishaji hivi sasa,"alisema George.

Aliongeza kuwa baada ya kukamilika hatua hizo, zitajengwa ofisi za usimamizi wa mradi huo zitakazokuwa zinaangalia ugawaji wa umeme kwa kila eneo la mpaka wa nchi hizo tatu.

Mradi huo ulianza mwaka 2017 na ulitarajia kukamilika Februari mwaka huu, lakini kutokana na changamoto za kifedha na matetemeko ya miamba kwenye makazi ya watu, ulisimama.

Ujenzi huo unasimamiwa na kampuni za CGCOC na JVJWHC za China.



Mwonekano wa ujenzi unaoendelea wa daraja la treni ya kisasa, unaofanywa na kampuni ya Yapi Merkezi ya Uturuki, katika eneo la Kamata, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Upelelezi kesi kusafirisha dawa za kulevya wakamilika

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri umedai katika kesi ya kusafirisha dawa za kulevya gramu 214.11 inayomkabili mfanyabiashara Mohamed Hariri na mke wake, Muna Said, upelelezi wake umekamilika na uko tayari kuwasomea maelekezo ya mashahidi.

Madai hayo yalitolewa jana, kesi hiyo ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi, Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi, Vicky Mwaikambo.

Wakili wa Serikali Ashura Mzava, alidai kuwa kesi ilipangwa jana kwa ajili ya kutajwa.

Alidai kuwa Jamhuri inaomba tarehe kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya mashahidi ili kesi ihamishiwe Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi maarufu kama Mahakama ya Mafisadi.

Wakili wa utetezi, Nehemiah Nkoko, hakuwa na pingamizi na ombi la Jamhuri.

Hakimu Mwaikambo alisema kesi hiyo itasikilizwa maelezo ya mashahidi Machi 10, mwaka huu.

Katika kesi ya msingi, Hariri aliunganishwa na mke wake katika kesi hiyo Agosti 22, 2019 na kwamba wote kwa kwa pamoja wanadaiwa kuwa Machi 2, 2018 eneo la Kinondoni Matitu, jijini Dar es Salaam washtakiwa walikutwa na dawa hizo za kulevya.

# Serikali yaombwa kuongeza dampo

**Na Romana Mallya**

UMOJA wa Makandarasi wa taka ngumu Tanzania (Uwatanguta), umeiomba serikali kuongeza dampo baada ya yaliyopo kutokidhi mahitaji na kusababisha magari kukaa siku tatu bila kushusha uchafu.

Akisoma risala ya umoja huo kwa niaba ya makandarasi, Mwanaasha Mrutu, kutoka Kimwede General, alisema jambo hilo linasababishwa na uchache wa dampo na kupendekeza ikiwezekana kila wilaya iwe na ya kwake.

"Makandarasi tunapitia vikwazo vingi vya kutekeleza majukumu yetu, kuna changamoto ya kukosekana kwa dampo za uhakika na rafiki kwa vyombo vyetu vya kuzolea taka tunaomba ikiwezekana kila wilaya iwe na ya kwake," alisema.

Mrutu alisema changamoto hiyo imewasababishia kupoteza siku tatu dampo wakati ratiba zinawataka wazimwage na kurudi mtaani kuchukua nyingine.

Alisema changamoto nyingine ni wananchi kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uhifadhi wa taka na utunzaji wa mazingira.

"Changamoto nyingine ni mikataba yetu kuwa ya muda mfupi ambayo imezisababishia kampuni kushindwa kupata mikopo kwenye taasisi za fedha ili kuongeza vifaa zaidi, tunaomba jambo hili manispaa ambao ndiyo mdhamini mlifanyie kazi," alisema.

Pia waliomba halmashauri zinazowakodi na wanaofanya nao kazi ziwalipe kwa wakati ili waweze kuwalipa wafanyakazi wao.

Mwenyekiti wa taifa wa Uwatanguta, Mary Shekoloa, alisema wanafanya kazi ngumu na wafanyakazi wake wapo kwenye mazingira hatarishi na kuiomba serikali izifanyie kazi changamoto zao.

"Sote tunafahamu mazingira machafu yanahatarisha afya zetu hivyo lengo letu ni kuhakikisha Tanzania inakuwa safi, tunaomba Halmashauri na Manispaa tunazofanya nazo kazi zitusaidie kuziondoa changamoto hizi," alisema.

Ofisa Tawala Wilaya ya Ilala, Jabiri Makame, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa wilaya hiyo, Sophia Mjema, alisema taka zinazozalishwa Mkoa wa Dar es Salaam ni tani nyingi, lakini uwezo wa kuziondoa bado hawajaweza kukabiliana nao kwa asilimia 100.

Kuhusu changamoto zilizoelezwa na makandarasi hao, alisema amezipokea na zitawasilishwa kwenye mamlaka husika ili zitafutiwe ufumbuzi.

Katika mkutano huo, makandarasi hao wamemkabidhi mgeni rasmi katiba na cheti ikiwa ni sehemu ya ushirikiano walionao na kuonyesha kutambuliwa kazi zao.

Pia makandarasi hao wamekabidhi vifaa mbalimbali vya tiba Hospitali ya Rufani Amana iliyopo Manispaa ya Ilala.

# MATANGAZO

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## President's Office – State House
## TANZANIA SOCIAL ACTION FUND

**Tender No. TZ-TASAF-161184-NC-RFB for Printing Handbooks, Manuals, Publicity Materials and Reports**

## Invitation for Tenders

**Date: 4th March, 2020**

1. This Invitation for Tenders follows the General Procurement Notice for this Project which appeared in UN Development Business Issue no. WB-P475857-02/20 dated 4th February, 2020.

2. The Government of the united republic of Tanzania has received financing from the World Bank toward the cost of the Productive Social Safety Net II. This project will be jointly financed by the Agency for International Development, Bill and Melinda Gates Foundation, The Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis & Malaria, International Fund for Agriculture Development, The government of NORWAY and OPEC. The Tanzania Social Action Fund the implementing agency for this Project intends to apply part of the proceeds toward payments for printing services.

3. The The Tanzania Social Action Fund now invites sealed Tenders from eligible providers of for printing services.

4. Tendering will be conducted through the National Competitive Tendering procedures specified in the Public Procurement (Regulations, 2013 – Government Notice No. 446 as amended in 2016 and is open to all Tenderers as defined in the Regulations.

5. Interested eligible Tenderers may obtain further information from and inspect the Tendering Documents at the office of the *Secretary of the Tender Board, Tanzania Social Action Fund, Dar es salaam, Old Kilwa /Malindi Road, Main Building, Third Floor, Room No. 20 from hours 0800 to 1600 hours* on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays.

6. A complete set of Tendering Documents in English and additional sets may be purchased by interested Tenderers on the submission of a written application to the address given under paragraph 5 above and upon payment of a non-refundable fee of *Fifty Thousand (50,000) Tanzanian Shillings or in a convertible currency.* Payment should be direct *deposit to CRDB Bank PCL, Vijana Branch, Dar es salaam, Tanzania Social Action Fund account number 01J1005174000.*

7. All Tenders must be accompanied by a Tender Securing Declaration in the format provided in the Tendering Documents.

8. All Tenders in one original plus three copies, properly filled in, and enclosed in plain envelopes must be:

| ADDRESSED to: | DELIVERED to: |
|---|---|
| ***The Executive Director,*** <br> ***Tanzania Social Action Fund, 4th Floor, PSSSF Plaza, Jakaya Mrisho Kikwete Road,*** <br> ***P. O. Box 2719,*** <br> ***Dodoma, Tanzania*** <br> ***Phone: +255 26 2963866*** <br> ***Facsimile: +255 26 2963871*** <br> ***Email address: info@tasaf.go.tz*** <br> ***Website: www.tasaf.go.tz*** | ***TASAF, Dar es salaam,*** <br> ***Old Kilwa /Malindi Road,*** <br> ***Main Building, Third Floor,*** <br> ***Room No. 20,*** |

at or before **10:00 hours on 31st March, 2020.** Tenders will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Tenderers' representatives who choose to attend in the opening at the Conference Room.

9. Late Tenders, portion of Tenders, electronic Tenders, Tenders not received, and not opened and not read out in public at the Tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**The Executive Director,**
**Tanzania Social Action Fund,**
**4th Floor, PSSSF Plaza, Jakaya Mrisho Kikwete Road,**
**P. O. Box 2719,**
**Dodoma, Tanzania**

215653102

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## President's Office – State House
## TANZANIA SOCIAL ACTION FUND

**Request for Bids**
**Framework Agreements for Goods**
**(Primary Procurement, One-Envelope Bidding Process)**

**Procuring Agency: Tanzania Social Action Fund**

**Country: Tanzania**

**Name of Project: Productive Social Safety Net Project II**

**Framework Agreement Title: Supply ICT Consumables, Stationery and Motor Vehicle Spare Parts**

**RFB Reference No.: No. TZ-TASAF-148779-GO-RFB to Supply ICT Consumables, No. TZ-TASAF-148787-GO-RFB to Stationery and No. TZ-TASAF-148782-GO-RFB to Motor Vehicle Spare**

**Credit No.: 6489-TZ**

**Date: 4th March, 2020**

1. The Government of the united republic of Tanzania has received financing from the World Bank toward the cost of the Productive Social Safety Net II. This project will be jointly financed by the Agency for International Development, Bill and Melinda Gates Foundation, The Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis & Malaria, International Fund for Agriculture Development, The government of NORWAY and OPEC. The Tanzania Social Action Fund the implementing agency for this Project intends to apply part of the proceeds toward payments under Call-off Contracts that may be awarded under Framework Agreements to Supply ICT Consumables, Stationery and Motor Vehicle Spare Parts. The Primary Procurement to conclude Framework Agreements award Call-off Contracts will be governed by the World Bank's Procurement Regulations concluded through this RFB Primary Procurement process.

2. The Procuring Agency is undertaking the Primary Procurement with a view to concluding Framework Agreements. The Procuring Agency is the sole Purchaser under the Framework Agreements. The Procuring Agency now invites sealed Bids from eligible Bidders to Supply ICT Consumables, Stationery and Motor Vehicle Spare Parts.

3. The Framework Agreements to be concluded will be Single-User. The Single-User entitled to purchase under the Framework Agreements is the Tanzania Social Action Fund.

4. The Framework Agreements to be concluded will be Single-Supplier.

5. The selection of a FA Supplier to be awarded a Call-off Contract will be direct to the Single-Suppliers for each Lot who a particular Framework Agreement is concluded with. However, the conclusion of Framework Agreements shall not impose any obligation on the Procuring Agency to purchase Goods under a Call-off Contract. The conclusion Framework Agreement does not guarantee that a FA Supplier will be awarded a Call-off Contract.

6. Bidding will be conducted through National Competitive Procurement using a Request for Bids (RFB) as specified in the World Bank's "Procurement Regulations for IPF Borrowers" the World Bank's "Procurement Regulations for Investment Project Financing (IPF) Borrowers" (Procurement Regulations) dated July 2016 and revised in November 2017 and August 2018 ("Procurement Regulations"), and is open to all eligible Bidders as defined in the Procurement Regulations.

7. Bidders may submit Bids for one or more lots in a particular bid.

8. The Framework Agreements shall be concluded for a Term of 3 years subject to appraisal annually from the commencement date stated in the Framework Agreement.

9. The Primary Procurement shall establish Closed Framework Agreements.

10. Interested eligible Bidders may obtain further information from Secretary of the Tender Board, Tanzania Social Action Fund, Dar es salaam, Old Kilwa /Malindi Road, Main Building, Third Floor, Room No. 20 and inspect the Bidding document during office hours 0800 to 1600 hours at the address given below.

11. The Bidding document in English may be purchased by interested Bidders upon the submission of a written application to the address below and upon payment of a nonrefundable fee of Fifty Thousand (50,000) Tanzanian Shillings or in a convertible currency. The method of payment will be direct deposit to CRDB Bank PCL account number 01J1005174000 Name of the account is Tanzania Social Action Fund. The document will be collected by bidder at Tanzania Social Action Fund, Dar es salaam, Old Kilwa /Malindi Road, Main Building, Third Floor, Room No. 20 upon presentation of evidence for payment of fees for purchase of bidding document.

12. Bids must be delivered to the address below at or before 10.00 hours East African time on 31st March, 2020. Electronic Bidding will not be permitted. Late Bids will be rejected. Bids will be publicly opened in the presence of the Bidders' designated representatives and anyone who chooses to attend, at TASAF Dar es salaam, Conference Room, Old Kilwa/Malindi on 31st March, 2020.

13. The addresses referred to above is are:

| Bids must ADDRESSED to: | Bids shall be DELIVERED to: |
|---|---|
| **The Executive Director, Tanzania Social Action Fund, 4th Floor, PSSSF Plaza, Jakaya Mrisho Kikwete Road,** <br> **P. O. Box 2719,** <br> Dodoma, Tanzania <br> **Phone: +255 26 2963866** <br> **Facsimile: +255 26 2963871** <br> **Email address: info@tasaf.go.tz** <br> **Website: www.tasaf.go.tz** | **TASAF, Dar es salaam,** <br> **Old Kilwa /Malindi Road,** <br> **Main Building, Third Floor, Room No. 20,** |

215653102

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Wafanyabiashara waitumie fursa soko la uhakika DRC*

**TAASISI** ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imesema inatarajia kuongoza ziara ya wafanyabiashara wa Tanzania kwenda Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC) ili kunadi na kutafuta soko la uhakika la bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya Tanzania.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana kuhusu ziara hiyo ya siku tatu inayoanza Machi 6 hadi 8, Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, alisema ziara hiyo imekuja wakati mwafaka ambapo bidhaa kutoka sekta mbalimbali za kiuchumi zitanadiwa na kutafutiwa masoko DRC.

Alisema taasisi hiyo imeandaa ziara hiyo kwa lengo la kutangaza fursa za kiuchumi zilipo nchini, na kuwa wanaamini Tanzania kwa sasa inazalisha bidhaa bora kutoka katika viwanda vya ndani katika sekta ya kilimo na mifugo, hivyo lazima kuwekwa mikakati ya namna ya kutumia fursa hizo hasa katika kipindi hiki ambacho TPSF ni mwenyekiti wa Baraza la Biashara la nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Ngalula alisema taasisi, idara na wizara zinazohusika zimetaarifiwa na kwamba zimetoa baraka zake kwa ziara hiyo kufanyika DRC.

Taasisi hiyo imewahamasisha wafanyabiashara kujitokeza kwa wingi katika ziara hiyo ili kwenda kuangazia fursa zilizopo katika taifa hilo ambalo ni mwanachama wa SADC.

Naye Mwenyekiti wa chama cha wasindikaji wa wadogo (TAFOPA), Suzie Laizer, alisema wanategemea kutangaza na kupanua wigo wa bidhaa za usindikaji kutoka Tanzania, na kwamba zara hiyo itasaidia katika kuongeza ukubwa wa biashara ya bidhaa za kusindikwa, ambazo wamekuwa tukizifanya kwa miaka mingi.

Mkakati wa kusaka masoko nje ya nchi ni mbinu yenye tija katika mpango wa kuipaisha nchi kiuchumi na hususan wakati huu ambao Tanzania imejizatiti kuingia katika uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda.

Kwa hiyo tunapoanza kujianda na ujenzi wa viwanda kuingia uchumi wa kati, jitihada hizo hazinabudi kwenda sambamba na kuanza kusaka masoko ya kuuza bidhaa zitakazozalishwa na viwanda vyetu.

Utafutaji wa masoko unapaswa kuwahusisha wadau wengi ikiwamo serikali yenyewe kupitia wanadiplomasia wanaoiwakilisha nje, ambao ndio watekelezaji wa sera yetu ya nje ya Diplomasia ya Uchumi.

Hao wajibu wao ni kutangaza fursa zilizoko nchini kwa ajili ya kuwavutia watalii, wawekezaji pamoja na kuangalia ni masoko yapi tunaweza kuuza bidhaa zetu zitakazozalishwa na viwanda tunavyokusudia kuvijenga.

Wengine ni wafanyabiashara wenyewe kupitia vyama vyao, kama ambavyo TPSF ilivyofanya kwa kuandaa ziara ya wafanyabiashara ya kusaka masoko DRC.

Tunaona kuwa TPSF imeona mbali kwa kuona fursa zilizoko DRC kwa ajili ya kuwa soko kwa bidhaa zinazozalishwa na zitakazozalishwa nchini katika siku za usoni. Tunasema ni fursa ya maana kwa kuwa taifa hilo lina idadi kbwa ya watu sambamba na mahitaji ya bidhaa kutoka Tanzania.

Ikumbukwe kuwa DRC ina mahusiano mazuri na ya karibu na Tanzania katika nyanja mbalimbali ikiwamo ya biashara. Kadhalika, nchi hiyo inaitegemea Tanzania kupitisha bidhaa zake inazoziagiza nje kupitia Bandari ya Dar es Salaam, hivyo ni fursa muhimu kwa nchi yetu.

Tunatarajia kuwa wafanyabiashara wetu wataichangamkia fursa hiyo na nyingine zilizoko katika nchi zingine, na tunavyishauri vyama vyao kuwa na mikakati endelevu ya kusaka masoko ya uhakika nje ya nchi. Hata hivyo, changamoto kwao ni kuhakikisha wanazalisha bidhaa zenye ubora wa viwango.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Ianzishwe kampeni lipa kodi ulipwe maendeleo

Na Reubeni Lumbagala

**KODI** ni chanzo muhimu cha mapato kinachowezesha ufanisi wa uendeshaji wa shughuli mbalimbali za serikali kuanzia miradi mikubwa ya miundombinu hadi ujenzi wa makazi nafuu mijini na vijijini. Juhudi za kimaendeleo zinazofanywa na serikali na taasisi zisizo za kiserikali zinategemea makusanyo ya kodi kwani upatikanaji wa fedha za kutosha hufanikisha mipango wanayoitekeleza.

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambayo ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ina wajibu wa kutoa elimu juu ya ulipaji wa kodi pamoja na kukusanya kodi kutoka kwa walipaji kodi ili kuchagiza utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo kama utoaji wa elimu bila malipo, usambazaji wa nishati ya umeme, maji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara, shule, vituo vya afya na hospitali, ununuzi wa ndege, meli, rada, ununuzi wa pembejeo za kilimo.

Utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo inategemea sana upatikanaji wa fedha ambazo ni zao la ukusanyaji wa kodi kwa wananchi.

Ni wakati wa TRA kuanzisha kampeni maalum "Lipa Kodi Ulipwe Maendeleo" kwa lengo la kuelimisha na kuhamasisha kila wananchi mwenye sifa ya kulipa kodi kutimiza kikamilifu wajibu wake huo muhimu kwa ajili ya kuwezesha kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo kwani matokeo ya maendeleo yanagusa moja kwa moja maisha ya wananchi.

Kampeni hii isimamiwe vyema na maofisa wa kitengo wa Elimu kwa Mlipakodi kutoka TRA lengo la kampeni hii ni kuwaelimisha wananchi kwa kuwaonyesha uhalisia wa namna mwamko wa ulipaji kodi ulivyosaidia utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati hapa nchini. Suala la ulipaji kodi ni suala la kizalendo, lakini upo umuhimu wa walipa kodi kuona matunda ya ulipaji wao kodi namna unavyogusa maisha yao kupitia nyanja mbalimbali za maendeleo.

Kampeni ya "lipa kodi ulipwe maendeleo" ilenge kuwaelimisha wananchi namna ambavyo maendeleo ya nchi yetu hayawezi kutenganishwa na mafanikio katika nyanja ya ukusanyaji wa kodi kutoka kwa raia wake. Mathalani, tangu serikali iingie madarakani kumekuwa na mafanikio katika ukusanyaji wa mapato hali inayopelekea mafanikio katika utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Mathalani, Desemba 2019, TRA ilikusanya mapato ya trilioni 1987 , makusanya haya ni makusanyo mkubwa yaliyovunja rekodi kwani hayajawahi kutokea tangu kuanzishwa kwa mamlaka hii.

Wananchi wanataka watoto wao wapate elimu bora, huduma bora za afya, za maji, nishati kupata pembejeo bora za kilimo, kuboreshewa miundombinu ya barabara. Pia wanahitaji kujengewa mazingira bora ya ufanyaji biashara na ajira yote hayo ni kodi.

Haya yote yanaweza kutimia pale ambapo serikali itafanikiwa katika ukusanyaji wa kodi. Hivyo basi, kampeni hii iwaelimishe wananchi kuwa pindi wanapolipa kodi serikalini, kodi hiyo inarudi kwao kwa mifumo ya miradi ya maendeleo ambayo inagusa maisha ya wananchi moja kwa moja.

Kipo kilio kutoka kwa wananchi wa maeneo mbalimbali nchini kutaka serikali kuwatatulia changamoto kama kujengewa shule, vyuo, masoko, hospitali, viwanda, barabara na madaraja ili wananchi watatuliwe kero zao ni kuwa na mwamko wa kulipa kodi kwani ndiyo itakayomaliza shida zao.

Kampeni ijikite kuwaelimisha wananchi namna ambavyo serikali isivyokuwa na namna nyingine ya kuwaletea maendeleo wananchi wake kama wananchi wenyewe hawatakuwa na mwamko wa kulipa kodi.

Kampeni izidi kuweka mkazo kwa wananchi kuwa na moyo wa kizalendo wa kuona fahari ya kulipa kodi kwani kodi hizo zina manufaa katika ujenzi wa Taifa lao. Kampeni iwafungue macho wananchi wanaopenda kuishi nchi za Magharibi kwa kudhani wakienda huko watapata maendeleo. Maendeleo yanayoonekana leo katika nchi za Magharibi ni matokeo ya juhudi za wananchi hao wazalendo ambao wanalipa kodi kikamilifu kwa mustakabali na ustawi wa nchi yao.

Ni muhimu kampeni hii ikawafikia wananchi hasa wa vijijini kwani mara nyingi wamekuwa hawafikiwi ipasavyo na kampeni nyingi zinazosimamiwa na taasisi mbalimbali pia isisitize umuhimu wa wanunuzi wa bidhaa na huduma kwa risiti za kielektroniki wafanyapo manunuzi kwani ni katika risiti hizo serikali hupata kodi na mapato yake ambayo yanasaidia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayojibu hoja na changamoto mbalimbali za wananchi.

HABARI KITAIFA

# Waziri arejesha mitumbwi iliyokamatwa uvuvi haramu

**Na Mwandishi Wetu, SIMIYU**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amerejesha kwa wamiliki wa mitumbwi 68 iliyokamatwa kwa makosa ya kujihusisha na uvuvi haramu Ziwa Victoria, baada ya wamiliki wake kukiri makosa yao na kuapa kutojihusisha tena na uvuvi haramu.

Amefikia uamuzi huo baada ya wavuvi wa Mwalo wa Nyamikoma wilayani Busega mkoani Simiyu kufikisha kilio hicho kwa serikali, wakiomba kusamehewa makosa yao na kuomba kurejeshewa mitumbwi hiyo ili waendelee na shughuli za uvuvi endelevu.

Mmoja wa wavuvi hao, Ally Bogoye mbali na kukiri makosa mbele ya Waziri Mpina na Katibu wa CCM Wilaya ya Busega, alisema kwa sasa wanashirikiana na serikali kulinda rasilimali za uvuvi na ndiyo maana kumekuwapo na ongezeko kubwa la samaki aina ya sangara na samaki wengine.

Mbali na maombi ya wavuvi hao, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Nyamikoma, Kulwa Lilaga, pia aliomba mitumbwi hiyo kuuzwa kwa mnada kwa kuwauzia wamiliki wenyewe ili kuinusuru isiendelee kuharibika ikiendelea kushikiliwa na serikali.

Kutokana na maombi hayo, Waziri Mpina alimwagiza Mkurugenzi wa Uvuvi kuhakikisha wavuvi wote wenye mitumbwi yao wanarejeshewa mitumbwi yao bila masharti yoyote ili waendelee na shughuli za uvuvi.

Mpina pia aliagiza wamiliki wote wenye mitumbwi yao, waandike barua za kukiri makosa yao na kuieleza serikali kwamba hawatarudia tena kujihusisha na uvuvi haramu.

Waziri huyo pia aliwashukuru wananchi wa Nyamikoma kwa kukiri makosa yao na kuyaona mafanikio ya operesheni za kupambana na uvuvi haramu.

Aliwahakikishia wavuvi hao kuwa serikali iko kwenye hatua za mwisho za kutanua wigo wa masoko kwa kusambaza mnyororo wa baridi hadi kwenye ngazi za vijiji ili wananchi wapate samaki wabichi na kuongeza masoko mapya ya samaki.

Alisema dhamira ya serikali ya kudhibiti uvuvi haramu ilikuwa na nia njema na siyo kumwonea mtu yeyote na ndiyo maana hata wananchi wenyewe wanakiri matunda ya kufanyika kwake.

Katibu wa CCM Wilaya ya Busega, Burhan Rutta, alimpongeza Waziri Mpina kwa kufika katika mwalo huo ikiwa ni siku chache tangu Katibu wa CCM wa Mkoa wa Simiyu kufika na kutoa maelekezo ya chama kwa serikali.



Ujenzi wa barabara za juu (Interchange), ukiendelea katika eneo la Ubungo jijini Dar es Salaam jana, ambapo ukikamilika unatarajia kupunguza msongamano wa magari kwenye eneo hilo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Watakiwa kuchangamkia fursa kiwanda cha ngozi

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amewataka wazawa nchini kuchangamkia fursa ya kuwekeza kiwanda cha kusindika ngozi Shinyanga mjini, ili wajikwamue kiuchumi.

Balozi Seif ambaye ni mlezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Shinyanga, alitoa rai hiyo jana wakati akikagua ujenzi wa machinjio ya mifugo ya kisasa, inayojengwa katika eneo la Ndembezi Shinyanga mjini ambayo inatarajiwa kukamilika mwezi huu.

Alisema huu ni wakati wa wazawa kuchangamkia fursa ya kuwekeza kiwanda cha kusindika ngozi badala ya kusubiri watu kutoka nje ya nchi kwenda kuwekeza mjini humo, wakati kuna Watanzania matajiri na wenye uwezo wa kuwekeza kiwanda hicho, na hatimaye kukua kiuchumi pamoja na kutoa ajira.

"Natoa wito kwa matajiri wazawa wakiwamo wa hapa Shinyanga mjini mchangamkie fursa hii ya kuwekeza kiwanda cha kusindika ngozi, kwa sababu mali ghafi ipo ya kutosha ambayo itakuwa inatoka kwenye machinjio hii ya kisasa ya uchinjaji wa mifugo," alisema Balozi Seif.

"Tuacheni tabia ya kutegemea kila kitu kutoka nje ya nchi, jaribuni wazawa kuwa mnawekeza kwenye miradi inayoanzishwa na serikali kama ujenzi wa kiwanda cha ngozi, hii ni fursa ambayo ipo wazi kabisa na pia itasaidia kupunguza tatizo la ajira na kuinua pia vipato vya wananchi na taifa kwa ujumla," alisema.

Aliiagiza serikali mkoani humo kuwa machinjio hayo yatakapoanza, miguu ya ng'ombe na mbuzi wauziwe wananchi kwa bei nafuu, ili wafanye biashara ya kuuza supu na kujipatia kipato ambacho kitabadilisha uchumi wa kaya zao.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, alisema watalitekeleza agizo hilo na kusisitiza wananchi wachangamkie fursa hiyo ya kuwekeza kiwanda cha ngozi, pamoja na kumwomba Balozi Seif asaidie kutafuta wawekezaji ili ngozi hizo zipate soko la uhakika.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Geofrey Mwangulumbi, akisoma taarifa ya ujenzi wa machinjio hayo, alisema ulibuniwa na serikali mwaka 2013, na kusanifiwa mwaka 2014 na ujenzi ulianza mwaka 2017 na utakamilika mwezi huu kwa gharama ya Sh. bilioni 5.7 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.


## TANGAZO KWA UMMA

### MATUMIZI MABAYA NA YA UDANGANAYIFU YA JINA LA BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA (AfDB)

Tumepata taarifa za mawakala mbalimbali wanaojivika nafasi za uongo za kusaidia katika kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa nia ya kujipatia fedha. Udanganyifu huu mara nyingi hufanywa kwa kupitia barua-pepe, au njia nyingine za mawasiliano.

Benki ya Maendeleo ya Afrika inasikitishwa sana na udanganyifu huu, ambao ni ukiukwaji wa maadili ya taasisi, na itashirikiana na mamlaka zinazohusika kupambana na mtandao huo wa ulaghai.

Sisi, Benki ya Maendeleo ya Afrika, tunathibitisha kwamba:

- Tunatangaza waziwazi maombi yote ya manunuzi ya taasisi kwenye tovuti ya Benki, ambayo ni: **www.afdb.org/en/about-us/corporate-procurement**. Ikiwa ombi lolote la manunuzi halijatangazwa kwenye tovuti hiyo, ombi hilo halipo, ni ulaghai.
- Hatudai wala kupokea malipo kutoka kwa watoa huduma, wagavi, wataalamu-washauri, wanaotafuta ajira, n.k., ili kuwapa mikataba ya kutoa huduma, ugavi wa bidhaa au malipo ili kutoa ajira.
- Hatutumii anuani za barua-pepe kama vile Gmail, Yahoo Mail n.k.
- Tunatangaza nafasi zote za ajira kwenye tovuti yetu: **www.afdb.org/jobseekers**. Kama nafasi ya ajira haijatangazwa kwenye tovuti hiyo, nafasi hiyo haipo, ni ulaghai.

Kwa hiyo, tunawashauri watu wote, pamoja na wafanya biashara wanaopenda kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuzingatia yafuatayo:

- Zingatia matangazo yanayohusu manunuzi, ambayo yanapatikana kwenye tovuti ya Benki tu, na si kwingineko.
- Kamwe usilipe au kutuma fedha kwa mtu yeyote ili kupata kazi, mkataba wa huduma au kufanya biashara yoyote na Benki.
- Toa taarifa za majaribio yote ya udanganyifu kwa mamlaka zinazohusika za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na pia ifahamishe Benki kupitia anwani hii ya barua-pepe: **security@afdb.org.**

2156530002

## HABARI KITAIFA

# Lema atakiwa kujisalimisha polisi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMISHNA wa Operesheni na Mafunzo CP Liberatus Sabas, amemtaka Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, kujisalimisha polisi kwa kutoa taarifa za upotoshaji zenye lengo la kuleta taharuki kwa Jamii na kuwachonganisha wananchi na jeshi lao la polisi.

Pia, amemwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, kumtafuta mbunge huyo popote alipo na kumkamata.

Kamishna Sabas alitoa agizo hilo jana, wakati akitoa ufafanuzi wa matukio ya mauaji ya watu 14 yaliotokea mkoani Singida, wilayani Manyoni kuanzia mwaka jana mpaka Februari, mwaka huu.

Akitoa ufafanuzi huo Kamishna Sabas alisema, Februari 29, mwaka huu, wilayani Manyoni wakati wa kutoa salamu kabla ya mazishi ya marehemu Alex Jonas, aliyekutwa ameuawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali sehemu mbalimbali za mwili wake eneo la Mbugani, Lema alionyesha orodha ya watu 14 ambayo pia aliiweka katika mitandao ya kijamii akidai waliuawa kwa kuchinjwa.

Alisema aliweka taarifa hizo bila ya kuwa na uhakika kama ni sahihi huku akilituhumu Jeshi la Polisi Mkoa wa Singida kushindwa kutekeleza wajibu wake.

Kamishna Sabas aliwataja marehemu hao kuwa ni Sichelela Mosses (22), Abdallah Lyama (38), Rajabu Abasi (36), Martini Motekwa (30), Hamad Hussein (37), Emmanuel Meso (50), Mika Saimon (38), Mshoma Ngassa (30) na John Logion (60).

Wengine ni Michael Charles (35), Issa Abdallah (2), Jumanne Ndelemo (22), Heri Mamba na Alex Jonas (40),

Akimtaja kila marehemu na sababu za kifo chake, Kamisha Sabas alisema Sichelela mkazi wa Sayuni, alikutwa ameuawa na uchunguzi ulibaini kuwa mauaji hayo yametekelezwa na mume wake Rashidi Hamisi, akishirikiana na Timoth Leonard, kwa sababu ya wivu wa mapenzi kwa kumtuhumu mkewe huyo kuwa na mahusiano ya kimapenzi watu wengine.

Kamishna Sabas alisema watuhumiwa wote wawili wamekamatwa pamoja na vielelezo vyote vilivyotumika kwenye mauaji hayo.

Lyama mkazi wa Kihanju, Itigi, alifariki dunia Agosti 26, 2019 wakati akiendelea na matibabu katika Hospitali ya St. Gaspar Itigi, kutokana na shambulio la kupigwa kwa fimbo pamoja na mateke na ngumi sehemu mbalimbali za mwili wake.

Katika tukio la Septemba 14, 2019, Abasi, alifariki dunia akiwa anapatiwa matibabu katika Hospitali ya St. Gaspar, Itigi kutokana na tukio la kuchomwa na kitu chenye ncha kali na mtuhumiwa Mohammed Abdi. Chanzo cha tukio hilo ni wivu wa kimapenzi baada mtuhumiwa kudaiwa kumfumania akiwa na mke wake nyumbani kwa mtuhumiwa. Mtuhumiwa amekamatwa na upelelezi umekamilika.

Motekwa, ambaye inasadikiwa kuwa ana upungufu wa akili na akiwa hana makazi maalum, mwili wake ulikutwa kwenye kibanda alichokuwa akijihifadhi nyakati za usiku ukiwa umechomwa moto. Katika uchunguzi mwili huo pia ulibainika kuwa na jeraha kichwani.

Mkazi wa Manyoni, Hussein alifariki dunia baada ya kushambuliwa na wananchi wanaosadikiwa kujichukulia sheria mikononi kwa kutumia fimbo na mawe kutokana na tuhuma za wizi wa mifugo.

Pia, Meso, mkazi wa Kijiji cha Maweni, Tarafa ya Kintinku, alifariki dunia kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali sehemu za siri.

Kamishna Sabas alisema Saimon (38), alifariki dunia kwa kukatwa na vitu vyenye ncha kali katika sehemu mbalimbali za mwili, Novemba 15, 2019 na mtoto wake Saimon Mika kwa akishirikiana na mama yake mzazi Mea Mwarabu na rafiki wa mtoto wake Robert Elia, waliodaiwa kutaka kurithi shamba la baba yao.

Ngassa, alifariki dunia kwa kupigwa kwa fimbo kichwani na mume wake Mariyambelele Senzo, Novemba 21, 2019 Majiweni, Kata ya Mitundu, chanzo cha kifo ni wivu wa kimapenzi akimtuhumu mke wake kutembea na mwanamume ambaye bado hajafahamika.

Logion, mkazi wa Mitundu alifariki dunia Novemba 22, 2019 kwenye shamba la mihogo, linalomilikiwa na Anthony Lipiti huko Itigi. Uchunguzi wa awali wa Polisi umebaini kuwa chanzo cha tukio hilo ni wizi.

Tukio lingine ni la Januari 1, mwaka huu, Charles, mkazi wa Mwamagembe alifariki wakati anapatiwa matibabu katika Zahanati ya Mwamagembe, Itigi kutokana na taarifa za kujeruhiwa tukio lililotokea Desemba 21, 2019. Vile vile Abdallah aliyekuwa na ulemavu wa miguu alifariki dunia Januari 24, mwa huu kwa kunyongwa na mama yake mzazi kwa kile kinachodaiwa kukosa mahitaji kutoka kwa baba wa mtoto.

Ndelemo, alifariki dunia baada ya kukatwa na kitu chenye ncha kali na kaka yake Hamisi Ndelemo, kutokana na kumfumania akiwa na mke wake.

Mamba alifariki dunia baada ya kugongwa na pikipiki. Uchunguzi wa awali wa Polisi umebaini kuwa marehemu alikuwa amelewa huku akikatiza barabarani bila kuchukua tahadhari.

Jonas (40), dereva bodaboda, aligundulika kufariki dunia Februari 26, mwaka huu na uchunguzi unaendelea ili kubaini chanzo cha kifo hicho.

Kamishna Sabas alisema hakuna mwanasiasa au mtu yeyote atakaetumia Jeshi la Polisi kama kimvuli cha kujipatia umaarufu.


The Guardian Limited

## JOB VACANCY

**The Guardian Limited ,publisher of leading Tanzania newspapers, The Guardian and Nipashe, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:**

### CIRCULATION FIELD OFFICER – DAR ES SALAAM

**Job Purpose:**

To boost copy sales and develop relationships with agents and vendors in the sales channel in the assigned area to meet your set sales targets.

**Main Responsibilities:**

The successful candidates will be responsible for the following key results:

- Work with the agents and vendors in making sure that the business grows and The Guardian Limited publications are available and visible and sold at the set retail prices with optimal return levels.
- Develop and grow more channels of distribution.
- Monitor indicators relating to market arrivals, circulation sales and returns indicators and make appropriate reports to Circulation Supervisor.
- Identify and build rapport with existing and potential customers by communicating the benefits of Selling The Guardian and Nipashe.
- Monitor newspaper distribution and sale trends in particular areas, prepare weekly sales plans and update supervisor on a regular basis.
- Monitor daily performance of TGL brands in your particular areas of operation in comparison to our rival publications and make reports that guide growth strategies.
- Open up new markets in particular areas of operation that will in turn translate into higher sales.
- Attend customer complaints that in one's particular area of operation so as to maintain good customer relations and protect the company's interests.
- Liaise with supervisor in credit control and debt management within particular area of operation.
- Submit daily and weekly reports on progress on activities, including meeting set sales targets.
- Manage debt collection and credit control within one's respective area operation.
- Demonstrate ability to work under minimum supervision.

**Minimum Qualifications and Experience:**

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 2 year's relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge, and familiarity with a wide range of newspapers brands.

**MODE OF APPLICATION:**

Apply online via HRO email address: ;**vacancy@guardian.co.tz** by March 13, 2020

NB: Only shortlisted candidates will be contacted.

***The Guardian Limited is an equal opportunity employer.***

615654302


# Trafiki hatarini kupoteza usikivu

**Na Mary Geofrey**

ASKARI wa Usalama Barabarani, maarufu trafiki, na wafanyakazi viwandani, wako hatarini kupoteza usikivu kutokana na kufanya kazi kwenye mazingira yenye kiwango kikubwa cha sauti.

Kwa kawaida kiwango cha ukubwa wa sauti (Decibel) kinapaswa kuwa 40 hadi 60, lakini trafiki na wafanyakazi wa viwandani wanafanya kazi katika kiwango cha 85 hadi 120 ambacho ni hatari kwa usalama wa masikio yao.

Daktari Bingwa wa Masikio, Pua na Koo wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Edwin Liyombo, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika kuadhimisha Siku ya Usikivu Duniani.

Maadhimisho yalifanyika kwenye Tawi la Mloganzila kwa kutoa huduma ya kupima masikio bure kwa Watanzania waliojitokeza kupata huduma hiyo.

Dk. Liyombo alisema trafiki na wafanyakazi wa viwandani wanafanya kazi kwenye kiwango kikubwa cha sauti, hivyo wanapaswa kufanya kazi kwa saa nane kwa siku ili kuepuka tatizo hilo la kupoteza usikivu.

"Kutibu tatizo la usikivu ni gharama kubwa kiliko kuzuia tatizo, hivyo kama madaktari tuna wajibu wa kutoa elimu kwa jamii kuepuka kukaa au kufanya kazi kwenye mazingira yanayoweza kusababisha kupoteza kiwango cha usikivu au wachukue tahadhari kwa kuvaa vifaa vya kupunguza sauti.

"Mfano mzuri ni matrafiki ambao wametajwa hata kwenye ripoti za dunia kuwa wapo hatarini kupata tatizo la usikivu kwa sababu ya kufanya kazi kwenye mazingira ya 'Decibel' ya 85 na wafanyakazi wa viwandani ambao wakati wote mashine zinanguruma.

Aliilitaja kundi lingine ni vijana kuanzia miaka 12 hadi 35 ambao wanasikiliza muziki kwa sauti kubwa zaidi kwa muda mrefu bila kuchukua tahadhari.

"Hawa ni wengi na hasa wapiga muziki kwenye nyumba za starehe maarufu kama DJ, wao wanaweka muziki hadi mwisho ili kusikiliza mdundo na kadiri siku zinaenda anapoteza usikivu bila kujua, dalili moja wapo ni kuongeza kiwango cha sauti wakidhani ni ndogo kumbe wanazidi kuua masikio," alisema.

Alibainisha kuwa takwimu za dunia zinaonyesha watu milioni 466 wana tatizo la usikivu. Kati yao, milioni 34 ni watu wazima na asilimia 60 ya wagonjwa sababu zake zinazuilika.

Alisema nchini hakuna takwimu halisi zinazoonyesha kiwango cha tatizo lakini makadirio ni kati ya watu 20, mmoja ana tatizo la usikivu.

Akizungumza upimaji huo wa bure, Daktari Bingwa wa Msikio, Pua na Koo, Dk. Jaria Rahib, alisema mwaka jana walitoa huduma ya upimaji bure na kati ya watu 497 waliojitokeza, 197 walibainika kuwa na tatizo.

# Watakiwa kupima gesi kabla matumizi

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

WAFANYABIASHARA wa gesi ya kupikia (LPG), Kanda ya Ziwa, hususani wasambazaji wametakiwa kuhakikisha mitungi ya gesi inakuwa na uzito sahihi na wafanyabiashara kuzingatia sheria, kanuni, utaratibu na usalama.

Wito huo ulitolewa na Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura) Kanda ya Ziwa, George Mhina, katika semina ya kuwajengea uwezo wasambazaji wa gesi kutoka mikoa saba ya Kanda ya Ziwa ikiwamo Kigoma, Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Simiyu na Geita, iliyoandaliwa na mamlaka hiyo ilifanyika, jijini Mwanza, alisema wamewafundisha namna ya kuhifadhi mitungi sehemu za kivuli na kuiweka mita nane kutoka eneo la kupikia.

Aliwataka kuwa na vifaa vya kupimia uzito na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu kinyume chake adhabu kali itafuata kwa kuwa Ewura inafanya ukaguzi wa mara kwa mara na sheria inawapa mamlaka ya kutoza faini.

"Tumesisitiza watu wanaouza na kusambaza gesi sehemu zao za kuuzia wahakikishe kuwa wanaweka mizani ya kupimia mitungi yao pamoja na kuwaelimisha wateja wao namna bora ya utunzaji, usafirishaji wa gesi, changamoto Watanzania tunatumia usafiri wa bodaboda wakati gesi inapaswa kusafirishwa ikiwa mtungi umesimama na kuhakikisha sili ipo taiti," alisema.

Pia alisema, matumizi ya gesi ya kupikia ni muhimu kwa kuwa inatunza mazingira pia gharama zake ni nafuu.

Mkaguzi Mwandamizi wa petroli Ewura Kanda ya Ziwa, Mhandisi Joseph Shija, alisema lengo la mafunzo hayo kwa wauzaji wa gesi ya kupikia (LPG) ni kujizatiti katika masuala ya usalama na kufuata sheria na taratibu, pia mamlaka hiyo inafahamu changamoto ya uchakachuaji wa gesi hiyo kutokana na ujazaji haramu kwenye mitungi.

Alisema, Ewura itaendelea kushirikiana na kampuni za LPG kuwabaini wafanyabiashara wanaojihusisha na vitendo hivyo kwa kuchukua hatua stahiki na hivi karibuni itaanza kuchukua hatua za kisheria dhidi ya LPG wasambazaji ambao hawana leseni ya mamlaka hiyo.

**"Tumesisitiza watu wanaouza na kusambaza gesi sehemu zao za kuuzia wahakikishe kuwa wanaweka mizani ya kupimia mitungi yao pamoja na kuwaelimisha wateja wao namna bora ya utunzaji, usafirishaji wa gesi, changamoto Watanzania tunatumia usafiri wa bodaboda wakati gesi inapaswa kusafirishwa ikiwa mtungi umesimama na kuhakikisha sili ipo taiti," alisema.**

# Nyanza kuanza ununuzi mazao ya kimkakati

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

CHAMA Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Mwanza (Nyanza 1984 Limited), kinatarajia kuanzisha ununuzi wa mazao ya kimkakati ya biashara dengu na choroko, kupitia mfumo wa ushirika wa stakabadhi ghalani.

Akizungumza na Nipashe, Kaimu Meneja Mkuu wa chama hicho, Martha Ndeto, alisema kuwa chama hicho kitakuwa kinakusanya mazao hayo kupitia vyama vya msingi vya ushirika vya mazao (Amcos).

"Tunatarajia mwaka huu kuanzia Machi kuanza kununua mazao ya kimkakati ya biashara, kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani...sisi kazi yetu ni kukusanya mazao hayo kupitia vyama vya msingi vya ushirika vya mazao ili kampuni zinazonunua zije kununua kupitia ushirika kwa njia ya mnada," alisema Ndeto.

Ndeto alisema serikali inajitahidi kuboresha vyama vya ushirika lengo wakulima waweze kuuza mazao yao kwa bei nzuri yenye faida pamoja na kuepuka kupunjwa bei na kampuni binafsi zinazonunua mazao hayo.

Alisema wakulima wamekuwa wakiuza mazao hayo kiholela kwa kampuni binafsi kwa kutumia visado badala ya kupima kwenye kilo, jambo ambalo linawafanya wasinufaike na kilimo cha mazao ya kimkakati ya biashara.

Alizitaka mamlaka zote zinazohusika na usimamizi wa mazao ya wakulima ya kimkakati mkoani Mwanza kushiriki kikamilifu katika kutimiza wajibu wao, ili kusaidia kuwainua wakulima kiuchumi, kwani mfumo utakaotumika hivi sasa utazinufaisha pia Amcos pamoja na Nyanza katika kukuza uchumi wake.

Alisema Amcos hivi sasa zimeshindwa kujiendesha zenyewe katika utekelezaji wa majukumu yake, kutokana na kutolipwa fedha za ushuru wa pamba, na baadhi ya makampuni ya ununuzi wa zao hilo tangu msimu uliopita 2019 ulioanza Mei.

Ndeto alifafanua kuwa wakulima mwaka huu mkoani Mwanza, wameshindwa kulima pamba kwa wingi kama mwaka jana kutokana na kuwapo mvua nyingi ambayo pamba haiwezi kustawi katika maeneo mengi.



Ofisa Elimu Taaluma wa Halmashauri ya Wilaya Masasi DC, mkoani Mtwara, Rajabu Said, akizungumza na wazazi, walezi na wanafunzi katika sherehe za kuadhimisha miaka 10 tangu kuanzishwa kwa Shule ya Msingi Nakachindu, wilayani humo jana. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# Wanachama wailalamikia NIC malipo

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

SHIRIKA la Bima la Taifa Tanzania (NIC) Tawi la Shinyanga, limedaiwa kutowalipa wanachama wake fedha wanazodai za makato ya kila mwezi kwenye mishahara yao kwa ajili ya bima ya maisha.

Lawama hizo zimetolewa jana na wanachama zaidi ya 10 wakati wakizungumza na vyombo vya habari.

Walidai shirika hilo kuwazungusha kuwalipa madai yao, pamoja na kuorodheshewa malipo ya madai tofauti na yale waliyokuwa wakikatwa kwenye mishahara, huku wengine wakinyimwa mikataba ya madai hayo.

Mmoja wa wanachama hao, Benedicto Mandago, ambaye ni mwalimu wa Shule ya Sekondari Ihugi, wilayani Shinyanga, alisema aliingia mkataba na shirika hilo kukatwa bima ya maisha tangu mwaka 2015 na Januari mwaka huu ilipaswa apewe fedha zake, lakini anazungushwa.

Alidai, fedha walizokubaliana kukatwa kwenye mshahara kwa mujibu wa mkataba ni tofauti na kushangaa kiasi kuongezeka cha makato kinyume na makubaliano, huku akiandikiwa kulipwa fedha za makubaliano ya awali na kutoongezeka, jambo ambalo amedai ni dhuluma.

"Mimi niliingia mkataba na Shirika hili la Bima mwaka 2015 na mkataba wangu ulikuwa unaisha Januari 2020 na tulikubaliana nikatwe Sh. 50,000, kila mwezi kwenye mshahara wangu, lakini nimeshangaa kuona nilikuwa nakatwa Sh. 51,915 tofauti na makubaliano, hii ni dhuluma kabisa," alisema Mandago.

Naye Mtedaji wa Kijiji cha Luhaga, Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, Dalali Mayunga, alisema aliingia mkataba na shirika hilo mwaka 2007 na ulikuwa unaisha 2018, lakini hadi leo anapofuatilia malipo ya madai yake anazungushwa.

Akizungumzia madai hayo, Kaimu Meneja wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), tawi la Shinyanga, Hamis Mohamed, alikiri kuwapo na madai ya wanachama hao na kubainisha wapo zaidi ya 300, huku akifafanua hawaja dhulumiwa bali madai yao yameshawasilishwa makao makuu na wiki ijayo watalipwa fedha zao.

HABARI KITAIFA

# Shinyanga yamkosha waziri eneo la uwekezaji viwanda

**Na Mwandishi Wetu, KAHAMA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, amepongeza uongozi wa Mkoa wa Shinyanga kwa kutenga jumla ya hekta 23,289.25 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda ambapo viwanda vitatu vikubwa vitajengwa na kuzalisha ajira zaidi ya 6,000.

Akizungumza baada ya kufanya ziara ya kutembelea maeneo hayo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji katika Halmashauri ya Mji Kahama, Waziri Kairuki aliitaka mikoa mingine kuiga mfano wa Mkoa wa Shinyanga.

"Hii ni hatua nzuri katika utekelezaji wa azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025. Utengaji wa maeneo ya uwekezaji ni hatua nzuri katika kuweka mazingira rafiki na wezeshi kuvutia wawekezaji," alisema Waziri Kairuki.

Alisema kutenga maeneo ya uwekezaji sambamba na kujenga miundombinu wezeshi kama barabara na maji kutavutia wawekezaji wengi kujenga viwanda na kuongeza ajira na hatimaye mkoa kupiga hatua katika maendeleo ya kiuchumi.

"Nimeambiwa zaidi ya hekta 23,289 zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa na wito wangu kwa wafanyabiashara ni kwamba wachangamkie fursa hii ya kujipatia maeneo na kufanya uwekezaji," alisitiza.

Akiwa ameambatana na Mkuu wa Mkoa huo, Zainab Taleck, pamoja na viongozi waandamizi mkoa, Kairuki alisema maeneo hayo yanayolewa bure kwa kulipia tu gharama za hati pekee juhudi za serikali kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji na wafanyabiashara kujenga viwanda.

"Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa wafanyabiashara na wawekezaji kuhakikisha uwekezaji wao unafanyika katika mazingira wezeshi ili kuchochea ukuaji wa uchumi," alisema.

Aidha, Waziri Kairuki aliwataka wote waliopewa maeneo ya uwekezaji wa viwanda vidogo na vikubwa kutobadili matumizi ya ardhi kwani madhumuni ya kupewa hayo maeneo ni utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi hivyo ni lazima ardhi itumike kutokana na malengo yaliyokusudiwa.

Kwa upande wake, Taleck alisema kiasi cha shilingi 809,400,000 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na umeme ili kuvutia kwa ujenzi wa viwanda.

"Viwanja vidogo vidogo zaidi ya 623 vimepimwa kwa kuvigawa hasa kwa vijana ili waweze kufunga mashine mbalimbali kwa ajili ya kupasua mbao, kuchomelea," alisema na kuongeza kuwa lengo likiwa kuwatengenezea vijana ajira za uhakika.

Mmoja wa wanufaika wa maeneo hayo ambaye ameshajenga kiwanda cha kutengeneza samani, Ally Abed, alishukuru serikali kwa kutenga eneo la uwekezaji na kumpa kiwanja ambacho amelipia shilingi 300,000 tu kwa ajili ya hati na kuendelea na shughuli zake.

## Waziri Mkuu awahakikishia wawekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na wawekezaji katika sekta mbalimbali nchini, wakiwamo wenye viwanda vya kuzalisha saruji.

Amesema katika kuhakikisha inalinda viwanda vya ndani vya kuzalisha saruji, serikali imeamua kuzuia uingizwaji wa saruji kutoka nje ya nchi.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa kiwanda cha saruji cha Simba alipotembelea kiwanda hicho akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Tanga.

Alisema licha ya serikali kupata kodi kutokana na uwapo wa kiwanda hicho, pia kimesaidia katika kutatua changamoto ya ajira hususani kwa vijana.

Naye, Waziri wa Madini, Doto Biteko, aliupongeza uongozi wa kiwanda hicho kwa kuwa wanazingatia sheria zote za madini ukilinganisha na viwanda vingine.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Reinhardt Swart, alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha tani milioni 1.25 kwa mwaka, lakini kutokana na mahitaji ya soko kinazalisha tani milioni 1.075 kwa mwaka.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa kiwanda hicho kimeajiri jumla ya wafanyakazi 319 kati yao wazawa ni 316 na watumishi watatu ni raia ya kigeni.

Pia, mkurugenzi huyo alitumia fursa hiyo kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.



Abiria wakipita kwa shida kutokana na matope, baada ya kushuka kutoka kwenye mabasi ya daladala katika stendi ya Kawe jijini Dar es Salaam wmwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kibiti walalamikia mtumbwi kubeba wajawazito

**Na Yasmine Protace, KIBITI**

DIWANI wa Kata ya Maparoni katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti mkoani Pwani, Ngachoka Haji, ameomba kata hiyo ipatiwe boti ili wagonjwa na wajawazito wasitumie usafiri wa mitumbwi kama ilivyo kwa sasa wanapokwenda kutafuta huduma za kiafya.

Ngachoka aliyasema hayo, katika kikao cha robo mwaka cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo.

Alisema katika kata yake mitumbwi ndio imekuwa ikitumika kuwabeba wagonjwa, hivyo inatakiwa kuwapo na boti ya kubeba abiria.

"Ni muhimu kuwapo na boti ambayo itawabeba abiria na sio kama ilivyo sasa mitumbwi kutumika kubeba wagonjwa wajawazito na abiria," alisema.

Aliongeza kuwa boti ilikuwapo, lakini cha kushangaza imechukuliwa na sasa inatumika kufanya doria katika maeneo ya delta.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Khatibu Chaurembo, alisema kuwa atalifuatilia suala hilo ili kujua kama ni kweli boti imechukuliwa, na kusababisha wananchi kupata shida ya usafiri.

Alisema kuwa kiasi cha Sh. milioni 140, kilitolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kununuliwa kwa boti hiyo, ambayo itasaidia wakazi wa ukanda wa delta.

Alisema walishatoa ushauri boti hiyo iwe ya abiria ili iwasaidie kuongeza mapato delta ya kusini na kaskazini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Mohamed Mavulla, alisema kuwa boti ilikuja na idhini na fedha za kuinunua ilitolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Alisema boti hiyo ililetwa kwa ajili ya kufanya doria, hivyo hawawezi kuvunja mkataba.

# Mbunge aombea umeme wafugaji

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

MBUNGE wa Simanjiro, James Ole Milya, amewaomba Wakala wa Umeme Vijijini (REA), kuwanusuru wafugaji wa Kata ya Terati wilayani Simanjiro mkoani Manyara, kwa kuwapelekea huduma ya umeme.

Alitoa ombi hilo juzi mbele ya wajumbe wa Bodi ya REA, ambao walitembelea eneo hilo.

Alisema Kijiji cha Terrat kina maendeleo makubwa ikiwamo viwanda, visima vya maji pamoja na shule nyingi za msingi na sekondari, hivyo kuwapo kwa umeme kutaleta chachu ya maendeleo katika eneo hilo.

"Umeme ukifika katika eneo hili kutawawezesha vijana wengi wanaokaa mtaani kupata ajira kwa kuwa watafungua biashara ndogo kama saluni, kuchomelea vyuma na kazi nyingine," alisema Milya.

Mwenyekiti wa Bodi ya REA, Julius Kalolo, alisema baada ya kutembelea maeneo hayo, na kusikiliza kero ya wananchi, watahakikisha Machi mwaka huu umeme utafikishwa katika eneo hilo.

Kalolo alisema mwishoni mwa Machi mwaka huu, wananchi wa Terati watapata huduma ya umeme.

Mkurugenzi wa Kiwanda cha Maziwa cha IOPA, Martin Sanin'go, alisema kukosekana kwa umeme katika kijiji hicho, kumesababisha kufungwa kiwanda chao.

Alisema katika Kata ya Terati kiwanda hicho, ni moja ya kitega uchumi kwa wanawake wanaoishi maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Simanjiro.

# Makada CCM watifuana ubunge Simanjiro

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

WAKATI joto la uchaguzi likizidi kushika kasi nchini, Kamati ya Maadili na Usalama ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Simanjiro mkoani Manyara, imepanga kumwita aliyewahi kuwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Peter Ole Toima, kwa kupanga mikakati ya kupitishwa kugombea ubunge wa jimbo hilo.

Mbali na tuhuma hizo, pia kamati hiyo imepanga kumhoji kada huyo, kuhusu ugomvi na Mbunge wa jimbo hilo, James Ole Milya.

Ugomvi wa makada hao, umesababisha kufikishana mbele ya Jeshi la Polisi wilayani humo.

Hivi karibuni Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, aliwaonya wanachama wa chama hicho, walioanza mikakati ya kugombea nafasi za ubunge, udiwani na urais, na kusisitiza kuwa kufanya hivyo ni makosa kwa mujibu wa katiba ya chama hicho.

"Watu walionza mikakati ya kutaka kupitishwa kugombea nafasi za ubunge, udiwani na urais hawatavumiliwa kwa kuwa taratibu za kuwania nafasi mbalimbali ndani ya chama zipo wazi na zina muda wake," alisema Bashiru.

Kuna taarifa kuwa kamati hiyo imepanga kumwita Toima ili kujibu tuhuma za kuanzisha harakati za kugombea nafasi ya ubunge kwa kutumia mwamvuli wa Taasisi yake ya ECLAT Foundation.

Toima anatuhumiwa kuitisha mikutano katika maeneo mbalimbali wilayani humo kwa kuitumia taasisi hiyo kama sehemu ya kugawa misaada katika sekta ya elimu, maji na afya.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Simanjiro, Awadh Omar, alipoulizwa kuhusu taarifa hizo, alithibitisha ni za kweli na kuwa chama hicho kimepanga kumwita kada huyo kumuhoji baada ya kupokea taarifa kuwa amekuwa akifanya kampeni kabla ya muda.

Awadhi alisema kamati itamwita kada huyo ili kujibu tuhuma zilizofikishwa mbele ya chama hicho.

"Kamati ya Usalama na Maadili itamwita na kumuuliza mambo yote aliyofanya kwa chama kimepokea taarifa kutoka Kitongoji cha Mazinde Kata ya Loborsoit, wakati akikabidhi madarasa," alisema Omar.

Katibu wa CCM wilayani humo, Ally Kitunda, alisema kumekuwapo mgogoro kati ya kada huyo na Milya.

Alisema sababu ya ugomvi huo haijajulikana na chama kimepanga kuwaita ili kujua sababu ya uhasama wao.

Milya alithibitisha kuitwa na Jeshi la Polisi wilayani humo Februari 20, mwaka huu, kwa ajili ya kuhojiwa kuhusu madai ya kumtolea maneno makali Toima katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kijiji cha Namalulu.

Milya alisema tangu alipoweka wazi msimamo wake kuhusu kampuni ya uchimbaji wa madini ya Tanzanite One, baadhi ya viongozi wa serikali na CCM wilayani humo wamekuwa wakimchukia, na wamekuwa na mipango ya kuwabeba baadhi ya wagombea kwa malengo ya kumdhoofisha kisiasa.

"Nilipokwenda kwenye mazishi Kijiji cha Namalulu, nilipewa taarifa kuwa Toima ana mkutano wa hadhara eneo hilo, na mimi kama Mbunge nilikwenda kushuhudia nini kinachoendelea, lakini baada ya muda nilishangaa kuitwa polisi kwa tuhuma nimemtolea maneno makali," alisema. Milya ambaye mwaka 2015 alijitoa CCM kwenda Chadema na kuchaguliwa kuwa mbunge kisha mwaka juzi kurejea CCM.



Mama mjasiriamali aliyejitambulisha kwa jina la Rose, akionyesha mvinyo alioutengeneza, wakati wa maonyesho ya wajasiriamali wadogo yaliyoandaliwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), wilayani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Waziri aagiza mkandarasi kunyang'anywa miradi 17

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, ameagiza mkandarasi wa Kampuni ya STC, kunyang'anywa kandarasi zote za ujenzi mkoani wa Arusha, kutokana na kushindwa kukamilisha kwa wakati miradi ya maji.

Kampuni hiyo itanyang'anywa kujenga miradi yote ya maji nchini, aliyoingia kandarasi ya ujenzi.

Waziri Mbarawa alisema atapita kukagua yote na wizara itaichukua ili kuiendeleza.

Alitoa agizo hilo juzi jijini Arusha wakati wa ziara yake ya kikazi ya siku tatu katika wilaya za Arusha, Arumeru na Monduli.

Alihoji kwa nini mkandarasi huyo amepewa miradi 17 ya kujenga hapa nchini wakati hana vigezo vya kutekeleza miradi hiyo.

"Mkandarasi huyu kati ya miradi yote ni mmoja tu ndio amekamilisha, tena kwa kusukumwa ambao ni wa maji wilayani Longido, siwezi kuendelea kumvumilia tena," alisema.

"Nasisitiza mwacheni aondoke zake, miradi hiyo tutaifanya sisi wenyewe... Wizara kuanzia Machi wananchi wapate maji kwa kuwa makandarasi wanatuchezea sana," alisema.

Aidha, alisema mkandarasi huyo amekuwa na zabuni nyingi za ujenzi, lakini miradi yote aliyojenga hairidhishi.

Pia alisema wizara imetoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya mradi wa maji Kijiji cha Loosikito katika Kata ya Mwandeti.

Awali Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha (AUWSA), Justine Rujomba, alisema tangi kuu la maji lenye ujazo wa mita 10,0000 lililojengwa Ngaramtoni wilayani Arumeru, limekamilika na ndani ya miezi minne ijayo tatizo la maji katika Jiji la Arusha litakwisha.

Aliishukuru serikali kutoa zaidi ya Sh. bilioni 520, kwa ajili ya usambazaji wa maji katika Jiji la Arusha.

Alisema mradi huo una matangi 11 na kati ya matangi hayo tisa yamekamilika.





# Muwsa yatekeleza agizo la Mbarawa

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Moshi (Muwsa) imeanza kutekeleza agizo la Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, la kufunga mita za maji za malipo katika makazi ya watu na taasisi za umma.

Taarifa ya Kaimu Meneja wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Aron Joseph, inaeleza kuwa kazi hivi sasa inaendelea katika maeneo mbalimbali wilayani hapa.

"Ni kweli tumeshaanza kutekeleza agizo la Waziri wa Maji la kufunga mita za prepaid (mita za maji za malipo kabla) kwa wateja wapya na kimsingi tumeshaanza utekelezaji wake katika makazi ya watu na taasisi zote za umma. Tunafanya hivyo ili kuwadhibiti wadaiwa sugu wasiendelee kuitia hasara mamlaka," alisema.

Kwa mujibu wa Mhandisi huyo, taasisi za umma zilizofungiwa mita hizo ni pamoja na Jeshi la Polisi, Magereza na Shule ya Polisi Moshi (MPS).

Hadi sasa, taasisi za umma mkoani Kilimanjaro ikiwamo Jeshi la Polisi, Magereza na Shule ya Polisi Moshi wanadaiwa zaidi ya Sh. bilioni 2.3

Mhandisi huyoa lisema kufungwa kwa mita za maji za malipo kabla zitasaidia kudhibiti madeni sugu ambayo yamekuwa yakikwamisha mamlaka hiyo kujiendesha kwa ufanisi zaidi.

Alisema itaanza kuwafungia mita za maji za malipo kabla kwa kila nyumba ya askari Polisi, badala ya kutumia mita moja ambayo pia ilikuwa ikitumiwa na ngome kuu na hivyo kufanya matumizi kuwa makubwa zaidi, na hivyo ngome kushindwa kusitishiwa huduma pale deni linapozidi kuwa kubwa.

Aidha, Mhandisi Aron alisema Muwsa imeshapata mita za malipo kabla zipatazo 97 ambazo zitafungwa katika taasisi za umma.

Alisema lengo la zoezi hilo ni kuhakikisha Muwsa haiendelei kulimbikiza madeni kwa taasisi za umma na makazi ya kila askari na kwamba pamoja na kufunga mita hizo, madeni yote ya nyuma wanayodai taasisi yatapaswa kulipwa na taasisi husika.

Ofisa Uhusiano wa Muwsa, Rashid Nachani, alisema mamlaka hiyo pia inakusudia kuanza zoezi la kuzijengea chemba zote za maji zilizopo mjini Moshi ili kuongeza usalama kwa watumia huduma ya maji, kwa kuwa chemba nyingi ni chakavu hazina vifuniko.

"Tunakuja na utaratibu wa kujenga chemba maalumu kuwa za aina moja na tutazijenga katika maeneo sahihi kwani nyingi zilijengwa katika maeneo ambayo siyo sahihi na kuzifungia ufuniko kwa ajili ya kuimarisha usalama," alisema Rashid.

# Mvua yakosesha makazi kaya 39 Hai

**Na Godfrey Mushi, HAI**

MVUA za masika zilizoanza kunyesha juzi jioni katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini hasa mkoa wa Kilimanjaro, zimesababisha kaya 39 kukosa makazi katika Kijiji cha Sanya Station kilichopo Kata ya KIA, Wilaya ya Hai.

Kitongoji cha Palestina kilichopo Kijiji cha Sanya Station, ndicho kilichoathirika zaidi baada ya mvua kubwa iliyokuwa imeambatana na upepo mkali, kuezua paa za nyumba hizo na nyumba tano kubomoka kabisa.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Moses Mbaayo, alisema mvua hiyo iliyoanza Machi 2, mwaka huu, majira ya saa 12:00 jioni imesababisha kaya hizo kukosa makazi, huku ikisababisha madhara ya kiafya kwa mtoto wa miaka minne aliumia baada ya kuangukiwa na kitu kizito.

Kwa mujibu wa Mbaayo, mtoto huyo alikimbizwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC kwa ajili ya matibabu.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Hai, Upendo Wella, alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhisiana na taarifa hiyo ya mvua, alisema atafutwe baadaye ili afuatulie na kupata taarifa kamili ya walioathirika.

Hivi karibuni, Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA), ilitoa utabiri wa mvua za masika kwa kipindi cha Machi hadi Mei, 2020 ambazo zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani.

Mvua hizo zinatarajia kunyesha katika maeneo ya Mkoa wa Tanga, Visiwa vya Unguja na Pemba, maeneo mengi ya Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro, Mashariki mwa Mkoa wa Geita pamoja na mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara.

Maeneo mengine ni ya Mkoa wa Kagera, Magharibi mwa Mkoa wa Geita, Kaskazini mwa mkoa wa Kigoma, Dar es Salaam, Pwani (ikijumuisha kisiwa cha Mafia) pamoja na kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani.

Huku mvua za nje ya msimu zinazoendelea kunyesha katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hususan yaliyopo katika pwani ya kaskazini zinatarajiwa kuendelea na kuungana na msimu wa mvua wa masika 2020.



Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi, Michael Mwandezi (aliyevaa koti), akiwa na viongozi wa Kamati ya Siasa ya CCM ya Wilaya na Mkoa wa Kilimanjaro, kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa stendi ya kimataifa ya mabasi katika eneo la Ngangamfumuni, mjini Moshi, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wanawake walalamikia mamlaka kukwama mashauri ukatili kijinsia

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

VIONGOZI wa majukwaa ya wanawake wanaotoka kwenye halmashauri saba za mkoa wa Kilimanjaro, wamelalamikia baadhi ya mamlaka za serikali zilizopewa jukumu la kutekeleza sheria, kutoshughulikia mashauri yanayohusu mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Jana, kwa nyakati tofauti viongozi hao wanaounda Jukwaa la vuguvugu la ukombozi wa mwanamke kimapinduzi (Tapo) Mkoa wa Kilimanjaro, walieleza masikitiko yao kuhusu baadhi ya madawati yanayoshughulikia kesi za ukatili zinafika kwao, lakini hazichukuliwi hatua zaidi.

Walitoa malalamiko hayo, wakati wa kikao kazi cha pamoja cha tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango kazi wa Tapo katika kila wilaya.

Mwenyekiti wa Jukwaa hilo Wilaya ya Siha, Rhoda Mshomi, alisema mara kadhaa wamekuwa kikatishwa tamaa na baadhi ya waliopewa mamlaka ya kushughulikia kesi hizo hasa madawati ya Polisi wakati mwingine wanamaliza mashauri hayo kimya kimya pasipo kuyapeleka mahakamani.

Aidha, Mratibu wa mradi wa nguvu ya pamoja katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia katika mkoa wa Kilimanjaro, Veronika Ullomi, alisema:

"Tatizo kubwa ambalo limebainika ni ushirikiano mdogo kutoka kwa waathirika wa ukatilili wa kijinsia ambao wanawashughulikia kwamba watu wanatoa taarifa sawa, na Tapo inachukua hatua wanapeleka malalamiko Polisi au Ustawi wa Jamii, lakini mwisho wa siku, wale waaathitika wanarudi nyuma wanamaliza masuala yao nyumbani.

"Kana kwamba haitoshi, kuna suala pia la ushirikiano hafifu katika taasisi za serikali kwa mfano kuna baadhi ya madawati yamelalamikiwa kwamba kesi zinafika pale, lakini hazichukuliwi hatua zaidi. Yaani zinaishia pale pale dawati na hawaoni zinaenda labda mahakamani... na ni matukio mazito kwa mfano suala la ubakaji ambalo wana Tapo walilifuatilia wakapeleka taarifa Polisi, walikiuliza suala la kwenda mahakamani wanapigwa chenga, kwa hiyo kuna tatizo kama hilo imejitokeza."

Katibu wa Jukwaa hilo Wilaya ya Same, Peniel Malimbwi, alisema Tapo kwa kushirikiana na Ofisa Ustawi wa Jamii, katika kutekeleza jukumu hilo wamefanikiwa kumkamata mama mmoja ambaye ni mlevi ambaye ana desturi ya kumfungia ndani mtoto wa miezi mitatu na kwenda baa kulewa.

"Baada ya kumkamata na kukaa nae kumpa elimu wala hakusikia kabisa na mwisho wa yote ikabidi sasa tufanye mchakato wa kumnyang'anya mtoto na huyo mwanamke ni mkazi wa Moshi," alieleza Malimbwi.

Hata hivyo mama huyo, baada ya kunyang'anywa mtoto na yeye alichukuliwa na ndugu zake na kurejeshwa Moshi.



Ukurasa 20

**Jambo la 50/50 Uchaguzi 2020**

Sudan inavyoonja shubiri ya wafadhili ikijikwamua



Ukurasa 19



Ukurasa 18

**Kifuatacho baada ya BVR kiwe mafunzo elimu uraia**


# siasa

JUMATANO MACHI 4, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 17

**Netanyahu adai kushinda uchaguzi uliofanyika Israel**

# ‘Safari ya matumaini’ tarajiwa ya kada Membe inaishia wapi?

**Na Ani Jozeni**

KUNA msemo wa falsafa kuwa historia inajirudia, lakini siyo kwa mazingira yale yale. Baadhi ya wanafasihi wanasema mara ya kwanza tukio hilo la kihistoria linakuwa ni mkasa, ila linapojirudia inakuwa ni mzaha.

Ndivyo ambavyo inawezekana tukio la uchaguzi mkuu uliopita lijirudie mwaka huu, lile la ‘safari ya matumaini,’ kutokana na mtangaza nia mahiri uchaguzi wa mwaka 2015 Edward Lowassa, ‘kukatwa’ na chama chake. Safari hii kilichokatwa si jina la mtangazania ila la mwanachama mkongwe kufukuzwa na chama chake cha Mapinduzi -CCM, anayefukuzwa ni Bernard Membe.

Hata hivyo kinachowapasua vichwa baadhi ya watu ni hatma ya kada Membe, je itakuwaje?

INAENDELEA UK.16



Bernard Membe. **PICHA: MTANDAO**

**Utaratibu huu utazima wanaotumia mlungula** Ukurasa 14




Katibu Mkuu wa CCM, Bashiru Ally. **PICHA: MTANDAO**

# Utaratibu huu utazima wanaotumia mlungula

**Na Reubeni Lumbagala,**

DODOMA

WENYE NIA ya kugombea nafasi za uongozi kwa kutumia nguvu ya mlungula safari hii wanaambiwa watafakari njia zao, kwani wapo wanaoibuka kidedea kura za maoni lakini kwa kutumia mbinu za kupenyeza rupia.

Kwa kawaida kabla ya kupewa kibali cha kupeperusha bendera ni lazima kuomba kwanza ridhaa ndani ya vyama kwa hiyo lazima wagombea wampitishe mhusika ambaye anapigiwa kuwa za maoni.

Inaamaanisha kuwa wanaowania nafasi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, uwe udiwani , uwakilishi na ubunge, kabla ya kupitishwa kuwakilisha vyama vyao, huanzia kuomba ridhaa ndani ya vyama vyao ambapo wanachama ndiyo wanaoanza kuwapigia kura.

Ni utaratibu ambao wagombea na walioongoza kwa kura nyingi katika kupigiwa na kura za maoni hupitishwa na vyama vyao kupambana na wagombea wengine ili kutafuta mshindi mmoja wa kuwakilisha kata au jimbo ili kuwatumikia wananchi wote bila kuzingatia itikadi za vyama, dini wala kabila.

Mara nyingi wale wanaojipanga kugombea nafasi mbalimbali za uongozi, hupanga mapema namna ya kupata kura za wajumbe ili kupitishwa kugombea.

Hii imepelekea baadhi ya wagombea kujitutumua kwa rushwa ya kuwahonga wajumbe wa ndani ya vyama vyao ili kupitishwa kwa kishindo.

> Aidha, sifa ya ziada ya mgombea kupitishwa ni pamoja na kukubalika kwake kwa wananchi ambao ndiyo wapiga kura.

Wapo wanaodaiwa kuwahonga wajumbe kwa kuwapatia fedha au kuwafanyia jambo linalowavuta. Mathalani, kinamama wanadaiwa kulipia fedha za vikoba. Kuna wengine wanaowapa kinababa fedha za michango inayohitajika kutolewa kwenye shughuli fulani.

Aidha wanadaiwa kuwa wengine hutoa pesa kwenye vikundi vya wanachama hasa wale ambao ni wanachama wa chama anachotaka kukiomba kura.

Ukweli ni kuwa hali hiyo inawafanya watu kuona kuwa mgombea aliyeongoza kura za maoni ndani ya chama si tiketi ya moja kwa moja kuwa mwenye nia huyo anakubalika nje ya chama yaani kwa wananchi wa eneo lake ambao ndiyo wapiga kura.

Kwa mantiki hiyo, mgombea anaweza akaongoza kwa idadi kubwa ya kura ndani ya chama lakini akawa hakubaliki kwa wananchi, kadhalika, mgombea anaweza akashindwa katika kura za maoni ndani ya chama lakini akawa anakubalika na ni kipenzi cha wananchi ambao ndiyo wenye kauli ya mwisho ya kuchagua aina ya kiongozi wamtakaye .

Chama Cha Mapinduzi kina utaratibu mzuri wa kupata wagombea wake katika safu mbalimbali za uongozi ambapo mgombea anapitia ngazi mbalimbali hadi kufikia hatua ya mwisho ya kupitishwa kugombea akishindana na wagombea wa vyama vingine katika uwanja wa mapambano.

Akiwa katika ziara za kuimarisha chama na kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya CCM katika Wilaya za Pangani na Muheza mkoani Tanga, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi Dk. Bashiru Ally, alitoa rai kwa wale wanaotaka kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama hicho kuwa kuongoza kura za maoni si sifa ya pekee na ya msingi kuteuliwa kugombea.

Katibu Mkuu Bashiru anaendelea kusema mchakato wa kuwapata wagombea wa kupeperusha bendera ya chama hautaangalia aliyeongoza kura za maoni pekee bali mgombea atapitia ngazi mbalimbali hadi kufikia ngazi ya mwisho ya maamuzi.

Aidha, sifa ya ziada ya mgombea kupitishwa ni pamoja na kukubalika kwake kwa wananchi ambao ndiyo wapiga kura.

Anawaambia zaidi kuwa :"Kura za maoni ni sehemu tu ya utaratibu, lakini si sifa mama kwa mwombaji wa nafasi ya ubunge ama udiwani. Unaweza kuongoza kwa kuhonga wajumbe, mtu huyo hatufai kwa kuwa wajumbe hao si wapigakura. Kinachoangaliwa pamoja na mambo mengine ni kukubalika kwake kwa wananchi ambao ndiyo watakaomchagua", anasisitiza.

Utaratibu huu upo ndani ya CCM, lakini katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, njia hiyo inaonekana itatumika kwa msukumo wa kipekee ili kuwapata wagombea bora wanaokubalika kwa wananchi katika nafasi za udiwani na ubunge ili kuwatumikia wananchi na kushirikiana na wapiga kura wao katika juhudi za kuleta maendeleo ya nyanja mbalimbali.

Ifahamike kuwa wajumbe wa ndani ya vyama ni wachache ambao kura zao pekee haziwezi kusababisha mgombea kushinda atakaposhindanishwa na watu wengine ambao ni chaguo la wananchi.

Hivyo basi, mgombea bora anayefaa kupeperusha bendera ya chama chake ni yule anayekubalika ndani na nje ya chama lakini hasa nje ya chama yaani anayekubalika kwa wananchi.

Katika kupigilia msumari wa moto dhidi ya wagombea wanaosaka uongozi kwa rushwa, Dk. Bashiru anasisitiza kuwa mwanachama aliyeongoza kura za maoni anaweza akawa ni chaguo binafsi la wajumbe, hivyo kikao cha mkoa au Taifa kitarejesha jina la mtu mwingine atakayeonekana anakubalika kwa wananchi hata kama katika mchakato wa kura za maoni ya chama alipata sifuri.

Vyama vya siasa vinatumia gharama kubwa kuwanadi wagombea wa vyama vyao, lakini kama mgombea atakuwa ni chaguo la wananchi kazi ya kunadi itakuwa nyepesi sana kwani kizuri chajiuza chenyewe.

Mgombea ambaye ni chaguo la wananchi anatoa uhakika wa chama chake kushinda katika ulingo wa ushindani wa kisiasa huku gharama ndogo ikitumika katika kampeni za kusaka kura.

Ni lazima wenye nia ya kugombea wakatanguliza dhamira ya kweli ya kuwatumikia wananchi wanaotaka kuwaongoza si kujinufaisha kupitia jukwaa la kisiasa.

Kiongozi ambaye ni chaguo la wananchi ni lazima apange kutumika akili, ujuzi, uzoefu na ubunifu wake katika kuzitafutia suluhisho shida za wananchi.

Itoshe kusema kiongozi wa aina hii ndiye anayehitajika, ambaye ataacha alama isiyofutika kwa wananchi anaowaongoza, na jina lake litaandikwa kwa wino wa dhahabu.

Tafakari.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali wilayani Kongwa mkoa wa Dodoma.***

MAKAMBA, KINANA;

# Hakuna aliye juu ya chama

Na Seif Khamis Gulamali



Makatibu wakuu wastaafu Kinana na Makamba. **PICHA: MTANDAO**

NIMEZALIWA na kukulia kijijini. Huko nimejifunza maana halisi ya kuheshimu, kulinda na kuzingatia mila, desturi, maadili na hata tamaduni za aina mbalimbali. Nilijifunza miiko ya kifamilia, ukoo, kijiji, jamii na taifa kwa ujumla.

Moja ya mambo makubwa niliyojifunza na kukua nayo katika maisha yangu yote, ni kwamba hakuna mtu mmoja anayeweza kuwa na nguvu kuliko familia, ukoo, jamii, kijiji, chama, kikundi au hata taifa. Kwamba, katika muungano wa aina yoyote haiwezekani akawa na nguvu au mamlaka ya kushinda muunganiko huo.

Ambacho hutokea ni baadhi ya wanachama kuwa na ushawishi wenye kuvutia kidogo kuliko wenzao kutokana na utendaji kazi wao, lakini hiyo haimaanishi kwamba mwanachama au mwanakikundi huyo anakuwa na nguvu au mkubwa kuliko wenzake, wengi huponzwa na umaarufu 'kiduchu' ambao hudhani wanao kutokana na kushangiliwa na wengi au watu walio nje.

Nipo kijijini kwetu Manonga-Igunga, nikiendelea na shughuli zangu za kulijenga taifa baada ya kumalizika kwa vikao vya Bunge jijini Dodoma, ambapo pamoja na wenzangu huungana kuwakilisha wananchi wenzetu, kama mbunge.

### SAKATA NDANI YA CCM

Nimelazimika kushika kalamu ili nitoe maoni na mawazo yangu, kufuatia sakata linaloendelea ndani ya chama changu cha CCM, ambacho kimetoa mwanga na taswira kubwa ya maendeleo kwa taifa. Tena kimekuwa chachu na nguzo kuu ya ukuaji wa uchumi tangu uhuru kutoka kwa wakoloni wa Kiingereza.

Sakata la baadhi ya viongozi wetu wastaafu, ambao binafsi ninawaheshimu sana kutokana na utumishi wao ndani ya chama na taifa kwa ujumla, waliolazimika kuitwa na kamati ya maadili inayoundwa na Makamu Mwenyekiti Bara, Philip Mangula, Katibu Mkuu, Dk. Bahiru Ally na wajumbe wengine ndani ya chama ni mambo mengi ambayo sina sababu ya kuyarudia hapa.

Ndani ya chama na kwa taifa, ninayo heshima kubwa mno kwa viongozi wetu hawa. Ninajua na kutambua mchango mkubwa wa Kanali mstaafu, Abdulrahman Kinana na sijasahau utumishi mzuri wa Luteni mstaafu, Yusuf Makamba katika kukiongoza chama chetu.

Hapohapo usinikumbushe juu ya ufanisi wa mbunge na waziri mstaafu, Bernard Membe. Wote hawa wana mchango mkubwa na uliotukuka kwa chama na taifa kwa ujumla, lakini ninalo neno kwao.

### NINALOWAKUMBUSHA

Ieleweke kuwa hapa siingilii mamlaka ya Kamati ya Maadili ya CCM ambayo ndiyo yenye jukumu la kulinda maadili yetu. Ninakumbusha tu machache niliyonayo husus kwa wanachama wenzangu na umma kwa ujumla.

> Kufanya mambo makubwa kwa maslahi ya chama pia ni kitu chenye afya na ustawi kwa jamii, lakini narudia tena kwamba, hiyo haimaanishi kuwa wewe ni mkubwa na muhimu kuliko wanachama wengine.

Kama mbunge, kuna wakati huwa najiuliza maswali mengi, tena nawaza, hivi bila hiki chama changu cha CCM, leo hii ningekuwa wapi katika utumishi wangu kwa wananchi? Nani angenijua Seif Khamis Said Gulamali? Nikifika hapo, ninajikumbusha heshima na utii mkubwa kwa CCM.

Hawa wazee wetu, ni muhimu na lazima sana tuwakumbushe kuwa hakuna aliye mkubwa kuliko chama. Tena hapa naomba nisisitize .Kujitoa kikamilifu katika kukitumikia chama na taifa ni jambo jema. Kufanya mambo makubwa kwa maslahi ya chama pia ni kitu chenye afya na ustawi kwa jamii, lakini narudia tena kwamba, hiyo haimaanishi kuwa wewe ni mkubwa na muhimu kuliko wanachama wengine. Hakuna.

(CCM inayo maadili na makuzi mengi yenye kujenga wananchama na wananchi katika taifa. Ndani ya chama tumefunzwa na kukuzwa kuheshimiana, kuthaminiana, kila mmoja kutambua mchango wa mwenzake na zaidi sana kuwa watiifu kwa chama.

Binafsi nimejengwa na chama nikiwa kijana mdogo mno. Huko nimejifunza mambo mengi ya kiuongozi, kisiasa na maisha kwa ujumla. Mafunzo niliyoyapata ndani ya CCM, yameniwezesha kuishi kwa amani katika jamii, kwani yanazingatia utu, nidhamu na maadili.

Sitaki kuingilia kamati ya maadili ya chama changu na siandiki haya kwa maana ya kujadili kinachoendelea kuhusu wazee wangu hawa, ninacholenga hapa ni kuwakumbusha viongozi wenzangu na Watanzania kwa ujumla kwamba hakuna mwanachama ndani ya CCM aliye mkubwa na nguvu au maarufu kushinda chama.

Unaweza kuwa na ushawishi mkubwa kuliko wenzako ndani ya chama, ukawa na nguvu kuliko wanachama wenzako, ukawa maarufu kuliko wanachama wenzako, lakini huwezi kuwa mkubwa, mwenye nguvu na maarufu kuliko Chama Cha Mapinduzi naomba hilo lieleweke.

Wito wangu kwa wananchama wenzangu na Watanzania kwa ujumla, Sauti kutoka Manonga inawakumbusha kuweka pembeni ushabiki wa aina yoyote juu ya jambo hili, kinachofanyika ni kuwekana sawa pale ambapo mwanachama au wanachama wenzetu wanapokuwa wataonekana wamekengeuka kidogo, hivyo ni vyema kuwarejesha katika mstari .

### KWA WASTAAFU

Jambo hili lisichukuliwe kwa ukubwa kama ambavyo naona baadhi ya watu wanalikuza kuliko hata lilivyo kiuhalisia. Mambo haya yapo duniani kote. Iwe kwa ngazi wa familia, ukoo, kijiji au chama chochote, kwamba mwanachama anarejeshwa kundini kwa kukumbushwa. Kinachotokea kwa viongozi wetu wastaafu ndiyo hicho cha kukumbushana na lengo kuu ni kuendelea kukijenga chama chetu.

Nimeona na kusikia ushabiki kutoka kwa baadhi ya wenzetu wa upinzani wakishangilia juu ya suala hili. Nimebaki nikicheka kwa kujikumbusha minyukano yao mingi tu ambayo bado ni mibichi kabisa. Lakini kwa kuwa siyo ajenda yangu, ngoja tuwaweke kando kwa leo.

Nimalize kwa kuwapongeza viongozi wetu wastaafu kwa kutii na kuitikia wito kwa kamati ya maadili inayoongozwa na Komredi Mangula, hakika mmeonyesha ukomavu wenu wa kiongozi na utumishi na pia ukongwe wenu ndani ya chama, lakini zaidi mmeonesha kwa vitendo mapenzi yenu kwa CCM.

Wanachama wenzangu tuendeleeni kushikamana katika kukijenga chama. Kujitolea kwa moyo wetu wote. Mambo haya nimeyakuta ndani ya chama na nikayaishi. Vilevile niliyasisitiza wakati nikiwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Mkoa wa Tabora na ninaendelea kuyahubiri hata leo.

Suala la kujitoa kwa ajili ya kujenga chama siyo rahisi, kuna gharama zake lakini kitu kizuri hujengwa kwa kuvuja jasho kwelikweli.

Waingereza wao husema; Nothing good comes easily. Wakimaanisha kwamba hakuna kilicho kizuri ambacho hutokea kwa wepesi.

Niwashukuru viongozi wetu wa ngazi za juu wakiongozwa na Mwenyekiti Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Magufuli, Makamu Mwenyekiti Bara, Komredi Mangula, Makamu Mwenyekiti, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, Katibu Mkuu, Dk. Bashiru Ally kwa kuendelea kutuongoza kwa njia bora zenye ustawi kwa chama na taifa kwa ujumla.

CCM ina watu makini ndiyo maana imeendelea kuwa madarakani kwa muda mrefu. Watanzania wanaelewa ufanisi na utendaji kazi wake. Kwa hiyo CCM haiwezi kuruhusu watu wachache waiyumbishe na kuitoa katika njia thabiti ya kuwatumikia Watanzania kwa kuunda serikali imara.

Uhai wa maisha ni kufanya kazi. Watanzania tuendeleeni kuchapa kazi kwa ustawi wa maisha yetu na ujenzi wa uchumi wa taifa letu.

***Mwandishi wa makala hii ni Seif Khamis Gulamali ambaye ni Mbunge wa jimbo la Manonga (CCM), wilayani Igunga mkoa wa Tabora.***

# ‘Safari ya matumaini’ tarajiwa ya kada Membe inaishia wapi?


Membe muda mfupi baada ya kuhojiwa na kamati ya maadili ya CCM jijini Dodoma hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO.**

**INATOKA UK.13**

Safari ya matumaini itaishia kujiunga na kina nani?

Maelezo ya Sekretariati ya CCM kuhusu ‘kupigwa kalamu’ uanachama wa kada Bernard Membe, yanakumbushia usemi wa Waziri Mkuu, wakati huo, Mizengo Pinda kuhusu wapinzani na maandamano ‘yasiyoisha.’ ‘Wapigwe tu, kwa sababu hakuna namna, wapigwe tu,’ kauli iliyovuma na kupeperushwa na’pepo za kusi’ hadi mabaraza kadhaa ya Haki za Binadamu huko ‘majuu.’

Ndivyo alivyoelekea kuyakinisha Humphrey Popepole, Katibu wa Itikadi na Uenezi, kuwa Membe ni mkosaji mzoefu, hivyo ‘hakuna namna, akatwe tu,’ kuwa kada huyo hakuyaanza leo.

Kama ilivyokuwa kwa Edward Lowassa, kada huyo mwandamizi pia alisisitiza kutumia chama tawala kama chombo cha kupeleka mbele matazamio yake ya kuendelea na ‘safari ya matumaini’ aliyoianza kabla ya mwaka 2015.

Ila wakati ule ilisikika zaidi safari ya Edward Lowassa, ndani ya ule msemo wa Kiswahili kuwa ‘avumaye baharini papa, lakini wengine wapo.’ Katika kipindi cha miaka minne sasa tangu awamu ya tano ianze, na wakati hakuna ‘dirisha’ kama hilo kwa CCM uchaguzi mkuu mwaka huu, hakuna aliyedhihirisha uthubutu kama Membe ndani ya CCM.

> Endapo kungekuwa na mazingira yoyote yale ya kuwa na mgombea wa pamoja, Membe angeweza kuwa chaguo rahisi kufikia ila hilo haliwezekani kwa sasa.

Ila hakuna mazingira ya Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), kama ilivyokuwa mwaka 2015 kwani kiwango cha maelewano katika vyama vya upinzani ni kidogo sana na haielekei kuwa suala la kuwepo mgombea wa pamoja linaweza hata kutajwa. Kwa maana hiyo matunda ya upinzani kwa ‘msimu’ huu yanatarajiwa kuwa haba, kwani watatumia nguvu kubwa kuparurana wakati makada wao waandamizi wengi tu walishahama na kuingia CCM, wakiwa wameshindwa kujizuia kueleza wanavyoridhishwa na kazi ya awamu ya tano.

Endapo kungekuwa na mazingira yoyote yale ya kuwa na mgombea wa pamoja, Membe angeweza kuwa chaguo rahisi kufikia ila hilo haliwezekani kwa sasa.

Ni hali hii ambayo inaweza kumpa taabu kidogo kada Membe akitafuta mahali pa kuendelea na ‘safari ya matumaini’ kama kada mwenzake alivyofanya uchaguzi uliopita na inavyoelekea hatakuwa na njia nyingine isipokuwa hiyo.

Sababu zake zitakuwa kama zile za kina Lowassa na Waziri Mkuu mstaafu Frederick Sumaye, kwamba kwa upande mmoja kuna matumaini ya aina fulani aliyonayo, na licha ya kuwa anaweza asiamini katika muujiza wa kushinda uchaguzi mkuu, si rahisi aone kuwa hakuna haja ya kushiriki uchaguzi.

Ni mantiki ya alichosema Sumaye, kuwa atakuwa na haja ya jukwaa la kuchangia maendeleo ya nchi na mustakabali wa uchumi na jamii, na hasa kwa kugombea. Ni wajibu ambao mtu anakuwa nao kwa nafsi yake mwenyewe, kuitii.

Kiongozi wa kihistoria wa Ufaransa Jenerali Charles de Gaulle (alifariki mwaka 1970) aliwahi kusema wakati fulani kuwa’wiki moja ni muda mrefu katika siasa,’ hivyo kutabiri au kuyakinisha kinachoweza kutokea hadi nchi ifikie katika uchaguzi mkuu ni ‘kumkosea adabu’ mhenga huyo.

Hakuna kinachoweza kuwa wazi katika wakati kama huu kwani vyama bado vinajitafuta wapiga kura kusema nini na kwa nia gani.

Ila kila chama kinawakilishwa na watu kadhaa wenye ushawishi katika vyama hivyo, na kimsingi wanachama na makada wa vyama hivyo wanasubiri tu ‘amri’ kutoka kwao; uchaguzi ni operesheni, kijeshi.

Katika chama cha Chadema, hisia inayotawala mahusiano ndani ya chama (unaweza kusema ndiyo hisia inayotangulia itikadi na uenezi kwa chama hicho) ni kuridhishwa na yaliyotokea baada ya kukubaliwa Lowassa kuwa mgombea wa urais kwa tiketi ya chama hicho.

Licha ya kuwa kila mtu ana hisia zake kwa suala hilo lakini baadhi ya mashabiki wa Lowassa wanaona kulikuwa na ‘intolerance,’ kukosekana uvumilivu wa utofauti wa mawazo na tamaduni tofauti za kisiasa. Lowassa alikuwa anataka kuwapo ‘mwavuli’wa kuwaleta CCM na Chadema pamoja katika masuala muhimu ya maendeleo, lakini akakwamishwa.

Kimsingi Chadema ilivyojengeka ndivyo ilivyo au itakavyokuwa hata katika uchaguzi mkuu unaokuja, kwani si rahisi kuona sauti ya kutoa ushauri tofauti kwa mwenyekiti wa taifa Freeman Mbowe, baada ya kuondoka kina Lowassa na huku mwanasheria Tundu Lissu ni makamu mwenyekiti.


James Mbatia Kushoto pamoja na Hamad, kwenye harakati za kisiasa.


Mtangaza nia wa mwaka 2015 Lowassa, muda mfupi baada ya kujiunga na Chadema. **PICHA: ZOTE MTANDAO.**

Na kwa njia hiyo pia kuna tatizo la msingi katika chama hicho nani atakuwa mgombea, kwani Mbowe bado ana kumbukumbu ya idadi ya kura alizopata uchaguzi mkuu 2005.

Anayeelekea kuziba pengo hilo ni Lissu, ila hana upana wa ufuasi nchini kama alivyokuwa katibu mkuu wa zamani Dk. Wilibrod Slaa, hivyo kurudia mafanikio yake si rahisi.

Kwa upande mwingine kuna ushawishi wa aina fulani hasa kutokana na eneo analotoka Membe na msingi wa kupata wapiga kura angalau kwa kufahamika kwake kama mbunge, kuwa ni eneo la kusini.

> Ila kila chama kinawakilishwa na watu kadhaa wenye ushawishi katika vyama hivyo.

Pengine Chama cha Wananchi CUF, ambacho sasa kimegawanyika katika kundi Mwenyekiti wa Taifa Profesa Ibrahim Lipumba na waliojiengua kwenda ACT-Wazalendo wakiongozwa na aliyekuwa katibu mkuu, Seif Shariff Hamad, kingeweza kuhusika.

Tatizo hapo ni kuwa kundi la Profesa Lipumba halina haiba inayoendana na Membe kwani anatakiwa kujiunga na ‘wapatanishi,’ kwa kiwango fulani, lakini kule ACT-Wazalendo haitakuwa rahisi kumwambia kiongozi mkuu Zitto Kabwe angoje muda mwingine. Membe akienda NCCR-Mageuzi atabadilisha ulinganisho wa nguvu upinzani, suala linalofanana na ‘jukwaa’ alilotaka Sumaye, ila ndoto itafifia.

## Netanyahu adai kushinda uchaguzi uliofanyika Israel


Benjamin Netanyahu. **PICHA: MTANDAO**

CHAMA cha Likud cha Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, kinaongoza katika uchaguzi wa bunge uliofanyika jana ikiwa ni wa tatu katika kipindi cha mwaka mmoja.

Hii inamaanisha kuwa Netanyahu anaelekea kushinda muhula wa tano madarakani licha ya kesi ya ufisadi inayomkabili, inayotarajiwa kuanza tena kusikilizwa Machi 17.

Tume ya Uchaguzi ya Israel imetangaza sehemu ya matokeo ya mwanzo yakionyesha chama tawala cha kihafidhina cha Netanyahu, Likud kimeshinda asilimia 28.72 ya karibu thuluthi moja ya kura zilizohesabiwa, dhidi ya asilimia 23.26 ya muungano wa siasa za wastani wa Blue and White wa mpinzani wake mkuu Benny Gantz. Tume hiyo ya uchaguzi inasema kucheleweshwa kwa shughuli ya kuhesabu kura kumetokana na idadi kubwa ya wapiga kura waliojitokeza wakifikia asilimia 71 ya walioandikishwa.

Netanyahu ameyaita matokeo ya uchaguzi huo kuwa “ushindi mkubwa” wakati akiwahutubia wafuasi wake mjini Tel Aviv hapo jana.

Matokeo ya uchunguzi wa maoni ya waliopiga kura yaliyochapishwa baada ya vituo vya kupigia kura kufungwa saa nne usiku yalionyesha chama cha Likud kikikadiriwa kuwa na uongozi wa pengo la viti vine hadi vitano dhidi ya Blue and White – ikiwa ni pengo kubwa zaidi kuliko utabiri wowote mwingine uliochapishwa kabla ya uchaguzi huo wa jana.

Kundi la Netanyahu la vyama vya siasa za mrengo wa kulia na kidini, hata hivyo kwa mujibu wa matokeo ya uchunguzi wa maoni ya waliopiga kura, kinashinda jumla ya viti 59 katika bunge la Knesset, ikiwa ni pungufu ya viti viwili ili kupata wingi wa viti unaohotajika kuunda serikali.

“Nilizungumza awali na viongozi wote wa vyama vya kundi la siasa za mrengo wa kulia, washirika wetu wa asili. Baada ya kupata usingizi kidogo, tutakutana tena ili kuanza kuunda haraka iwezekanavyo serikali yenye nguvu na thabiti, serikali nzuri ya kitaifa kwa ajili ya taifa la Israel.

Gantz anaelezea kusikitishwa kwake na matokeo hayo na kuwatuhumu wapinzani wa kisiasa kwa kusambaza uwongo dhidi yake. Anasema uchaguzi huo ndio uliokuwa na kampeni chafu zaidi katika historia ya Israel.

“Ninatambua na kuwa na hisia za maumivu na kukatishwa tamaa kwa sababu haya si matokeo ambayo labda tulitaka kuyaona na kama haya ndio matokeo yenyewe, basi sio matokeo ambayo yatairejesha Israel kwenye mkondo sahihi.”

Msaidizi Mkuu wa Rais wa Palestina Mahmoud Abbas, ameyashutumu mafanikio hayo yanayotabiriwa ya Netanyahu, akisema kuwa unyakuzi wa maeneo ya Ukingo wa Magharibi unaokaliwa umepata ushindi.

Katibu Mkuu wa Chama cha Ukombozi wa Palestina – PLO, Saeb Erakat, akisema katika taarifa kuwa Netanyahu ameamua kuwa muendelezo wa kuikalia ardhi ya Wapalestina na mzozo ndicho kinacholeta maendeleo na ustawi nchini Israel, na kwa hiyo amechagua kuimarisha misingi na nguzo za mgogoro huo na mzunguko wa machafuko, itikadi kali, vurugu na umwagaji damu.

Hatua inayofuata ni unyakuzi, anasema Erakat. **DW**

# Kifuatacho baada ya BVR kiwe mafunzo elimu uraia



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akifuatilia usajili wa wapiga kura kwa kutumia teknolojia ya bayometriki- BVR: **PICHA: MTANDAO.**

**Sabato Kasika**

MWEZI huu ndiyo unakamilisha kazi ya kuboresha Daftari la Kudumu la Wapigakura linalotumia utaratibu wa kibayometriki (BVR), iliyozinduliwa rasmi na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Julai mwaka jana mkoani Kilimanjaro.

Lengo la uboreshaji huo ni kutaka wale waliotimiza umri wa miaka 18 wapate haki ya kushiriki katika uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani, ambao unatarajia kufanyika Oktoba mwaka huu.

Wakati uboreshaji ukiendelea, kuna kitu ambacho Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec) inasema imekigundua kwenye uboreshaji huo, ambacho ni watu wengi kupoteza vitambulisho na kuwataka kuwa makini katika hilo.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji Semistocles Kaijege ndiye anayesema hayo katika moja ya hotuba zake na kusisitiza umuhimu wa Watanzania kutunza vitambulisho hivyo.

Bila kuwa na vitambulisho hivyo, ambavyo baadhi ya wanasiasa wanaviita kwa jina la 'kichinjio', mtu hawezi kuwa na haki ya kupiga kura, hivyo umakini ndiyo unaotakiwa katika utunzaji huo.

> Umefika wakati sasa Watanzania kuzingatia kile ambacho kimeelekezwa na Nec , kwamba wanaojiandikisha watunze vitambulisho hivyo baada ya kugundulika kuwa wengi wamevipoteza.

**UMUHIMU WA KADI**

Wananchi wanatakiwa kutunza vitambulisho hivyo vya kupigia kura, kwa sababu ndivyo vinawapa haki ya kushiriki katika uchaguzi, vinginevyo hawawezi kuruhusiwa kuchagua viongozi.

Hata hivyo, wapo ambao hupoteza vitambulisho hivyo, kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo hata kutokuwa makini katika utunzaji na hivyo kujikuta hawana na kulazimika kujiandikisha upya.

Umefika wakati sasa Watanzania kuzingatia kile ambacho kimeelekezwa na Nec , kwamba wanaojiandikisha watunze vitambulisho hivyo baada ya kugundulika kuwa wengi wamevipoteza.

Kwa wale ambao wamehama au kufariki dunia, suala la kuboresha au kubadili taarifa zao hakuna shida, vilevile uwezekano wa kupoteza upo, lakini umakini katika utunzaji unatakiwa kuwapo.

Hii itasaidia mtu kutopoteza muda kwenda kituoni kujiandikisha upya, na badala yake ataendelea na shughuli zake kama kawaida, kwa sababu atakuwa ametunza vizuri kitambulisho chake.

**ELIMU YA URAIA**

Katika kufanikisha uchaguzi, ni muhimu pia wananchi kuwa na elimu ya uraia ambayo ni mafunzo yanayowapa stadi na ufahamu, maadili, maarifa na mwelekeo unaowawezesha kushiriki kikamilifu katika masuala ya umma na kuwatayarisha kwa majukumu ya kijamii.

Elimu hii pia inawapa wapigakura maarifa na ufahamu kuhusu masuala ya demokrasia, utawala bora na mchakato wa uchaguzi, hasa katika demokrasia ya vyama vingi, ambapo kunakuwa na ushindani mkubwa wa kisiasa.

Kimsingi elimu ya uraia huwapa wananchi stadi na kuwahamasisha kushiriki kikamilifu, katika uchaguzi na kuhakiki rasilimali za umma, kwani haki ya kupata elimu ya uraia na kupiga kura ni haki ya mwananchi kikatiba.

Kwa kuzingatia hilo, uboreshaji wa daftari hilo unakwenda sambamba na utoaji wa elimu hiyo, ambayo inatolewa na baadhi ya asasi za kiraia zilizopewa jukumu hilo na tume ya uchaguzi.

Kutoa elimu ya uraia kwa wapigakura ni utaratibu mzuri, na utasaidia wananchi kulielewa suala zima la uchaguzi na jinsi ya kutunza vitambulisho ambavyo watavitumia katika uchaguzi.

Elimu hii siyo kwa wananchi wa kawaida tu bali hata viongozi wa vyama vya siasa wanatakiwa waipate kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu ili wawasaidie wanachama na wafuasi wa vyama vyao.

Viongozi wa vyama vya siasa ni wadau wakubwa wa uchaguzi, ndiyo wanatakiwa kupata elimu ya uraia na kuwasaidia watu wao, na hatua hiyo pia inaweza kuwa na mchango mkubwa katika utunzaji wa vitambulisho.

Hii inatokana na ukweli kwamba wapigakura wanatakiwa kuandaliwa vyema katika mambo yote ya msingi yanayohusu uchaguzi na wajue maana ya uchaguzi na umuhimu wake na haki zao zao kama raia katika uchaguzi.

Kimsingi, wananchi wanatakiwa kujua taratibu zote za uchaguzi na kile kinachotakiwa kufanywa wakati wote wa uchaguzi, hivyo elimu ya uraia ina umuhimu wake katika kufanikisha uchaguzi.

**ANGALIZO**

Waswahili wanasema kuwa, penye wengi hapakosi neno, kwamba inawezekana katika utoaji wa elimu ya uraia kukawa na mchezo ambao unaweza kuharibu lengo la utoaji wa elimu hiyo.

Kutokana na hilo, asasi za kiraia ambazo zimepewa jukumu la kutoa elimu ya uraia, zinapewa angalizo kwamba, zijiepushe na ushabiki wa kisiasa na kuzingatia mwongozo wa elimu hiyo uliotolewa na Nec.

Kwamba, wananchi wakipata elimu kuhusu uboreshaji huo watahamasika kutumia haki yao ya kikatiba ya kujiandikisha katika daftari hilo na hatimaye kushiriki kwa wengi kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Angalizo hilo ni la Waziri Mkuu, wakati akizindua uboreshaji wa daftari hilo, kwa ajili ya kuhakikisha kila kitu kinakwenda sawa na kila Mtanzania anatumia haki yake ya kikatiba ya kuchagua kiongozi anayemtaka.

Ni wazi kwamba, asasi kujikita katika ushabiki wa kisiasa ni sawa na kuwachanganya wapigakura, hivyo elimu itolewe, ili mwisho watu waamue wenyewe ni nani wanamtaka awaongoze kuliko kushawishiwa.

# Sudan inavyoonja shubiri ya wafadhili ikijikwamua

Na Mashaka Mgeta

SUDAN imefikia hatua ya kushtukiza kwa kufungua milango yake kwa Israel, ikitangaza fidia kwa meli ya kivita ya Marekani iliyolipuliwa miaka 20 iliyopita na imeahidi kushirikiana kwa asilimia 100 na Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai (ICC) iliyopo Hague nchini Uholanzi.

Ushirikiano huo na ICC 'inayokimbiwa' na baadhi ya nchi hasa za barani Afrika, unahusiana na masuala yanalenga makosa dhidi ya ubinadamu yaliyotokea kwenye jimbo la Darfur nchini humo.

Jitihada zote hizo zinatajwa kuwa ni sehemu ya kujenga upya uhusiano na ushirikiano kati ya taifa hilo masikini katika bara la Afrika na nchi za Magharibi, baada ya kutengwa na jumuiya ya kimataifa kwa miongo kadhaa iliyopita.

Kwa kufungua milango hiyo, Sudan itakuwa imejiwekea mazingira bora ya kupokea misaada hasa ya kifedha ili kuboresha uchumi wake.

Lakini hatua hizo zilizofanyika miezi kadhaa iliyopita hazijafikia kiwango cha vigezo.

Jumuiya ya kimataifa imeweka wazi kwamba kunahitajika uwazi zaidi kwa umma kuhusu matumizi ya fedha katika taifa hilo lililo katika kipindi cha mpito baada ya kupinduliwa kwa utawala wa Omar al-Bashir.

Pia jumuiya hiyo inaitaka Sudan kuwa mpango wa mageuzi ya uchumi na kupandisha ruzuku ya mafuta inayokadiriwa kugharimu takribani dola bilioni 3.5 kwa mwaka.

Hatari iliyopo, wanasema baadhi ya raia wananchi hiyo, ni kwamba uchumi wa taifa hilo unaweza kuporomoka endapo hapatakuwa na msaada wa kutosha, hivyo kuchochea vurugu za kisiasa zinazoweza kuhatarisha matarajio mapya katika kipindi cha demokrasia nchini humo.

Wahisani maarufu kutoka nchi za Magharibi na zile za Guba, wameshakutana mara kadhaa, lakini wakaahirisha mazungumzo yao kuanzia Aprili hadi Juni mwaka jana.

Marekani imeeleza kwamba Sudan inaweza kuondolewa kwenye orodha ya nchi zinaaminika kufadhili ugaidi, lakini haikusema ni hadi kufikia muda gani hatua hiyo itatangazwa.

Hatua ya Sudan kwenye orodha ya nchi hizo inaweka ugumu wa mazungumzo kati ya yake na wafadhili kuhusu madeni kwa jumuiya ya kimataifa, kuachiwa kwa fedha kutoka kwa wakopeshaji wa kimataifa na kuiunganisha nchi hiyo kwenye mtandao wa kimataifa wa benki duniani.

Serikali ya Sudan inayotambuliwa kuwa ya kikiritimba, ikiundwa kwa mfumo wa makundi mawili ya kushirikishana madaraka kati ya wanajeshi na raia hadi ifikapo mwaka 2022, inakabiliwa na mgogoro wa kiuchumi uliokuwa zaidi baada ya kuondolewa madarakani kwa al Bashir Aprili mwaka jana.

"Tuna mawazo kuhusu uchumi lakini ni namna gani tutayatekeleza. Lakini nadharia zote hizo zinategemea aina fulani ya msaada kutoka mataifa ya nje," Waziri wa Habari wa Sudan, Faisal Salih, ameliambia shirika la utangazaji la Reuters na kuongeza, "kwa hakika tunahitaji msaada wa nguvu."



Waziri Mkuu wa Sudan Abdalla Hamdok, anayepambana na changamoto za kujikwamua kiuchumi. **PICHA: MTANDAO**

> Unaweza kuwa na kipindi cha mpito cha utawala wa kiraia na demokrasia, au utakuwa unaelekea kwenye hali ya uchumi uliodorora na hali ya kushindwa.

Waziri wa Fedha anasema katika kipindi cha Novemba mwaka jana kuwa, serikali hiyo inahitaji kiasi kinachofikia Dola za Marekani bilioni 5 Shilingi $5 bilioni (Sh504.3 bilion) kulinusuru taifa hilo dhidi ya mdororo wa kiuchumi.

Tangu wakati huo, viongozi wa serikali wamekuwa wakihangaika kukabili uhaba mkubwa wa mafuta na mikate uliohusishwa na uhaba wa dola na kuingizwa kwa bidhaa zilizopewa ruzuku, licha ya msaada kutoka Ghuba.

Mfumko wa bei unaokuwa kwa zaidi ya asilimia 60; ambao ni mkubwa duniani, umesababisha matumizi ya mamlaka ya utawala kwa zaidi ya milioni tisa katikati ya jumla ya watu milioni 43 wanaohitaji msaada wa kibidamu huku kiwango cha lishe duni kwa watoto kikiongezeka.

Mawaziri wanasema wamefikia hatua nzuri katika mchakato wa amani unaolenga kuponya migogoro ya muda mrefu ya wenyewe kwa wenyewe, lakini changamoto za kudorora kwa uchumi zimekuwa kubwa kuliko ilivyotarajiwa.

Ingawa serikali inafurahia kuungwa mkono na raia mitaani, wanadiplomasia na wachambuzi wanasema imezidiwa na hofu kwamba huenda raia wakafikia ukomo wa uvumilivu kwa matatizo ya kiuchumi yanayolikabili taifa hilo.

"Sidhani kama kuna mwamko wa kimkakati kwamba wakati huu katika historia ni muhimu sana kwa Sudan," anasema Suliman Baldo, Mshauri Mwandamizi wa Sera wa kikundi cha utafiti na ushawishi cha Enough Project chenye makao makuu yake Washington, Marekani.

"Unaweza kuwa na kipindi cha mpito cha utawala wa kiraia na demokrasia, au utakuwa unaelekea kwenye hali ya uchumi uliodorora na hali ya kushindwa," anasema.

Anaongeza kuwa Serikali ya Sudan inakabiliwa na upinzani wa ndani kuhusu mageuzi ya kiuchumi.

Mawaziri wamejiondoa kutoka kwa hatua zozote kuu juu ya ruzuku hadi baada ya mkutano wa kiuchumi mwishoni mwa mwezi huu na kikundi kilichoratibu harakati za kisiasa, kuchochea ghasia na kujadili mpango wa kugawana madaraka (FFC).

"Kama hawatafanya kitu fulani katika ongezeko la ruzuku, hawawezi kupata msaada wa fedha, kirahisi tu hivyo," anasema mmoja wa wanadiplomasia wa nchi za Magharibi.

Mikondo ya mrengo wa kushoto wa kushawishi na FCC wanakosoa kwa kusema msaada wa nje hauhitajiki, badala yake wanapendekeza kujielekeza katika fedha za ndani zilizopotea kupitia rushwa na aina nyingine za ufisadi na kubadili umiliki wa vifaa vya usalama vya Sudani chini ya utawala wa al-Bashir.

Hatua kadhaa zimeshachukuliwa kupoteza nguvu za mtandao wa Imani kali ya kiislamy wa al-Bashir kwenye wizara za serikali na idara ya huduma za intelijensia.

Lakini upande wa jeshi umekitumia kipindi cha mpito kuongeza mamlaka zake, kwa mujibu wa Kiongozi wa FFC, Sadiq Farouk.

***Makala haya yamendikwa kwa msaada wa vyanzo vya mtandaoni na zaidi kutafsiriwa kutoka kwenye gazeti la The Standard la Kenya.***

# Jambo la 50/50 Uchaguzi 2020



Spika mstaafu, Anne Makinda akihamasisha wanawake kupigania 50/50. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

"WANAWAKE wenye nia ya kuwa viongozi wa kisiasa kwenye uchaguzi wa mwaka huu ni lazima waache woga na kujitokeza kushiriki katika mchakato huo bila kujali lugha chafu zitakazotolewa ili wafikie lengo la kuleta usawa wa kijinsia kwenye nafasi za uongozi. Hiyo ndiyo 50/50"

Ni neno la kuhamasisha kutoka kwa Spika mstaafu, Anne Makinda anayewataka wanawake kujituma na kuacha woga vinginevyo, Tanzania itaendelea kuota ndoto kwenye suala la taifa kutimiza lengo la kuwa na usawa wa kijinsia.

"Msijali lugha chafu zitakazokuwapo kwa kuwa haja yenu ni kuwa wabunge na madiwani ili kuwatumikia Watanzania. Nawahakikishia hakuna mwanamke makini atakayeshindwa kwenye uchaguzi hebu angalieni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Jenista Mhagama, mbunge wa jimbo Peramiho, alimuondoa mtu mwenye fedha zake.|" anaongeza.

"Kuna wanawake wengi wabunge wa majimbo wamefanyakazi nzuri hata mimi nilifanya kazi nzuri nilipofika miaka 40 nikaona niache nisiwe kikwazo kwa wengine ,"anasema wakati akizungumza kwenye maadhimisho na kongamano la kitaifa la siku ya wanawake, lililofanyika Dodoma.

Anabainisha kuwa kinamama wasipofanya hivyo Tanzania itaendelea kuota ndoto kwenye suala la usawa wa wanawake kushiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi kutokana na kuwa na woga wa kugombea.

"Kipindi cha uongozi wa kina Kawawa wanawake walikuwa wanapigana vita vya kisiasa kwa upendo .Sasa hivi kuna ubinafsi mwingi na mkifanya ubinafsi hatuwezi, hata asasi za kiraia utakuta kila asasi ina agenda tofauti na mwenzake sasa vita inapiganajwe wakati tumegawanyika,"anasema Makinda.

> "Tusikatishwe tamaa na maneno yakuturudisha nyuma maana mwanamke ukiwa kiongozi utaambiwa umelala na wanaume wote, pambana na hayo maneno yapo kwa kuwa hawataki kuona wanawake wameshika nafasi za uongozi.

Hata hivyo, anasema pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali bado kuna tatizo la mtazamo hasi kwa baadhi ya jamii kuhusu usawa wa jinsia, kuendelea kuwepo kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia,mila na desturi zenye kuleta madhara ya upungufu wa rasilimali za kutekeleza mipango kufikia 2025.

Makinda anasema suala la haki ya wanawake kushiriki kwenye siasa kama wapiga kura au wagombea wa nafasi mbalimbali jitihada zinaonekana ingawa kwa kusuasua kwa kiwango kikubwa.

Anasema hadi sasa kwa ngazi ya ubunge tangu mfumo wa chama kimoja kama isingekuwa kipengele cha viti maalum, Bunge lingekuwa na wastani wa wabunge wanawake asilimia kati ya sita na saba tu.

"Mimi nasema miaka 25 ya Beijing hatujafanya vizuri, wanawake ondoeni woga, acheni kukimbia kivuli chenu, hata kabla ya kwenda unaanza kuwaza utakavyoshindwa na hata bado kujaza fomu unawaza kushindwa, ni mapambano matusi utakuwa nayo, dharau kutukanwa. Lakini wewe shida yako ni nini si kuwa mbunge tu, kuwa diwani acheni woga,"anasema Makinda.

Kiongozi huyo anaongeza, "nafahamu kuna wakati mwingine vyama vyetu vya siasa ni kipingamizi, lakini hata sisi wenyewe ni kipingamizi hasa wanapotokea wanawake wawili wapo jimbo moja kutakuwa ni ugomvi tu wanaume wanasema waache waendelee kugombana wote wanakosa nafasi tumepoteza wenyewe."

Anawataka kujiandaa kwa ajili ya uchaguzi mkuu ili kufikia usawa huo na kuungana ili kupata ushindi kwenye majimbo.

### ILANI ZIWE 50/50

Ikumbukwe kuwa kila mwaka Machi 8, duniani inaadhimishwa siku ya wanawake ndiyo ,maana Umoja wa Mataifa (UN), ukaamua kuwapo na siku hiyo kutokana na ukweli kwamba masuala ya haki, afya na maendeleo ya wanawake yalihitaji msukumo wa kipekee.

Usawa wa kijinsia katika nafasi za kisiasa, uteuzi na utumishi kwenye maeneo mengine, ni mambo yanayowafanya wanawake kupaza sauti kupinga kuminywa kwa wanaopata nafasi hizo licha ya kuwa na sifa za uongozi na za kitaaluma.

Tumaini la kuwapo kwa usawa wa kijinsia katika nafasi za kisiasa lilionekana baada ya idadi ya wanawake waliojitokeza kuwania nafasi za ubunge katika majimbo kuongezeka tofauti na uchaguzi zuliopita.

Oktoba mwaka huu, inatarajiwa kufanyika uchaguzi mkuu, tayari wanawake wameanza kuhamasishana ili kufikia asilimia 50 kwa 50 ya usawa wa kijinsia kwenye nafasi mbalimbali za uongozi.

Akizindua Mtandao waViongozi Wanawake wa Afrika Tawi la Tanzania (AWLN Tanzania) unaoratibiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalojihusika na usawa wa jinsia na uwezeshaji mwanamke (UN Women), Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, anasema katika mchakato wa uchaguzi huo wanawake wahakikishe agenda ya 50 kwa 50 inaingizwa kwenye ilani za vyama vya siasa.

Anasema wanawake waingize agenda hiyo kwenye ilani za vyama vya siasa ambazo zitatumika kwenye uchaguzi huo.

"Ngoja niwaibie siri, hivi sasa vyama vya siasa vipo katika mchakato wa kutengeneza ilani za uchaguzi ni vyema wanawake tukasimama kidete katika kuhakikisha vinaingiza agenda ya 50 kwa 50 katika ilani zao na hata kama si kwenye maeneo yote basi baadhi ya maeneo 50 kwa 50 ionekane," anasema.

Pia, Makamu huyo anawataka wanawake kujitokeza kwa wingi na kushiriki kikamilifu katika kugombea nafasi za uongozi katika nyanja mbalimbali ikiwamo siasa, biashara, huduma za umma au asasi za kiraia.

Aidha, anasema nchi nyingi duniani bado usawa wa kijinsia haujafikiwa katika nyanja nyingi ikiwamo uongozi.

"Hali hii inaigusa nchi yetu ya Tanzania, ingawa kwa kiasi kikubwa tunafanya vizuri tukilinganishwa na nchi nyingine barani Afrika, tuna wabunge wanawake 126 kati ya 393 sawa na asilimia 36.7 huku baraza la wawakilishi Zanzibar ni asilimia 38, kiwango hichi ni juu ya uwiano uliowekwa na nchi za SADC cha angalau asilimia 30,"anasema.

Hata hivyo, anasema kwa upande wa mahakama idadi ya majaji wanawake wa Mahakama Kuu ni asilimia 30, Rufani ni asilimia 38, Baraza la Mawaziri wanawake ni asilimia 18, wakati Naibu Mawaziri ni asilimia33.

"Kwa mara ya kwanza nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshikwa na mwanamke.

Kwa takwimu hizo bado taifa halijaweza kufikia usawa wa kijinsia kwa kiwango kikubwa sana,"anasema.

Kadhalika, anasema utafiti unaonyesha kwamba ongezeko la idadi yaviongozi wanawake wa kisiasa limesababisha kuboreshwa kwa sera, sheria pamoja na bajeti.

"Kadhalika, imebainika kuwa uwepo wa wanawake zaidi katika usimamizi wa mashirika katika sekta binafsi umethibitika kusaidia kukuza faida za biashara kutokana na ujuzi, ufanisi, uaminifu na ustadi wa kipekee,"anasema.

### WANAUME MABALOZI

Kwa upande wake, Waziri wa Afya, Maendeleoya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anawataka wanawake na wanaume kuwa mabalozi wa kubadili mitazamo waliyonayo na badala yake washirikiane kwa lengo la kuleta usawa wa kijinsia.

"Tusikatishwe tamaa na maneno yakuturudisha nyuma maana mwanamke ukiwa kiongozi utaambiwa umelala na wanaume wote, pambana na hayo maneno yapo kwa kuwa hawataki kuona wanawake wameshika nafasi za uongozi,"anasema.

### WOSIA WA MONGELLA

Rais wa kwanza wa Bunge la Umoja wa Afrika, Dk. Getrude Mongella, anasema wanawake wapambane kuingia bungeni huku akisema ni hasara kuwa na wanawake viongozi bungeni ambao wanaona aibu na kigugumizi kuzungumzia masuala ya wanawake.

"Ninapotaka kuangalia lile bunge siku itafikia idadi ya 50 kwa 50 sitajali wewe umetokea chama gani isipokuwa nitajali kama wewe kweli mambo tunayozungumza hapa unayajua na kuyapenda,"anasema Mongela..

Anaongeza "Kama mtu anaingia bungeni kama anakwenda kwenye maonyesho heri nimpigie mwanaume, ni hasara kama tutakuwa na viongozi wanaoona aibu au kigugumizi kuzungumza maendeleo ya wanawake."

### UMUHIMU KUSAIDIANA

Kadhalika, mbunge wa zamani, Anna Abdallah, anasema kina mama watakaojitokeza wasaidiwe na wanawake waliopo kwenye nyanja mbalimbali za uongozi kama wao hawataki kugombea tena.



## H/shauri lawamani ukaidi mwongozo

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

HALMASHAURI nyingi nchini zinadaiwa kuwa hazitekelezi mwongozo wa serikali unaozitaka kurejesha asilimia 20 ya mapato yatokanayo na ushuru wa mazao na asilimia 15 ya mapato yanayotokana na ushuru wa mifugo kwa ajili ya kuendeleza sekta hizo.

Hayo yalisemwa juzi jijini Mbeya na viongozi wa mtandao wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali wakati wa mkutano wa wadau wa kilimo na ufugaji wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wakiwamo viongozi wa serikali.

Katibu wa Mtandao wa Mashirika hayo Mkoa wa Mbeya, Paul Kitta, alisema kitendo hicho kinazifanya sekta hizo kudumaa, hivyo akaiomba serikali kufuatilia na kuzilazimisha halmashauri zote nchini kurejesha fedha hizo.

Alisema miongozo hiyo inaeleza vizuri na imewekwa kwa mujibu wa sheria lakini usimamizi wake ndio mbovu, hali ambayo inazifanya halmashauri kufanya mambo kwa kujiamlia.

"Lengo la miongozo hiyo ilikuwa ni kuziendeleza sekta hizi, sasa tumefanya utafiti kwa nchi nzima ni halmashauri chache sana ambazo zinarejesha fedha hizo japo kidogo, sasa ni vizuri serikali iingilie kati kwa kuzilazimisha halmashauri zote," alisema Kitta.

Alisema sekta hizo zinachangia asilimia kubwa ya mapato ya halmashauri, hivyo zinatakiwa kusimamiwa vizuri ili ziwe endelevu na wananchi walipe mapato kwa moyo.

Akizungumza kwa niaba ya watendaji wa halmashauri nchini, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Iringa, Jeremiah Mkobo, alikiri halmashauri kutorejesha fedha hizo huku akidai kuwa sababu huwa ni ufinyu wa bajeti.

Alisema wakati mwingine halmashauri zinakusanya fedha kidogo kuliko makisio ya bajeti zao, hivyo kujikuta baadhi ya vipaumbele havitekelezwi.

"Ni kweli hizo asilimia zipo kisheria, lakini huwa havitekelezeki kwa sababu mbalimbali ikiwamo viwango vya makusanyo ya halmashauri pamoja, vipaumbele vyake pamoja na ufuatiliaji wa wahusika wanaotakiwa kunufaika na fedha hizo," alisema Mkobo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, alisema wakulima na wafugaji wanazalisha chakula kwa ajili ya Watanzania wote hivyo ni lazima watazamwe kwa jicho la pekee.

# 11 wanaswa tuhuma wizi mtandaoni

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

VIJANA 11 wenye umri kati ya miaka 20 na 25 wakiwamo mawakala wawili wa kusajili laini za simu, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa tuhuma za kuwatapeli wananchi kwa kutumia majina ya viongozi wa serikali na wasanii maarufu nchini.

Aidha, vijana hao wanadaiwa kuwa walikuwa wanatumia laini za simu ambazo zimesajiliwa kwa kutumia vitambulisho vya watu wengine, kuwatapeli wananchi kwa kuwatumia jumbe fupi za simu zinazosema 'ile pesa itume kwenye namba hii'.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Kituo Kikuu cha Polisi cha Mkoa wa Mbeya, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema vijana hao walifungua akaunti kwenye mtandao wa Facebook zenye majina ya viongozi hao pamoja na wasanii zikielezea malengo mbalimbali.

Aliwataja baadhi ya viongozi na wasanii ambao majina yao yalikuwa yanatumiwa na vijana hao ni Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, Jokate Mwegelo, Wema Sepetu, Jackline Wolper, Aunt Ezekiel na Kajala Masanja

Alisema kurasa zilizokuwa zimefunguliwa na vijana hao zilikuwa zinaonyesha kuwa viongozi na wasanii hao wanatoa mikopo yenye riba nafuu, kusaidia vijana kupata ajira, kuwainua wasanii wachanga na fursa zingine.

Alisema kwenye kurasa hizo waliweka namba za simu ambazo zimesajiliwa kwa kutumia majina na vitambulisho tofauti wakiwaelekeza wananchi kutuma fedha kwa ajili ya fomu na usajili pamoja na kuelekeza wananchi wawasiliane nao kupitia kurasa za Facebook.

"Fedha walizokuwa wanataka watumiwe na wananchi ni kati ya Sh. 20,000 na Sh. 30,000 ambazo wananchi wengi sana walikuwa wanawatumia na tulipopokea malalamiko mengi, tulishirikiana na kitengo cha upelelezi kutoka makao makuu na tukawanasa vijana hao," alisema Kamanda Matei. Aliwataja wanaoshikiliwa ni Alfred Kidunga, George Engeja, Eliud Mahenge, Philipo Alananga, Gasto Sanga, John Michael, Emily Kaleba, Daud Sanga, Junior Kawanga, Kasto Tweve na Alfa Kayoka ambao wote ni wakazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Alisema walikamatwa kati ya Februari 21 na 22 mwaka huu, na kwamba laini za simu walizokuwa wanazitumia kutuma jumbe za kuwatapeli wananchi, walikuwa wanauziwa na mawakala wa kusajili laini kwa gharama ya kati ya Sh. 1,000 na 1,500.

Kamanda Matei alisema baada ya kuwahoji walikiri kuhusika na matukio mbalimbali ya utapeli na kwamba mawakala waliokuwa wanasajili laini za simu walikutwa na fedha zaidi ya 600,000 ambazo walikuwa wamekusanya kutokana na biashara hiyo.

Aliwataka wananchi waliokumbwa na utapeli huo kwenda katika Kituo cha Polisi kutoa maelezo ili wasaidiwe.

Mpelelezi wa Makosa ya Mtandao Mkoa wa Mbeya, Ally Challu, alisema kutokana na vijana hao kutumia akaunti za viongozi na wasanii wa kike, walikuwa wanaziweka simu zao kwenye mifumo ya sauti za kike ili wanapopigiwa na wateja waonekane kweli ni wa kike.

Alisma mawakala waliokuwa wanawasajilia laini za simu, walikuwa wanatumia vitambulisho vya watu wengine wanaoenda kusajili laini zao kwa kuwadanganya kuwa mtandao unasumbua na hivyo kuwalazimisha wabonyeze vidole zaidi ya mara moja.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kulia), akibadilishana mawazo na watoto kwenye tangi la maji la kitalu nyumba cha Iganjo, kinachomilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Mbeya wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa ya kukagua miradi ya maendeleo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wazalishaji Nyanda Juu Kusini wafundwa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAKULIMA na wazalishaji mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameshauriwa kuwa waaminifu na kuzalisha mazao yenye ubora ili kuwa na uhakika wa bidhaa zao kupata soko la ndani na nje ya nchi.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito, wakati wa Mkutano wa Jukwaa la Wazalishaji Vijijini Tanzania (Juwavita) kutoka katika mikoa saba ya kanda hiyo.

Madito alisema baadhi ya wazalishaji nchini ambao sio waaminifu wamekuwa wakiharibu soko la mazao yao kwa kuchanganya mazao yao na vitu vingine ili kuongeza uzito wakati wa kuuza kutokana na tamaa ya kutaka kupata faida kubwa.

"Kahama ni miongoni mwa maeneo nchini ambayo yanazalisha mchele mzuri sana, lakini waliwahi kuharibu soko la mchele huo kwa kuchanganya na mchanga ili kuongeza uzito wakati wa kuuza, sasa wateja baada ya kugundua waliacha kununua japo kwa sasa waliacha kufanya hivyo," alisema Madito.

Aliwataka wazalishaji wa ukanda huo kuwa waaminifu hasa kipindi hiki ambacho nchi ina uhitaji mkubwa wa malighafi kwa ajili ya viwanda pamoja na soko la nje ili kufikia uchumi wa kati.

Madito aliwataka wananchi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuchangamkia fursa zilizopo hasa kwenye sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, pamoja na ufugaji wa nyuki kwa maelezo kuwa katika mikoa fursa hizo zipo nyingi.

Mkurugenzi wa Juwavita, Catherine Mlaga, alisema jukwaa hilo lina wanachama nchi nzima na kwamba lengo la kuundwa kwake ni kuwaunganisha wazalishaji, wadau pamoja na serikali ili kuwasaidia wazalishaji wadogo kupaza sauti zao kuhusu matatizo yanayowakabili kwenye uzalishaji.

Alisema jukaa hilo lilianzishwa na asasi za kiraia baada ya kufanya utafiti na kubaini kuwa wazalishaji hawana jukwaa la pamoja la kuwasaidia kuwasilisha malalamiko yao na badala yake kila wazalishaji walikuwa wana jukwaa lao.

"Kwa mikoa ya ukanda huu jukwaa hili linawahusu wakulima, wafugaji, wavuvi na walina asali lakini kitaifa lipo pia kundi la jamii ya wale watu wanaoishi kwa kula matunda na nyama, tumeanza katika hii kanda kwa kuwashirikisha wadau zaidi ya 70 na tutaendelea na Kanda zingine mpaka tufikishe watu 3,000," alisema Mlaga.





# Takukuru yaweka kambi shuleni, vyuo

**Na Renatha Msungu,DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imeweka kambi shuleni na vyuoni kwa ajili ya kuanza kutekeleza mkakati wa kupiga vita vitendo vya rushwa.

Akizungumza jana jijini hapa, Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Brigedia Jenerali John Mbungo, alisema lengo la kambi hizo ni kutoa elimu shuleni na vyuoni ya kupambana na rushwa.

Alisema katika mkakati wa kutumia vijana wa Skauti nchini una nafasi kubwa ya kuleta matokeo chanya katika jamii.

"Tutautumia vizuri mkakati huu maana tunahitaji vizazi vijavyo vijue nini maana ya rushwa, lengo ni kuona Tanzania inapingana na suala la rushwa katika maeneo yao ya kazi," alisema Brigedia Mbungo.

Alifafanua zaidi kuwa elimu kwa wananchi inahitajika hususan vyuoni na shuleni ambapo wao nao watakwenda kufundisha katika sehemu wanazotoka.

Alisema elimu hiyo pia itatolewa kwa viongozi kwa mikoa ambao nao watatumia nyadhifa zao kuwaelimisha jamii yao kupitia mamlaka wanazoziongoza.

Kwa upande wake, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema elimu kuhusiana na rushwa inapaswa kufundishwa tangu shule za msingi na sio vyuoni na sekondari pekee.

Prof. Ndalichako alisema wanahitaji kupata kizazi ambacho kinajiepusha na rushwa ili kuwa viongozi wazuri hapo baadae.

Alisema anawapongeza Skauti Tanzania na Takukuru kwa kushirikiana kubuni mkakati huo wa Taifa ambao utasaidia kukomesha rushwa.

"Nawapongeza sana Skauti na Takukuru hili suala mlilobuni ni zuri na liwe endelevu," alisema Prof. Ndalichako.

**"Tutautumia vizuri mkakati huu maana tunahitaji vizazi vijavyo vijue nini maana ya rushwa, lengo ni kuona Tanzania inapingana na suala la rushwa katika maeneo yao ya kazi," alisema Brigedia Mbungo.**

# Utafiti wabainisha faida mkojo wa paka

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imesema kwa mwaka 2019 jumla ya miradi ya utafiti 145 ufadhiliwa na baadhi umeshatoa matokeo chanya kwa jamii ikiwamo mkojo wa paka ambao unazuia panya waharibifu wa mazao.

Hayo yalielezwa juzi na Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Wizara hiyo, Prof. Maulilio Kipanyula, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mashindano ya kitaifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu (MAKISATU), kwa mwaka 2020, yatakayofanyika kuanzia Machi 16-20 jijini Dodoma.

Alisema utafiti wa mkojo huo ulifanywa katika Chuo Kikuu cha Sikoine cha Kilimo (SUA) na umesaidia kuondokana na panya hao kwa baadhi ya maeneo.

Hata hivyo, alisema kuna watu wamekuwa wakidai kuwa serikali haitoi fedha za utafiti, jambo ambalo si kweli kwa kuwa mwaka jana ilifadhili miradi 145 kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Sayansi na Teknolojia (MTUSATE).

"Huu mfuko hadi kufikia mwaka 2019 ulishapata Sh. bilioni 50.55, wanaosema serikali haitoi fedha za utafiti ushahidi huu hapa, miradi 145 ya utafiti imefadhiliwa kwa mwaka 2019 na matokeo baadhi yameshatoka," alisema.

Alitaja baadhi ya matokeo hayo ni pamoja na mkojo huo wa paka, chanjo ya kideri au mdondo wa kuku na mbegu mpya za mahindi, maharage, mpunga na viazi.

Vile vile, alisema mfuko huo umefadhili watafiti na wahadhiri 517 katika mafunzo ya shahada ya uzamili na uzamivu.

Kadhalika, alisema teknolojia zaidi ya 150 kati ya 230 zilizogunduliwa na wabunifu nchini, zinahitaji kuendelezwa ili zitumike.

"Tunalenga kuanzisha kanzi data ya Taifa ya teknolojia na ubunifu ili wabunifu wajulikane na bunifu zao ziwasaidie kujikwamua kiuchumi," alisema.

Prof. Kipanyula alisema kupitia ubunifu serikali inaamini itazalisha teknolojia na ajira kwa wananchi wake na kwa mwaka wa fedha 2018/19 kiasi cha Sh. bilioni 2.6 kilitolewa kuendeleza ubunifu na wagunduzi.

"Kwa mwaka huo vilianzishwa vituo vya ubunifu 17, pia tumesaidia wabunifu kulinda bunifu zao, si kila kitu kinatakiwa kusemwa ni siri yako mgunduzi," alisisitiza.

Kuhusu mashindano hayo, Mkurugenzi huyo alisema wamepata waombaji wengi zaidi ya mwaka jana na kuwataka waandishi wa habari kuhamasisha zaidi wabunifu kujitokeza ili kutambulika na jamii.

Alisema kwa mwaka huu wamepokea maombi 583 na kutakuwa na makundi saba ambapo kila kundi litatoa washindi watatu ambao mshindi wa kwanza atapata Sh. milioni tano, wa pili atapata Sh.Milioni tatu na mshindi wa tatu atapata Sh.Milioni mbili.




Mwokota chupa tupu za plastiki, akila mabaki ya vyakula vilivyotupwa kwenye chombo cha kuhifadhia takataka katika eneo la Barabara ya Mbeya, jijini Dodoma jana, kitendo ambacho ni hatari kwa afya yake. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Ulaji nyama Tanzania ni hafifu'

**Na Augusta Njoji, KONGWA**

IMEELEZWA kuwa ulaji wa mazao ya mifugo kwa Watanzania ni hafifu, ambapo kwa sasa mtu mzima anakula nyama kilo 15 kwa mwaka.

Kwa mujibu wa kiwango kilichowekwa na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), mtu mmoja anatakiwa kula kilo 50 za nyama kwa mwaka.

Hayo yalielezwa jana na Ofisa Mifugo Msaidizi Mwandamizi wa Idara ya Uzalishaji na Masoko kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Charles Lugamara, kwenye utoaji chanjo ya mifugo kwa wafugaji wanaozunguka Ranchi ya Kongwa.

Alisema ulaji wa nyama bado upo chini licha ya Tanzania kuwa na mifugo mingi zaidi ya milioni 32.

"Licha ya kuwa na mifugo mingi, tija ya mazao ya mifugo bado ni ndogo, ndio maana wizara ina mikakati mingi ya kuboresha sekta ya mifugo ili mazao yanayozalishwa yawe ni bora," alisema.

Alitaja miongoni mwa mikakati ambayo ipo mbioni kutekelezwa ni uzalishaji nyama kwa ajili ya soko la nje ambao unalenga kutatua kero zinazowakabili wazalishaji ili kuzalisha nyama bora kukidhi mahitaji ya ndani na nje.

"Nyama zetu kumekuwa na kikwazo cha kuuzika kwenye baadhi ya nchi kutokana na magonjwa, ndio maana idara hii kwa kushirikiana na idara zingine imeandaa mkakati wa kuuza nyama nje kwa ajili ya kuangalia namna ya kuondokana na tatizo la mazao ya mifugo kutokuwa bora," alisema.


Ofisa huyo alisema kupitia Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) wizara imejipanga wafugaji waliopewa vitalu watazingatia misingi ya uzalishaji kwa kuzalisha nyama itakayokidhi ubora na uchanjaji mifugo.

"Hadi jana ng'ombe 24,999 wamechanjwa, hizi ni jitihada nzuri kwa serikali kuhakikisha mifugo inayozalishwa inakuwa inatija na kukidhi ubora wa uzalishaji," alisema.

Naye, Kaimu Meneja Mkuu wa NARCO, Masele Mipawa, alisema Ranchi ya Kongwa ina ukubwa wa hekta 38,000 ambapo hekta 12,076.6 limetengwa vitalu kwa ajili ya wafugaji wanaozunguka ranchi hiyo.

Alisema katika kutekeleza mpango wa uthibiti wa magonjwa na kuwa eneo huru, ranchi hiyo ilianza kuchanja mifugo ya wananchi kulingana na kalenda ya chanjo.

"Tumeanza zoezi hili Februari 21, mwaka huu kwa ng'ombe ambapo wanapatiwa chanjo ya homa ya mapele ngozi, mapafu na magonjwa mengine tupo hatua za mwisho kukamilisha zoezi, na mwitikio ni mzuri," alisema.



# Shein ataka kasi Wizara ya Ujenzi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameutaka uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kuongeza kasi katika kuitumikia wizara hiyo kutokana na huduma inazozitoa kuwa muhimu kwa wananchi.

Alitoa agizo hilo Ikulu mjini Unguja alipokutana na uongozi wa wizara hiyo kupokea taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi kwa kipindi cha Julai hadi Desemba kwa mwaka huu wa fedha.

Dk. Shein aliutaka uongozi kuongeza kasi katika utendaji wake ili mafanikio zaidi yapatikane, ikizingatiwa wananchi wengi wanategemea huduma zake.

Alisema kuna haja uongozi wa wizara hiyo kuwawekea mazingira mazuri zaidi wafanyakazi wake ikiwamo kuwatunza na kuwapa stahiki zao hasa kwa wale wanaofanya kazi za barabara na baharini.

Rais Shein alisema wapo watu wasiokuwa na nia nzuri na wizara hiyo, hivyo ni vyema uongozi ukawaelewa na kutowaacha wakaendelea kuharibu na badala yake wawachukulie hatua za kisheria.

Aliutaka uongozi huo kukaa pamoja kwa taasisi za serikali wakati wa maandalizi ya miradi ili kuepuka athari zinazoweza kutokea baadaye.

Dk. Shein pia alizungumzia umuhimu wa kuwapo kwa Wakala wa Serikali wa Karakana Kuu ya Vyombo vya Moto Zanzibar itakayotoa huduma bora kutokana na uwapo wa wataalamu na vifaa vinavyokwenda na wakati uliopo.

Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Abdulhamid Yahya Mzee, aliupongeza uwasilishaji na utayarishaji wa taarifa hiyo na kusema kuwa wizara hiyo imekusanya mapato mengi.

Waziri wake, Sira Ubwa Mamboya, alisema kwa kipindi hicho, wizara ilifanikiwa kukamilisha sehemu ya ujenzi wa barabara mbalimbali Unguja na Pemba kwa kiwango cha lami ikiwamo Barabara ya Ole-Kengeja yenye urefu wa kilomita 35.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo unaendelea na kwa sasa jumla ya kilomita 22.5 zimeshawekwa lami na kazi ya usafishaji kwa barabara yote imekamilika.

Alisema ni matarajio ya wizara yake kuwa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume litakamilika katika muda uliopangwa hasa ikizingatiwa kuwa serikali imetenga fedha zake za ndani ili kukamilisha ujenzi huo.

Waziri Mamboya pia alisema wizara kupitia Shirika la Meli inaendelea kuzifanyia matengenezo meli zake ili ziendelee kutoa huduma.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na uongozi wa Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano, Ikulu mjini Zanzibar, juzi.
**PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# TIRA yabaini tatizo wakataji wa bima

**Na Rahma Suleiman, UNGUJA**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), imewataka wananchi kuacha utaratibu wa kununua vyombo vya usafiri ambavyo tayari vimekatiwa bima na waliokuwa wamiliki wa awali na badala yake wakate bima kwa majina yao ili kuwe na taarifa sahihi za umiliki wa vyombo hivyo.

Meneja Uendelezaji Soko la Bima Tanzania, Salum Yungwa, alitoa rai hiyo wakati wa mafunzo kwa wanahabari yaliyofanyika mjini Unguja.

Alisema kuvikatia bima vyombo vyao kutasaidia kuwapa umiliki halali wa vyombo hivyo na kuondokana na matatizo mbalimbali ambayo hujitokeza, yakiwamo majanga.

Alisema imezoeleka utaratibu wa kuuziana vyombo vya aina mbalimbali yakiwamo gari na kuendeleza matumizi ya bima zenye majina ya wamiliki wa awali, jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

Alisema endapo gari likipata ajali, anayemiliki hatakuwa na haki kutokana na jina lilokatiwa bima kuwa la mmiliki wa awali.

Aliwataka wananchi kutambua kuwa kuendelea kutumia bima ya zamani ya mmiliki wa aliyemuuzia gari, kutamkosesha kupata fidia endapo atapata ajali au majanga mengine.

"Kumekuwa na utaratibu wa kuuziana vyombo vya moto na kuendelea na matumizi kwa bima zenye majina ya wamiliki wa awali, hali inayomkosesha kupata fidia kwa mmiliki wa sasa endapo atapata ajali au majanga mengine," alionya.

Meneja huyo alisema lengo la bima ni kupunguza umaskini kwa jamii na kupunguza majanga kwa kuwalipa watu wanaopata majanga, yakiwamo ya moto.

Aliwataka wanahabari kusaidia katika kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa bima katika kukua kwa uchumi na kuimarisha uwekezaji nchini.

Meneja Mamlaka ya Bima Ofisi ya Zanzibar, Mohammed Khamis Ameir, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuhamasisha jamii kutambua umuhimu wa bima ili kuzitumia kwa kujikinga na majanga yanayoweza kutokea.

"Imani yangu ni kwamba, kupitia ninyi waandishi wa habari, jamii itapata uelewa juu ya umuhimu wa kukata bima, hivyo tunawaomba elimu hii mloipata, mkaitumie kwa wananchi," alisema.

# Wanawake wakoshwa mafanikio uvuvi pweza

**Na Mwandishi Wetu, UNGUJA**

WANAWAKE wa Kijiji cha Mtende, Mkoa wa Kusini Unguja, wamesema wamepata mafanikio makubwa baada ya kijiji hicho kupitia kamati yake ya uvuvi kuanzisha utaratibu wa Leeds katika uvuvi wa pweza.

Wamesema kuwa awali walikuwa wakipata kipato kidogo, lakini sasa wanapata kati ya Sh. 80,000 na 100,000 kwa msimu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mjumbe wa Kamati hiyo Hidaya Mohammed, alisema utaratibu huo umewasaidia wanawake kuongeza kipato chao.

"Zamani tulikuwa tunaenda pwani kuvua pweza, lakini kutokana na kuwa hakukuwa na utaratibu, tulikuwa tunapata mavuno madogo ambayo wakati mwingine hupata kitoweo tu, lakini sasa kwa utaratibu huu tunavua pweza ambao hata kama siyo sawa na wanaume, lakini tunapata mpaka laki na nusu (Sh. 150,000)," alitamba.

Hata hivyo, mjumbe huyo alisema bado kuna mwitikio mdogo wa wanawake katika kujiunga na kamati hiyo na kuwataka kujitokeza kujiunga ili kuongeza nguvu na ushirikiano katika shughuli mbalimbali za kijiji hicho.

Katibu wa Kamati ya Uvuvi ya Mtende inayojihusisha na ufugaji wa pweza, Abuu Faida Haji, alisema tangu kuanza kwa utaratibu huo ambao wameupata kupitia Mradi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (Swiofish), kumekuwa na mabadiliko makubwa katika uvuaji wa samaki hao.

Alisema awali kipato chao kilikuwa chini, lakini baada ya kuanzisha mfumo huo, wamevua pweza wenye thamani ya Sh. milioni moja na nusu, tofauti na awali.

Alisema kuwa fedha hizo hupatikana kila wanapovua pweza hao kwa kipindi cha siku tatu ambazo matumizi yake huenda asilimia 60 katika shughuli za kijamii za kijiji hicho na asilimia 40 kwa Kamati ya Uvuvi.

Alisema wanapofungulia, pweza huvuliwa kwa siku tatu na siku zilizobakia eneo hilo huwa huru mpaka pale wanapolifungia tena baada ya miezi miwili hadi mitatu.

Kwa mujibu wa kamati hiyo kijiji hicho kina wavuvi 250 na kwa kipindi cha miaka mitatu(2017 hadi 2019), Sh. milioni 6.625 zilipatikana kutokana na uvuvi wa pweza.

**"Zamani tulikuwa tunaenda pwani kuvua pweza, lakini kutokana na kuwa hakukuwa na utaratibu, tulikuwa tunapata mavuno madogo ambayo wakati mwingine hupata kitoweo tu, lakini sasa kwa utaratibu huu tunavua pweza ambao hata kama siyo sawa na wanaume, lakini tunapata mpaka laki na nusu (Sh. 150,000)," alitamba.**

## Ushirika wakopeshwa matrekta ya mil. 500/-

**Na Mwandishi Wetu, MWANZA**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imekabidhi matrekta tisa yenye thamani ya Sh. milioni 541.8, kwa vyama vya ushirika kwenye wilaya za Magu, Buchosa, Kwimba na Bunda ikiwa ni jitihada ya kuchagiza maendeleo ya kilimo nchini.

Makabidhiano kwa vyama vya ushirika wa mazao na masoko tisa katika halmashauri tatu za mkoa wa Mwanza na halmashauri moja mkoa wa Mara ulifanyika jijini hapa na Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Dk. Severine Lalika.

Meneja wa benki hiyo, Jumanne Kezilahabi, alisema TADB imedhamiria kuhakikisha inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuleta mapinduzi yenye tija katika sekta ya kilimo nchini kwa kusaidia upatikanaji wa fedha, vitendea kazi, kufanya utafiti na uboreshaji wa sera zitakazosaidia maendeleo ya kilimo nchini ili kuwanufaisha wakulima.

Alisema TADB imekuwa mdau mkubwa sana kuleta mapinduzi kwenye sekta ndogo ya pamba katika Kanda ya Ziwa, ambapo benki ilianza kwa kuvikopesha vyama vya ushirika matrketa huduma ya pembejeo kupitia kampuni za usambazaji.

Kwa mujibu wa Kezilahabi, hadi kufikia Januari 2020, TADB imekabidhi jumla ya matrekta 31 kati ya 50 kwa vyama vya ushirika kutoka Halmashauri za Sengerema, Buchosa, Kwimba, Misungwi, Magu na Bunda Mji.

"Nimatumaini ya benki kuwa matrekta haya yameongeza hari ya uzalishaji kwa wakulima na kuwapunguzia adha waliokuwa wakipata wakati wa maandalizi ya mashamba yao. Pia nje ya zao la pamba, matrekta haya yamekuwa yakiwasaidia wakulima kuandaa mashamba ya mazao mengine kama vile mpunga, na mahindi," alisema.

Alisema kuwa pamoja na kuwanufaisha wanachama wake wapatao 6,800, matrekta haya pia yanatumiwa na wakulima wasio wanaushirika, ambao wanakodisha matrekta haya kwa kulipia fedha kidogo kwa AMCOS.

Mkuu wa wilaya aliwakabidhi wakulima kutoka halmashauri nne za Buchosa (1), Kwimba (1), Magu (5) na Bunda mji (2). Trekta hizi zimenunuliwa kutoka kampuni ya LonAgro Tanzania Ltd (John Deere), zenye thamani ya Sh. milioni 541.8, kati ya hizo fedha za chama cha ushirika kitachangia asilimia 20 (Sh. 108,360,000) na TADB itakopesha asilimia 80 (Sh. 433,440,000).

# TPSF kusaka masoko ya bidhaa DRC

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) inatarajia kuongoza ziara ya wafanyabiashara wa Tanzania kwenda nchi ya Jamhuri ya Demokrasia ya watu wa Kongo (DRC) ili kunadi na kutafuta soko la uhakika la bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya Tanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu ziara hiyo ya siku tatu inayoanza tarehe 6 Machi hadi 8, Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, amesema ziara hiyo imekuja wakati mwafaka ambapo bidhaa kutoka sekta mbalimbali za kiuchumi zitanadiwa na kutafutiwa masoko DRC.

"TPSF tumeandaa ziara hii kwa lengo la kutangaza fursa za kiuchumi zilipo nchini, tunaamini Tanzania kwa sasa tunazalisha bidhaa bora kutoka katika viwanda vya ndani, sekta ya kilimo na mifugo, hivyo lazima tuweke mikakati ya namna ya kutumia fursa hizo hasa katika kipindi hiki ambacho TPSF ni Mwenyekiti wa Baraza la Biashara la Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)," alisema Ngalula.

Ngalula alisema taasisi, idara na wizara zinazohusika zimetaarifiwa na kwamba zimetoa baraka zake kwa ziara hiyo kufanyika DRC. "TPSF tumekuwa tukishirikiana kwa karibu na serikali katika kufanikisha mipango na malengo mbalimbali, hivyo tunaendelea kuzishukuru taasisi na idara zote za serikali kwa namna walivyotuunga mkono kufanikisha ziara hii, na kipekee kabisa tunaushukuru ubalozi wa Tanzania nchini Kongo kwa kueleleza maeneo yenye fursa kubwa kwa wafanyabiashara kwenda kuwekeza nchini humo," alisema.

"Tunaishukuru serikali ya Rais John Magufuli kwa kuimarisha miundombinu ambayo kwa kiasi kikubwa imeongeza uwekezaji na kukuza biashara ya ndani na nje ya nchi. Nitoe wito kwa wafanyabiashara kujitokeza kwa wingi katika ziara hiyo ili kwenda kuangazia fursa zilizopo kwa kuwa usafirishaji sio tatizo tena hasa ukizingatia uwepo wa reli ya Tazara, uwapo wa malori ya kutosha na hivi karibuni serikali imekusudia kufungua safari za Congo," alisema.

Mwenyekiti wa chama cha wasindikaji wa wadogo (TAFOPA), Suzie Laizer, alisema wanategemea kutangaza na kupanua wigo wa bidhaa za usindikaji kutoka Tanzania.

"Ziara ya Congo itasaidia katika kuongeza ukubwa wa biashara ya bidhaa kusindikwa ambazo tumekuwa tukizifanya kwa miaka mingi," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, aliwaomba wafanyabiashara kujitokeza kwa wingi na kuchangamkia fursa hiyo ya ziara nchini Congo kutangaza bidhaa zao na kupata masoko ya uhakika.

"Congo imekuwa ikiagiza bidhaa zake kutoka nchi mbalimbali, tukatumie fursa ya TPSF kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Biashara la SADC kutangaza bidhaa zetu, vivutio vya utalii, bidhaa katika sekta ya uvuvi pamoja na kilimo, hiyo itachangia kufikiwa kwa haraka uchumi wa kati na viwanda ka Taifa letu," alisema Simbeye.



Mwenyekiti wa kikao cha kujadili maeneo ya ushirikiano kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Mahmoud Omar Hamad ambaye ni Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti kutoka Wizara ya Habari, Utalii na Mambo Kale Zanzibar, akizungumza katika kikao hicho mjini Zanzibar, juzi. **PICHA: MAELEZO**

# Waziri abana watendaji uharibifu wa mazingira

**Na Robert Hokororo, GEITA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amewataka viongozi wa halmashauri za wilaya kujenga ukaribu na wananchi wa maeneo yanayozunguka migodi ili kusimamia vyema masuala yanayohusu mazingira na kutatua matatizo kwa haraka.

Alitoa agizo hilo jana katika ziara yake ya kikazi kukagua uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na kutoa elimu kuhusu athari za zebaki kwa wachimbaji wadogo mkoani Geita.

Katika ziara yake hiyo, Zungu ambaye alitembelea Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM) na wachimbaji wadogo wa Nyarugusu na Mgusu, alisema watendaji hususani maofisa mazingira wa halmashauri, lazima washirikiane na wananchi kuhakikisha mazingira yanatunzwa.

"Tumeambiwa hawaji kutembelea wananchi, jambo ambalo ni kosa kisheria, lazima wawe wanafika katika eneo hili washirikiane na jamii ya wachimbaji wadogo ambao ni wadau wakubwa.

"Eneo hili la Mgusu lina hifadhi ya msitu mkubwa na linahitaj kulindwa, zamani hapa walikuwa wanasafisha dhahabu kwenye mto, lakini wametii maagizo ya serikali na kuhamia upande wa juu, hivyo tuwapongeze," alisema.

Waziri huyo alisema halmashauri zitaendelea kuhamasishwa ili kuwapa miongozo na elimu kuhusu uhifadhi wa mazingira husus an vita dhidi ya ukataji miti kwa ajili ya migodi yao.

Aliwashukia wachimbaji wadogo wanaokata miti kwa ajili ya kuitumia katika migodi, akisema huo ni uharibifu wa mazingira hivyo akawataka wapande miti kwa wingi ili kuhifadhi mazingira.

Aliongeza kuwa mvua inayonyesha bila msimu ni matokeo ya ukataji miti ambayo unasababisha mabadiliko ya tabianchi, hivyo ni lazima wananchi wapande miti kwa wingi na kuitunza.

"Nilikuwa kwa RC (Mkuu wa Mkoa) Robert Gabriel, ana programu ya kupanda miti na anataka kuhusisha wanafunzi, ni vyema pia wakashirikishwa wachimbaji wadogo na wakubwa katika kupanda miti," aliagiza.

Waziri huyo pia alisema ipo haja ya kufanyia marekebisho Kanuni za Udhibiti Magugu Maji za Mwaka 1999 ili kuruhusu uvunaji magugu maji kwenye Ziwa Victoria. Alisema magugu maji ni sehemu nyingine ya uchafuzi wa mazingira na pia ni tishio kwa viumbe hai, hivyo kuna haja kuruhusu hatua ya kuyaondoa ziwani ili yatumike katika fursa mbalimbali.

"Sheria hii imepitwa na wakati, tunataka sasa magugu maji haya yawekewe kanuni ya kuyavuna na kuyasafirisha kwani samaki wanakosa hewa wanakufa, ng'ombe na wanyama wengine wanashindwa kunywa maji wakiogopa mamba wanaojificha humo," alisema.

Waziri huyo alisema mkakati uliopo ni kuwa na utaratibu wa kuyavuna na kuyaondoa kabisa magugu maji ili yatumike katika shughuli mbalimbali ikiwamo kutengeneza nishati mbadala na mifuko.

Ofisa Kilimo Mkuu Kitengo cha Afya ya Mimea, Wizara ya Kilimo, Elinisha Mb-

HABARI KIMATAIFA

## Kim asimamia urushaji makombora masafa marefu

**PYONGYANG,** Korea Kaskazini

KOREA Kaskazini inaendelea na mpango wake wa kurusha makombora ya masafa marefu, baada ya mazungumzo na Marekani kusimama kwa muda mrefu.

Siku ya Jumatatu, Kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong-un, alisimamia zoezi la kurusha makombora ya masafa marefu, shirika la habari la serikali KCNA liliripoti jana.

Tangazo hilo linakuja baada ya Korea Kusini kubaini mwanzoni mwa wiki kwamba Korea Kaskazini ilifanya majaribio ya makombora mawili ya masafa mafupi kutoka pwani yake ya Kusini kuelekea baharini.

Picha zilizotolewa na vyombo vya habari vya serikali huko Pyongyang zinaonyesha wanajeshi wa Korea Kaskazini wakijaribu kutumia bunduki kubwa ya kurusha roketi nyingi, banduki iliyonekana kwa mara ya kwanza mwaka jana.

Januari 1, mwaka huu Kim alisema kwamba nchi yake inataka kuendelea kuimarisha mpango wa nyuklia na kuzindua silaha mpya ya mkakati katika siku za usoni, baada ya kushindwa kuanza tena kwa mazungumzo na Marekani. **RFI**

## Mjumbe wa UN Libya ajiuzulu

**TRIPOLI,** Libya

MJUMBE maalumu wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini Libya, Ghassan Salamé, ameandika kwenye ukurasa wa kijamii wa Twitter kwamba amejiuzulu kwenye nafasi yake.

Ameeleza kuwa amechukuwa uamuzi huo kwa sababu za kiafya baada ya kushikilia nafasi hiyo kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili na nusu.

"Inanibidi nikiri kwamba afya yangu haniruhusu tena kuendelea kupata mfadhaiko, kwa hivyo nimemuomba Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuniruhusu kuachia ngazi," aliandika Ghassan Salamé, ambaye ni raia wa Ufaransa mwenye asili ya Lebanon.

Kujiuzulu kwake kunakuja baada ya mkutano na waandishi wa habari aliofanyika Februari 29, mwaka huu huko Geneva baada ya kushindwa kwa mazungumzo ya kisiasa katika ya wadau katika mgogoro unaoendelea nchini Libya.

Katika mkutano huu na waandishi wa habari, Ghassan Salamé alionekana akiwa na ghadhabu dhidi ya kambi zinazohasimiana nchini humo, ambazo haziheshimu ahadi zao walizoafikia huko Berlin.

Salamé alishutumu pande zote mbili kwa kueneza uwongo juu ya mazungumzo ya Geneva kuhusu uteuzi wa wawakilishi wanaotakiwa kushiriki kwenye mazungumzo hayo.**RFI**

# Waliofariki corona wafikia 3,100, maambukizi 90,000

**BEIJING,** China

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema idadi ya watu waliofariki kwa ugonjwa wa corona duniani imefikia 3,100 na walioambukizwa ni 90,000.

Vile vile limeonya kwamba dunia imeingia katika hali ya mtafaruku katika mapambano yake dhidi ya virusi vya Corona, wakati maambukizi mapya yameshuka nchini China lakini yanaongezeka katika nchi nyingine.

Limesema nchini Marekani idadi ya watu waliofariki imepanda na kufikia watu sita. Limesema wakati hali ya mzozo huo inabadilika, ambapo idadi ya zaidi ya mara tisa ya maambukizi yamerekodiwa nje ya China.

**China imeripoti kupungua kasi kwa maambukizi mapya ya virusi vya corona katika siku moja iliyopita, wakati maambukizi mapya yameongezeka nchini Korea kusini.**

Mwakilishi wa kudumu wa China katika Umoja wa mataifa, Zhang Jun alisema nchi yake inapiga hatua katika mapambano hayo.

China imeripoti kupungua kasi kwa maambukizi mapya ya virusi vya corona katika siku moja iliyopita, wakati maambukizi mapya yameongezeka nchini Korea kusini.

Kadhalika, China imeorodhesha watu wapya 125 walioambukizwa, ikiwa ni idadi ya chini tangu mwezi Januari. wakati huo huo watu 31 wamefariki na kufikisha idadi ya watu 2,943.

Wakati huohuo, Korea Kusini imetangaza kesi mpya 600 za maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo, na idadi hiyo inakamilisha watu 4,812 walioambulizwa virusi hivyo tangu ugojnwa huo ulizuka.

Katika taarifa yake ya kila siku, Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (KCDC) pia kimethibitisha vifo vipya vitatu. Watu 34 wamefariki dunia nchini Korea Kusini kutokana na virusi hivyo, kituo hicho kimebaini katika taarifa.

Kesi nyingi zimeripoitwa huko Daegu, mji unaopatikana Kusini-Mashariki mwa nchi ambapo kuna kundi la kidini ambalo haliitikii wito wa kujizuia au kujilinda na ugonjwa huo.

Mwanzilishi na kiongozi wa kundi hilo la kidini la Shincheonji, Lee Manhee, alitaja mlipuko wa ugonjwa huo kama janga na akaomba msamaha kwa kuenea kwake, huku akikataa kufanya vipimo. **DW**



Wanajeshi wa Korea Kusini katika zoezi la kupambana na kuenea kwa virusi vya Covid-19 huko Daegu, **PICHA: REUTERS**

# Meya ajitoa mbio za urais Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

MEYA wa zamani wa Jimbo la South Bend, Indiana, Pete Buttigieg ameamua kujitoa katika kinyang'anyiro cha kuwania urais wa Marekani unaotarajia kufanyika mwaka huu.

Kampeni ya Buttigieg ilitangaza Jumapili jioni kuwa mgombea wao ameamua kuchukua hatua hiyo baada ya kumaliza katika nafasi ya nne ambapo hakupata wajumbe wowote.

Wakati huo huo, Makamu wa Rais wa zamani wa Marekani Joe Biden, aliyeshinda kwa kishindo uchaguzi wa chama hicho South Carolina, anakabiliwa na changamoto mpya kutoka kwa Seneta wa Vermont Bernie Sanders wakati majimbo 14 yatakapopiga kura Jumanne katika mashindano ya chama kote nchini Marekani.

Biden, alikuwa hajawahi kushinda kwenye jimbo lolote katika uchaguzi huo wa awali wa urais mara tatu hadi mafanikio hayo ya Jumamosi.

Lakini utafiti wa maoni kabla ya uchaguzi unaonyesha kwamba Sanders, mwenye mrengo wa kushoto wa kisoshalisti aliyejitangaza kugombea kupitia chama cha Demokratic, anaongoza kwa kiasi kikubwa huko California.

Inatarajiwa kuwa atakuwa atapata kura nyingi kutoka kwa wajumbe wa mkutano mkuu ujao wa kitaifa wa uteuzi wa mgombea wa chama cha Demokrat katika msimu wa joto katika duru ijayo ya kupiga kura. **RFI**

# BM sasa kuunganisha magari nchini

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kimeahidi kutoa ushirikiano kwa mwekezaji wa kiwanda cha kuunganisha magari BM kilichopo Zegereni, Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani.

Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Zacharia Mganilwa, alitoa msimamo huo jana, wakati timu ya baadhi ya wataalamu ilipotembelea katika chuo hicho.

Profesa Mganilwa alisema, Chuo cha NIT kitatoa msaada wa wataalamu kwa kampuni hiyo kutengeneza magari yenye kiwango na pia wapo watakaotoa ushauri kuhusiana na bei za kuuza magari hayo.

Alisema, chuo hicho kina maabara ya kupima injini, uwiano wa mfumo wa gari, kiti cha dereva, viti vya abiria, usalama wa gari barabarani na baadaye kutaandaa ripoti.

"Hata gari itakapoanza safari, tutaendelea kuzikagua kuona utendaji kazi wake likiwa barabarani, tutaendelea kushirikiana na mwekezaji huyu kutoa vitu vyenye ubora," alisisitiza.

Kuhusu uunganishaji wa magari, Mkurugenzi wa Kampuni ya BM, Jonas Nyagawa, alisema anatumia gharama kubwa kuagiza magari kutoka nje ya nchi na ameamua kuanzisha kiwanda hicho kupunguza gharama za uagizaji.

Nyagawa alisema, kwa sasa kazi ya kuunganisha magari mawili imefikia asilimia 80 na hadi kukamilika yatagharimu zaidi ya Sh. milioni 400 na kuokoa Sh. milioni 500 endapo angeagiza magari hayo nje ya nchi.

Alisema, uundaji wa magari hayo umechukua miezi sita.



Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo (wa pili kushoto), akipokea maelezo ya uzalishaji wa kiwanda cha kisasa cha nyama cha TANCHOICE, kilichopo Kibaha, kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Rashid Abdulah (kushoto), wakati wa ziara yake ya kutembelea miradi ya maji inayotekelezwa na Dawasa, mkoani humo, jana. **PICHA: FRANK MONYO**

# Kortini mashtaka kusafirisha heroin

**Na Hellen Mwango**

WATU watatu wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam wakikabiliwa na tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroine gramu 509.63.

Wanaoshtakiwa ni Jimmy Mlaki mkazi wa Kinondoni Moscow, Stanley Ngowi 'Sultan' mkazi wa Tabata Segerea na Issa Omar mkazi wa Kimara.

Walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa Januari 27, mwaka huu eneo la Ubungo Kibo, Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam walikutwa wakisafirisha dawa hizo.

Kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo, washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote.

Wakati huohuo, Daniel Chizuwa, mkazi wa Kigamboni, jijini Dar es Salaam, amefikishwa mahakamani hapo kwa tuhuma za kukutwa na nyara za serikali.

Ilidaiwa kuwa Januari 22, 2020 katika maeneo ya Masaki Cliff Side, Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam alikutwa na kobe wawili wenye thamani ya Sh. 320,600, mali ya Serikali ya Tanzania bila kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Mshtakiwa Daniel aliruhusiwa dhamana kwa masharti ya kuleta mdhamini mmoja na kulipa bondi ya Shilingi milioni tano.

Kesi zote mbili zimepangwa kutajwa Machi 17, mwaka huu.

**Wanaoshtakiwa ni Jimmy Mlaki mkazi wa Kinondoni Moscow, Stanley Ngowi 'Sultan' mkazi wa Tabata Segerea na Issa Omar mkazi wa Kimara.**

# Kigwangalla aiagiza Tafori utafiti miti

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, ameiagiza Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (Tafori), kufanya utafiti wa miti inayoweza kupandwa na ikakua kwa muda mfupi itumike kuzalisha mkaa.

Kigwangalla amesema hatua hiyo itasaidia kuilinda misitu ya asili.

Waziri Kigwangalla, alitoa agizo hilo wakati akizindua Bodi ya 11 ya Wakurugenzi ya Tafori mjini Morogoro.

Alisema kuwa matumizi ya mkaa yamekuwa yakiathiri na kuchangia kukatwa kwa kiwango kikubwa cha misitu ya asili, hali ambayo inasababisha baadhi ya miti muhimu kuwapo kwa tishio la kutoweka kwake, hivyo kama utafiti huo utafanikiwa, utasaidia kuokoa miti hiyo ya asili.

Dk. Kigwangalla, alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi ikiwamo misitu yenye eneo la hekta milioni 48.1, sawa na asilimia 55 ya eneo la ardhi ya nchi mzima.

Alisema pamoja na kuwapo kwa misitu hiyo, lakini takwimu zinaonyesha uharibifu wa misitu ni kiasi cha hekta 469,420 kwa mwaka, na vyanzo vikuu vya uharibifu huo ni pamoja na ongezeko la watu, umaskini, ukuaji wa biashara, ukuaji wa miji, kilimo cha kuhamahama na wakimbizi.

Aliwataka Watanzania wawe na tabia ya kutumia matokeo ya utafiti katika kuendeleza usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu ili ziwasaidie kufaidika nazo bila kuziharibu.

Aliitaka bodi hiyo kufuatilia hali ya upatikanaji wa mbao ngumu katika maeneo tofauti tofauti ili kujua kiasi cha rasilimali hiyo kilichopo, kwani asilimia 98 ya mbao ngumu inatoka katika misitu ya asili.

Aliagiza bodi hiyo iendelee kuboresha maabara zilizopo kwenye taasisi hiyo ili kuhakikisha utafiti unafanyika katika mazingira mazuri ambayo yanatoa matokeo sahihi na yenye viwango vya kimataifa.

Awali Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dk. Felician Kilahama, alisema mafanikio mengi yamepatikana kwenye taasisi hiyo katika Mpango Kakambe wa Pili wa miaka 10 (2011- 2020), wa Mkakati wa Utafiti wa Misitu nchini.

Alimwomba waziri huyo kumfikishia ombi Rais John Magufuli, la kumpata Mkurugenzi Mkuu wa Tafori ili bodi iweze kufanya kazi vizuri na kwa uhakika, kwa kuwa tangu mwaka 2012 haijawahi kumpata.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

## KUPOTEA KWA CHETI



**Rayhope Mpazi Mkamba** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo; cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0867-0116** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2011 katika Shule ya Sekondari Pandahill na cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S1527-0062** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2014 katika Shule ya Sekondari Scolastika .

**Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**DSM/PHQ/RB/187154/2020**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARTHA ALLAN MROKI anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0184/0025 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia AGAPE LUTHERAN JUNIOR SEMINARY mwaka 2013.**

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi:**
**DAR/OST/RB/162045/2020.**

115653502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo:
MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;45/2020

Ombi la JUMA SALUM SAID Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SALUM SAID SALUM.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 05/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 25/02/2020.

HAKIMU
MOROGORO

115653702

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
LAND DIVISION
AT MWANZA
LAND CASE 43 OF 2007

DEVOTHA MKUBWA ......................PLAINTIFF
VERSUS
MWANZA CITY COUNCIL & 5 OTHERS ......DEFENDANTS

TO: NKUNKAR LIMITED
P.O. BOX 16-MWANZA
SUMMONS TO APPEAR

TAKE NOTICE that the above suit has fixed for Mention/Hearing on the 5 day of March 2020 At 9:00 a.m. Before Hon J. TIGANGA JUDGE.

YOU ARE required to appear in this court on the fixed date without fail.

In default of your appearance on that day before mentioned, the suit will be heard and determined in your absence.

Given under my Hand and seal of this court,this 12 day of February 2020

Copy to:

THE HIGH COURT OF TANZANIA MWANZA

DEPUTY REGISTRAR

115653602

## KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FAIR DEAL AUTO PVT LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipik Sina ya BAJAJI BOXERi yenye namba za usajili MC960AHV Chesis no.MD2A21BZ6F-WK52951 na Engine no.PFZWFK47853.

Yeyote ataeona atoe taarifa kituo Cha polisi.
DOD/DOD/RB/196312/2020

156538

## KUPOTEA KWA KADI

**Adam Said Rajabu** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Pikipiki aina ya TVS yenye Usajili wa namba MC960 CBS iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/KIJ/RB/198002/2020**

115653402

Uza, Chenye Thamani Kubwa

Kwa Kutangaza Nasi Kwa

Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HAALAND SASA ATAKA KUMFUATA IBRAHIMOVIC




**DORTMUND,** UJERUMANI

ERLING Haaland amesema atapenda kupita kwenye njia alizopita shujaa wake, Zlatan Ibrahimovic, jambo linalowapa matumaini Manchester United kuwa kuna siku wataweza kunasa saini yake.

Haaland alikuwa kwenye rada za Man United katika dirisha la Januari, lakini Borussia Dortmund waliingilia kati na kumsainisha wakiipa RB Salzburg pauni milioni 17.1.

Tangu atue Ujerumani, Haaland mwenye umri wa miaka 19, amefunga mabao 12 katika mechi tisa, ikiwa ni mabao mawili tu pungufu ya Marcus Rashford kwa msimu huu.

Haaland ghafla amekuwa gumzo huko Ulaya akisakwa na timu nyingi, huku Man United wakisakamwa kwa kushindwa kunasa saini yake. Lakini, mwenyewe alisema atakuwa mwenye furaha akipita njia alizopita Zlatan, ambaye ni mshambuliaji wa zamani wa Man United.

"Napenda akili yake na namna anavyoona mambo. Nadhani hata mimi ninajiamini, hivyo najiona kwa Ibra," alisema akinukuliwa na gazeti la Bild.

"Sisi sote ni washambuliaji, sote ni warefu. Lakini, tunatofautiana staili ya kucheza, hivyo ni ngumu kutulinganisha."

Ibrahimovic si mchezaji pekee wa zamani wa Man United, ambaye Haaland anamhesabu kuwa ni shujaa wake, kwani pia yumo kocha Ole Gunnar Solskjaer, waliyekuwa naye pamoja huko Molde na raia mwenzake wa Norway.

# Sturridge afungiwa kucheza, kisa kubeti

**LONDON,** England

DANIEL Sturridge amefungiwa kutocheza soka sehemu yoyote duniani hadi mwishoni mwa msimu huu, baada ya kufanikiwa kwa rufani ya Chama cha Soka cha England (FA) dhidi ya hukumu ya kwanza ya kujihusisha na kucheza kamari maarufu 'kubeti'.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Liverpool awali alifungiwa kwa wiki mbili na kupigwa faini ya pauni 75,000 Julai mwaka jana baada ya kutoa taarifa za ndani kuhusu uhamisho wa kaka yake Leon kwenda kwa miamba wa LaLiga, Sevilla, ambao haukufanikiwa.

FA iliona adhabu hiyo ni ndogo na ikaamua kukata rufani ili Sturridge apate adhabu kubwa zaidi.

Sturridge ambaye aliachwa na klabu yake ya Trabzonspor ya nchini Uturuki Jumatatu sasa amefungiwa kutojihusisha na soka hadi Juni 17, mwaka huu pamoja na faini ya pauni 150,000.

"Daniel Sturridge amefungiwa kutojihusisha na soka sehemu yoyote duniani hadi Juni 17, 2020," ilisema taarifa ya FA.

"Baada ya rufani ya FA kutokana na adhabu ya awali, bodi huru ya uchunguzi imebaini Strurridge alivunja sheria kwa kutoa taarifa za ndani kuhusu uhamisho.

"Pia FA imemkuta na makosa mengine mawili ambayo hakupewa adhabu yake, hivyo Sturridge amefungiwa hadi mwishoni mwa msimu huu."

Sturridge kabla ya kutemwa na Trabzonspor aliyojiunga nayo miezi saba iliyopita, alicheza pale Liverpool kwa kipindi cha miaka sita.

Sturridge amefunga mabao nane katika mechi 26 alizoichezea England.




# Foden atupia jicho England Euro 2020




**MANCHESTER,** England

PHIL Foden ana matumaini ya kuingia kwenye kikosi cha wakubwa cha timu ya Taifa ya England kwa ajili ya michuano ya Euro 2020, baada ya kuiongoza Manchester City kutwaa taji la EFL, Jumapili.

Foden mwenye umri wa miaka 19, alikuwa mchezaji bora dimbani wakati City wakipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Aston Villa, akitwaa tuzo ya nyota bora wa mchezo vijana hao wa Pep Guardiola wakibeba taji hilo pale kwenye Uwanja wa Wembley.

Mchezaji huyo aliyetokea kwenye akademi ya City, alitengeneza bao la kwanza lililofungwa na Sergio Aguero, kabla ya kuonyesha kiwango cha kuvutia akicheza winga ya kulia.

Kocha wa England, Gareth Southgate alimtaja Foden kama mchezaji bora wa baadaye na kwamba mchezaji huyo anaweza kufanya makubwa zaidi kabla ya mashindano hayo.

"Nataka kuwa pale (kwenye michuano ya Euro), kwa uhakika, lakini ni ngumu mno kutokana na wachezaji walioopo pale," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

HABARI MICHEZO

# Arteta: Kutofuzu Uefa kutaigharimu Arsenal

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amebainisha kwamba, klabu hiyo itakuwa kwenye wakati mgumu kuwashawishi wachezaji wakubwa kama watashindwa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu wa nne mfululizo.


'Washikabunduki' hao wanakabiliwa na uwezekano wa kutofuzu kucheza michuano ya Ulaya msimu ujao na kwa namna moja au nyingine itawaathiri kwenye mapato yao ya kifedha.

Kichapo walichokipata kutoka kwa Olympiakos kwenye Kombe la Europa kiliwatoa kwenye mashindano hayo hatua ya 32 na sasa wapo nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England.

Na sasa kocha huyo mwenye umri wa miaka 37, anajua kwamba, kukosa kwao kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya pia kutawafanya wawe kwenye wakati mgumu kuwashawishi kubaki wachezaji wenye vipaji kama Pierre-Emerick Aubameyang na Alexandre Lacazette.

"Nafikiri hakuna namna," alijibu Arteta wakati alipoulizwa kama kusajili wachezaji wapya wakati watakaposhindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya itakuwa vigumu.

"Kila mchezaji duniani anataka kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya na kama timu inashindwa kufuzu kwenye mashindano hayo, ni ngumu kuwashawishi wachezaji wakubwa kubaki au kusajili wapya."



TUMEWEZA...




Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe (katikati), Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira (wa pili kushoto) pamoja na baadhi ya wakimbiaji wa Benki ya Biashara ya DCB, Asnath Sayango (wa pili kulia), na Caroline Gabriel wakishiriki mbio za kujifurahisha za kilomita 5 wakati wa mashindano ya Kilimanjaro Marathon 2020 yaliyofanyika Mjini Moshi, Jumapili iliyopita. **NA MPIGAPICHA WETU**



# KLOPP: NITAKUWA MJINGA KUKITILIA SHAKA KIKOSI LIVER

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema atakuwa "mjinga mkubwa" kuwatilia shaka wachezaji baada ya matumaini yao ya kumaliza Ligi Kuu ya England bila kupoteza mchezo kufikia mwisho.

Kipigo cha Jumamosi cha mabao 3-0 kutoka kwa Watford kilimaliza matumaini ya Liverpool kumaliza msimu wa Ligi Kuu bila kupoteza - baada ya kucheza mechi 44.

Liverpool, bado inaongoza msimamo wa Ligi Kuu kwa pointi 22 na ipo kwenye nafasi nzuri ya kutwaa taji lake la kwanza la Ligi Kuu tangu mwaka 1990.

Na Klopp amesema ana imani kubwa na kikosi chake kabla ya mchezo wa jana Jumanne dhidi ya Chelsea wa Kombe la FA raundi ya tano.

"Kwa uhakika sina shaka kabisa na vijana wangu na nitakuwa mjinga mkubwa kama nitafikiria hivyo, kwa sababu wachezaji wanastahili imani yangu," alisema.

"Inaweza kutokea kwamba nakuwa na hasira, lakini siwezi kuwa na hasira na wachezaji ninapokutana nao.

"Kama nitakutana na kuwakaripia kama wamepoteza mechi 10 kwa hakika hilo litakuwa jambo la ajabu kweli."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MBAPPE KUIONGOZA UFARANSA OLIMPIKI

●●● Yupo katika kikosi cha awali cha wachezaji 80, orodha hiyo itapungua na kubaki 50 kisha 18+...

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amechaguliwa katika kikosi cha awali cha Ufaransa kitakachoshiriki michezo ya Olimpiki jijini Tokyo, Japan, Rais wa Shirikisho la Soka Ufaransa (FFF), Noel Le Graet amesema.

Nyota huyo wa Paris Saint-Germain na mshindi wa Kombe la Dunia, Mbappe, 21, yumo katika kikosi hicho cha awali cha wachezaji 80 walioitwa kwa ajili ya michuano hiyo, ambayo kwa timu ya wanaume inatakiwa kuundwa na wachezaji wenye umri chini ya miaka 23 huku kila timu ikiruhusiwa kujumuisha wachezaji wasiozidi watatu wenye umri mkubwa zaidi ya huo.

**Kwa upande wa soka katika michuano hiyo ya Olimpiki Tokyo, itaanza Julai 23 na kumalizika Agosti 8, mwaka huu wakati huu mabingwa watetezi, Brazil wakitolea jicho kutwaa medali nyingine ya dhahabu.**

"Mbappe yupo katika kikosi cha awali cha wachezaji 80 kwa ajili ya Michezo ya Olimpiki, kilichoandaliwa na kocha Sylvain Ripoll. Orodha hiyo itapungua na kubaki 50, kabla ya kuchujwa na kuwa 18 + wanne wa akiba," Le Graet aliwaambia wanahabari.

"Ana umri unaomwezesha kwenda [U-23]. Kama ilivyo kwa wachezaji wote wa umri wake ambao wana vipaji, kwa hiyo yupo kwenye orodha... Nimekutana na [Rais wa PSG] Nasser [Al-Khelaifi]. Nimemuuliza namna Mbappe anavyoendelea. Aliniambia: 'Vizuri sana'. Hapo ndipo tulipo.

"Kwa ujumla, rais wa klabu anahisi tarehe [ya Michezo ya Olimpiki] si nzuri haswa. Ni kama hivyo."

Mbappe amekuwa nyota kwa mabingwa wa Ligue 1, PSG msimu huu, akifunga mabao 18 kwenye ligi na 27 kwa ujumla kwenye michuano yote.

## ZISIKUPITE

### POGBA AREJEA KUJIFUA UTD

KIUNGO Mfaransa Paul Pogba, 26, atarejea kujifua na kikosi cha kwanza cha Manchester United wiki hii na yupo tayari kuendeleza ushirikiano na msajiliwa wa Januari, Bruno Fernandes. ***(ESPN)***

### BECKHAM AMTAKA STURRIDGE

ASTON Villa na klabu ya David Beckham inayoshiriki Ligi Kuu Marekani (MLS), Inter Miami zote zinavutiwa kumsajili mshambuliaji raia wa England, Daniel Sturridge, 30, ambaye kwa sasa amefungiwa kucheza soka hadi Juni 17. ***(Sun)***

### UPAMECANO LULU ARSENAL

BEKI wa RB Leipzig, Mfaransa Dayot Upamecano, 21, anawindwa na Arsenal, amesema anajisikia "vizuri sana" katika klabu yake ya sasa. ***(Mirror)***

### UTD KUMVUNJIA BENKI SANCHO

MANCHESTER United inaongoza mbio za kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, 19, kwa ada itakayoweka rekodi Ligi Kuu England katika majira ya joto. ***(Telegraph)***

### MADRID, PSG NAZO VITANI

REAL Madrid na Paris St-Germain pia zinamfuatilia Jadon Sancho, ambaye anapendelea kurejea England. ***(Mirror)***

### RB LEIPZIG KUMKOSA ANGELINO

KOCHA wa RB Leipzig, Julian Nagelsmann angependa kumbakisha beki wa kushoto wa Manchester City, Angelino, 23, lakini amesema 'dau kubwa' la Mhispania huyo kwa kujiunga nayo jumla linaweza kuwa tatizo. ***(Kicker - in German)***

### LAMPARD AMWONA KEPA

KOCHA Frank Lampard anaamini kipa wa Chelsea asiyekubalika, Mhispania Kepa Arrizabalaga, 25, bado ana mustakabali wa baadaye katika klabu hiyo. ***(Mail)***

### HOLGATE YEYE EVERTON TU

BEKI wa England Mason Holgate, 23, amesema mtazamo wake upo Everton huku klabu nyingi kama Manchester City zikivutiwa naye. ***(Mail)***

### ARTETA AHOFU TABU USAJILI

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anaamini klabu hiyo kama itashindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, itapata wakati mgumu wa kuwavutia wachezaji kujiunga nayo. ***(ESPN)***

### YAMFUATILIA TAYLOR

LEICESTER inamfuatilia beki wa Burnley, Muingereza Charlie Taylor, 26, kama mbadala wa nyota wa kimataifa wa England, Ben Chilwell, 23. ***(Times)***

### TELLES AIFUNGULIA CHELSEA

BEKI Mbrazil, Alex Telles, 27, anayewindwa na Chelsea, amekataa kuongeza mkataba na Porto. ***(A Bola, via Sun)***

## HABARI MICHEZO

## Simba wamlilia nguli Kimti

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Klabu ya Simba umeeleza kupokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha mchezaji wake wa zamani, Damian Mrisho Kimti aliyefariki dunia juzi jioni jijini Dar es Salaam.

Kimti alikuwa mmoja wa wachezaji ambao walicheza mchezo wa fainali ya ubingwa wa Afrika Mashariki mwaka 1992 ambao Simba ilibuka na ushindi dhidi ya Yanga na pia alikuwa sehemu ya kikosi kilichocheza fainali ya Kombe la CAF mwaka 1993 dhidi ya Stella Abidjan.

"Klabu itamkumbuka Kimti kwa mchango wake mkubwa alioutoa kwetu kwa kipindi chote ambacho alikuwa akichezea timu yetu.

"Simba inaungana na familia pamoja na wadau wa mpira wa miguu katika msiba huu. Tunatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na watu wote walioguswa na msiba huu. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi," ilieleza taarifa ya klabu hiyo jana.



## Bakuli gofu latua BMT

**Na Saada Akida**

WAKATI michuano ya Gofu Afrika ikitarajiwa kuanza Machi 30, mwaka huu nchini Namibia, Chama cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU), kimebisha hodi Baraza la Michezo la Taifa (BMT), kwa ajili ya kuomba msaada wa kuisafirisha timu ya Taifa.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Rais wa chama hicho, Sophia Reiffenstein, alisema baada ya kutafuta mdhamini kwa muda mrefu na kukosa, wameamua kupeleka barua BMT kuomba msaada wa kuwawezesha kuisafirisha timu ya taifa kwenda kushiriki kitimtim hicho.

Alisema barua ambayo wameipeleka BMT jana baada ya mipango yao yote kushindikana ni ya kuomba msaada wa nauli.

"Baada ya kuhangaika sana kutafuta wadhamini kwa kupeleka maombi mbalimbali, tumemuandikia barua Katibu wa BMT kuomba msaada wa kusaidia timu yetu kwenda Namibia, ikiwezekana kupata mahitaji mengine ikiwamo chakula na malazi," alisema Sophia.

Alisema michuano hiyo itakuwa ya siku 10, huku timu ikitakiwa kusafiri Machi 27, mwaka huu, ikiwa ni siku tatu kabla ya michuano hiyo kuanza.

# KMC KUANZA NA JKT IKIPANIA KUJINUSURU

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kufungwa mabao 2-0 na Simba katika mechi iliyopita, Kocha Mkuu wa KMC FC ya jijini Dar es Salaam, Haruna Harerimana, amesema ana matumaini makubwa ya kufanya vizuri katika michezo 13 iliyobaki na hatimaye kujinusuru na janga la kushuka daraja.

KMC FC inashika nafasi ya 19 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa na pointi 21 huku Singida United yenye pointi 12 ikiburuza mkia.

**Akizungumza na gazeti hili jijini juzi, Hererimana alisema kwa sasa wanapambana kutafuta alama 39 katika michezo hiyo iliyobaki na ana matumaini watabaki Ligi Kuu.**

Kocha huyo alisema wamepoteza michezo minne mfululizo, hivyo hawatakuwa tayari kuona wanaendelea kufanya vibaya katika ligi hiyo ambayo idadai ya timu zinazoshuka daraja zimeongezeka.

"Bado nina imani na timu yangu, hata tukiwa tunapata pointi moja moja, tutapanda juu kutokana na kutopishana sana alama kati ya sisi na timu zilizopo juu yetu," Hererimana alisema.

KMC itashuka Uwanja wa Uhuru leo kuikaribisha JKT Tanzania yenye pointi 38 na katika msimamo wa ligi iko katika nafasi ya nane baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 25.

## MARATHON...




Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo Tanzania, Simon Karikari, akiwasalimia washangiliaji wakati wa mbio za Tigo Kili nusu Marathon 2020, zilizofanyika Moshi mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Polisi Tanzania wataka tatu za Mwadui*

**Na Mwandishi Wetu**

IKITOKA kukusanya alama tatu katika Uwanja wa Liti (zamani Namfua) dhidi ya Singida United, Polisi Tanzania itashuka katika dimba la CCM Kambarage mjini Shinyanga leo kusaka alama nyingine tatu muhimu.

Jumamosi iliyopita, Polisi Tanzania iliyopo nafasi ya tano na alama zake 40, iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Singida United inayochechemea mkiani mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 12 baada ya mechi 25.

Hivyo, leo itashuka dimbani kuivaa Mwadui iliyoutumia vema uwanja wake wa nyumbani Jumamosi iliyopita kwa kuibugiza Coastal Union ya Tanga mabao 2-0 yaliyoifanya kufikisha alama 26 katika nafasi ya 16.

Akizungumzia mchezo huo, mshambuliaji tegemeo wa Polisi Tanzania, Marcel Kaheza, alisema leo watakuwa na kazi kubwa mbele ya Mwadui FC kwenye mchezo huo utakaochezwa Uwanja wa Kambarage.

Kaheza alisema mbinu nyingi wanazopewa na benchi la ufundi, anaamini zitaendelea kuwapa matokeo chanya kwenye ligi hiyo iliyopo katika raundi ya 26.

Kaheza amekuwa kwenye ubora wake msimu huu chini ya kocha Malale Hamsini na tayari amehusika katika mabao tisa kati ya 27 waliyofunga Polisi Tanzania huku akicheka na nyavu mara tano na kutoa pasi za mwisho nne.

# Michezo

Jumatano Machi 4, 2020

Nipashe




Mbappe kuiongoza Ufaransa Olimpiki UKURASA 30

YALAAAH...



Kiungo wa Arsenal, Lucas Torreira (juu) akilalama baada ya kuchezewa rafu mbaya na beki wa Portmouth, James Bolton, iliyomlazimu kutolewa uwanjani kwa machela kwenye mechi ya raundi ya tano Kombe la FA England iliyopigwa katika Uwanja wa Fratton Park juzi na Gunners kushinda 2-0 kupitia kwa Sokratis Papastathopoulos na Eddie Nketiah. **PICHA: MTANDAO**

# Simba: Azam FC daraja la Yanga

●●● Sven asema wataitumia leo kufikisha salamu Jangwani, Bocco na meneja watoa yao, lakini...

**Saada Akida na Shufaa Lymo**

KATIKA Kuhakikisha wanafikia malengo, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck amesema wamejipanga kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi dhidi ya Azam FC itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa.

**Simba wanaongoza Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na alama 65 baada ya mechi 25, wamepania kuhakikisha mchezo dhidi ya Azam unakuwa ni maandalizi kwa ajili ya kukabiliana na mahasimu wao Yanga hapo Jumapili wiki hii.**

Akizungumza na Nipashe jijini jana, Sven alisema anatambua mchezo utakuwa mgumu, lakini anaamini matokeo ya ushindi katika michezo mitano iliyopita ni ishara nzuri katika mchezo huo kupata alama tatu.

Alisema yuko makini kukisuka kikosi chake kuhakikisha kila wanapomaliza mchezo wanakuwa na maandalizi ya mchezo unaofuata.

"Kila kitu ni hatua na kwa sasa tulipo si sehemu mbaya, tunahitaji kuona tunapata matokeo mazuri yatakayotufanya tuzidi kuwa imara," alisema kocha huyo.

Alisema malengo yao ni kufanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yao ikiwamo huu wa Azam ambao ni mazoezi tosha kuelekea mechi dhidi ya Yanga. Alisema kwa sasa hawadharau timu yoyote wanayokutana nayo kutokana na kuhitaji kufanya vizuri na kupata pointi kila mechi kwa michezo iliyobaki.

Naye nahodha wa Simba, John Bocco alisema kuvuna pointi tatu katika kila mchezo kati ya mitano iliyopita kunawapa hamasa ya kutafuta alama zingine katika mechi dhidi ya Azam ambayo itakuwa maandalizi mazuri kwa ajili ya pambano dhidi ya Yanga.

"Wachezaji tumejiwekea mikakati ya kutafuta alama tatu, hivyo KMC ilikuwa ni maandalizi ya mchezo wetu dhidi ya Azam, tunahitaji kupata pointi ili tufikie malengo yetu ya kutwaa taji la ubingwa mara tatu," alisema Bocco.

Lakini Meneja wa klabu hiyo, Patrick Rweyemamu alisema: "Tupo vizuri kukutana na Azam wachezaji wana morali kuhakikisha wanatoka na ushindi na kupeleka maangamizi hayo Jumapili.

"Tunaiheshimu Azam ni timu nzuri tumejipanga kuhakikisha hatuwapi nafasi ya kuliona goli letu kirahisi."

Kwa upande wa Azam FC walisema, jana walifanya mazoezi ya mwisho huku kila mchezaji akiwaza ushindi katika mchezo huo.

Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema kikosi kipo vizuri na kuwataka mashabiki wao kujitokeza kwa wingi uwanjani leo.

## Cheche afunguka kutimuliwa Azam

**Na Shufaa Lyimo**

ALIYEKUWA Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Nassor 'Cheche' amesema ameyapokea maamuzi yaliyofanywa na uongozi wa klabu hiyo kwa kumwondoa katika benchi la ufundi.

Akizungumza na Nipashe jana, alisema ameondoshwa akiwa hana tatizo na uongozi na kudai anakwenda kuanza maisha mengine.

"Mimi nimeyapokea maamuzi hayo kwa mikono miwili siku zote makocha tunaajiriwa kwa ajili ya kufukuzwa," alisema Cheche.

Alisema alitarajia jambo hilo kutokea na kwamba maisha ya mpira ndivyo yalivyo "leo uko hapa kesho sehemu nyingine".

"Kipindi chote nilipokuwa na timu sijawahi kukutana na viongozi wa juu nilikuwa naonana na viongozi wa chini, maamuzi hayo huenda yametolewa na mtu mmoja ambaye alidhamiria jambo hilo," alisema.

Hata hivyo, aliwashukuru wadau wa Azam kwa ushirikiano waliompa katika kipindi chote alichokuwa na timu.

Cheche alianza kuinoa timu hiyo tangu ikiwa Ligi Daraja la Kwanza na ilipoanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2008/2009 hadi kibarua chake kinafikia ukingoni juzi amekuwa akikinoa kikosi cha vijana cha Azam kwa vipindi tofauti.

Mbali na Cheche, pia msemaji wa klabu hiyo, Jafarry Maganda amebadilishiwa majukumu na sasa anasubiri kupangiwa kazi nyingine.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >